ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Sita – Tarehe 22 Febuari, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Machano Othman Said: (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Sheria Utawala na Idara Maalum kwa mwaka 2016/2017.

Utaratibu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 37 kuuliza muongozo mzima wa kazi za shughuli za leo. Nina barua ambayo nimepewa na Baraza la Wawakilishi ambayo inasema kwamba swali langu namba 53 litaulizwa leo tarehe 22, lakini katika *Order Paper* ya leo swali langu halipo. Naomba muungozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Subiri tuangalie utaratibu. Subiri kidogo. Mheshimiwa Mjumbe zungumza na kiti swali namba ngapi unalodai.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Swali namba 53 Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Waziri lete ufafanuzi wa jambo hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu niliokabidhiwa rasmi kwa siku ya leo ni suala zima la *Order Paper* kama kuna barua yoyote aliyoandikiwa na Katibu yeye arudi kwa Katibu amuone kwa nini. Lakini hapa sisi tunafuata *Order Paper* na ndio utaratibu Mhe. Mwenyekiti, na huwezi kuhoji *Order Paper* ambayo tayari ina baraka zako zote za Spika. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante pamoja na kwamba siwezi kuhoji na imebidi nihoji kama tatizo liko kwenye Baraza la Wawakilishi mmeshindwa kutupa semina namna gani vya kufanya. *Order Paper* siwezi kuhoji lakini tarehe humu wameniandikia tarehe 22 nihoji wapi au nizungumze wapi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe hilo swali lako litaangaliwa kwa namna nyengine. Kwa vile Katibu ameshatuletea swali lako litaangaliwa na Katibu kama litakuwa limekosekana leo, litaangaliwa utaratibu mwengine. Naomba tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa lakini ilikuwa nipewe taarifa mapema.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba tuendelee.

MASWALI NA MAJIBU

Nam 108

Nyongeza ya muda kwa watumishi Wastaafu Vikosi

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa Mjumbe ninakushukuru sana kwa kujali muda na wengine tufanye hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ili tufanye shughuli zetu kwa utaratibu mzuri lazima ndani ya Baraza lako tukufu kuwe na nidhamu, mazungumzo yaende kutokana na taratibu za Baraza wananchi wa nchi hii wote wanatusikiliza sisi hapa kinachoendelea sio sehemu ya mazungumzo mengine zaidi ya mambo yaliokuwemo ndani ya *Order Paper*. Mhe. Mwenyekiti, naomba utaratibu wako ili shughuli ziende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa taarifa tumeisikia hiyo na mimi ndio pale ninaposema swali linapoulizwa hata kama ni mtu mwengine lakini majibu ni kwetu sote. Kwa hivyo, itaepusha ile kujibu maswali wakati jawabu imeshatolewa kama tutakuwa watulivu. Ahsanteni. Tuendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, sijamuaelewa bado Mheshimiwa Mjumbe ni lipi ambalo anataka ajibiwe ni 107 au 108.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi sikusikia vizuri huku. Lakini swali ambalo nimepatiwa majibu ni swali namba 108 kwa hiyo 107 lijibiwe.

Nam. 107

Madiwani kutopata nyongeza ya posho muda mrefu

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza**:**

Kwa kuwa Posho la Madiwani halijaongezwa tokea utawala wa Awamu ya 5 na kwamba Madiwani wanastahiki kuongezewa maposho kulingana na kuongezeka kwa makusanyo.

(a) Je, makusanyo ya Manispaa yameongezeka kwa asilimia ngapi kwa 2015/2016.

(b) Je, ni asilimia ngapi ya maposho ya Madiwani yaliongezeka.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Omar Seif Abeid wa jimbo la Konde swali lake Nam. 107 lenye vipengele (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamjibu Mheshimiwa mjumbe naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, Serikali za Mitaa Zanzibar zimeendelea na utaratibu wa kulipa posho wakati wa vikao na kila mwisho wa mwezi kwa Waheshimiwa Madiwani wake. Viwango vya malipo ya posho hizo vimekuwa vikiongezeka na kutofautiana baina ya Halmashauri moja na nyengine, hii inatokana na kutofautiana pia na viwango vya makusanyaji wa mapato. Kwa zile Halmashauri ambazo viwango vyake vya makusanyo vya mapato. Kwa vile Halmashauri ambazo viwango vyake vya makusanyo ni makubwa vile vile na maposho yao wanayolipwa kwa Waheshimiwa Madiwani navyo vinakuwa vikubwa ukilinganisha na Halmashauri ambazo mapato yake ni madogo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi sasa kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ naomba kumjibu kama Mhe. Mwakilishi swali lake namba 107 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa Fedha 2015/2016 makusanyo ya fedha kwa Manispaa ya Mjini yaliongezeka kwa asilimia 10 kutoka TZS. 2.069 bilioni zilizokusanywa mwaka 2014/2015 hadi kufikia TZS. 2.289 bilioni zilizokusanywa katika kipindi cha mwaka 2015/2016. Kwa upande wa Manispaa ya Magharibi 'B' makusanyo ya mapato yaliongezeka kwa asilimia 34 kutoka TZS. 950,000,000/- zilizokusanywa mwaka 2014/2015 hadi kufikia TZS. 1,269,583,000/- zilizokusanywa katika mwaka wa fedha wa 2015/2016. Kwa ujumla wake makusanyo ya Manispaa zote mbili yaliongezeka kwa asilimia 17 kutoka TZS. 3.019 bilioni kwa mwaka 2014/2015 hadi kufikia TZS. 3.558 bilioni katika mwaka 2015/2016.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kufuatia kuongezeka kwa makusanyo katika Manispaa hizo viwango vya posho kwa Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa hizo navyo vimeongezeka. Takwimu zinaonesha kuwa viwango vya malipo ya posho vya Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Mjini vimeongezeka kwa asilimia ishirini (20%) kwa mwezi katika mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Manispaa ya Magharibi 'B' viwango vya posho kwa Waheshimiwa Madiwani navyo viliongezeka kwa asilimia ishirini na tano (25%) katika mwaka wa 2015/2016. Sambamba na hilo, viwango vya posho kwa ajili ya vikao vya Mabaraza ya Madiwani na vile vya Kamati za Kudumu navyo pia vimeongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, Takwimu hizi zinaonesha namna ambavyo posho za Waheshimiwa Madiwani zimekuwa zikiongezeka kulingana na mapato ya Manispaa husika, hivyo si sahihi kusema kuwa posho la Madiwani halijaongezwa tokea utawala wa awamu ya tano.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa nini serikali haiweki kiwango kimoja cha posho la Madiwani wakati wote wana majukumu sawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi alitaka kujua ni kwa nini viwango vya maposho hayo ya Waheshimiwa Madiwani hatuwezi kuweka katika mfumo mmoja yaani kukawa na usawia.

Mhe. Mwenyekiti, mabaraza yetu au katika utaratibu wa Tawala za Mikoa kumekuwa na utaratibu huo ambao unatokana na miongozo lakini sambamba na hilo kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi kwamba hii ndio ambayo kwa kweli inategemeana na makusanyo na suala lile ambalo kwa kweli amesema kwamba kwa nini hatuweki usawia. Ushauri huu niseme kwamba ni mzuri lakini unahitaji kuwa na muda na kuangalia na hali halisi na mazingira ambayo tuliokuwa nayo.

Lakini napenda nichukuwe fursa hii kumwambia tena Mheshimiwa Mwakilishi ushauri huu tutauchukua tutauzingatia na tutakaa na wadau tukiona kwamba ipo haja ya kufanya hivyo basi nadhani ni jambo ambalo kwa kweli haliwezi kuwa na mashaka kwa upande wa Tawala za Mikoa.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba Madiwani wana mazingira magumu sana ya kufanya kazi. Lakini pia kutokana na hivi vijiposho ambavyo wanavipata muda mwengine havina uhakika wa hayo makusanyo ambayo yanakusanywa ndani ya hizo Halmashauri.

Je, wizara imejipanga vipi kuwasaidia angalau vile viusafiri vidogo vidogo japo vya maringi mawili hawa Madiwani wetu kwa ajili ya kujisaidia katika kufanya kazi zao kwa umakini zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba katika kipindi cha hapo nyuma kulikuwepo na hali kama hizo kwamba kutokana na mapato au zile posho ambazo walistahiki Waheshimiwa Madiwani wazipate kulikuwa na kusuasua. Lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba kwa sasa hivi wizara yetu imekuwa na mkakati madhubuti na endelevu katika kuona kwamba jambo hilo halitokei na badala yake kuona kwamba viwango vya maposho Waheshimiwa Madiwani wetu vimekuwa vikiendana kwanza na wakati lakini vile vile utaona kwamba vinakuwa vinaimarika zaidi na hili linatokana na msingi mzima wa kuhakikisha kwamba tunahimiza zaidi katika vile vianzo vyetu ambavyo vya makusanyo ambavyo vina uhakika basi kuweza kuvisimamia.

Lakini sambamba na hilo kukusanya kwa uwazi na mambo mengine yanayofanana na hayo. Kwa maana hiyo, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba mkakati tunao na unaendelea na hilo jambo kwa sasa naamini kwamba litakuwa ni historia na halitakuwa na taarifa kama hizo. Ila bado itabakia pale pale kiwango bado cha kupishana kinaweza kuendelea

kuwepo mpaka pale ambapo tutaona tunakuwa na utaratibu mwengine ambao utaweza kusaidia zaidi.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa mameya wote na wenyeviti wa Halmashauri katika maboresho ya Serikali za Mitaa walisema watawapa mshahara.

(a) Naomba anithibitishie Mhe. Waziri hawa Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri tayari wameshaanza kupata posho za mishahara.

(b) Mameya wote wanatakiwa wapeperushe bendera, lakini baadhi ya mameya hatuwaoni kuwa na usafiri wa uhakika wa magari yale ambayo yanapeperusha bendera zao. Je, wizara ina mpango gani wa kuhakikisha Mameya wote wanapatiwa magari kwa ajili ya kupeperusha bendera zao katika Manispaa zao.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Waziri utajibu swali namba moja la pili litakuwa limepita kanuni masuala yatakuwa manne.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba alirejee hilo swali namba moja.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud:

(a) Mamea na Mwenyeviti wa Halmashauri katika uboreshaji wa Serikali za Mitaa waliamua watalipwa mishahara. Je, Mamea hawa tayari wameshaanza kulipwa mishahara yao.

(b) Hawa Mamea wanatakiwa wapeperushe bendera, Je, serikali tayari imeshawanunulia magari kwenye Manispaa hizo kwa ajili ya kupeperusha bendera zao kwenye maeneo yao ya Manispaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu nilivyokufahamu nitajibu lile (a) kama ulivyotaka nijibu.

(a) Kuhusu suala la mishahara kama ambavyo kwa kweli amesema Mameya wetu ambao waliahidi kwamba watalipwa mishahara. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mwakilishi jambo kama limezungumzwa au kama limesemwa nataka nikuhakikishie tutalifanyia kazi.

Kuhusu kuanza utaratibu unaendelea na wakati wowote kama hili jambo kwa kweli kama limesemwa basi tutaona kwamba hilo linafanyika kwa mujibu wa miongozo na kanuni za mabaraza hayo au za Manispaa hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa majibu ya zaida ambayo yameuliza swali la nyongeza. Kwanza nataka niendelee kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa ndani ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, Mabaraza ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri ni vyombo ambavyo vipo kwa mujibu wa sheria Na. 7 ya mwaka 2014, utaratibu wake uendeshaji wake umeelezwa wazi wazi ndani ya Sheria hiyo Na. 7 ya mwaka 2014. Hivyo basi Waheshimiwa Madiwani wanastahiki kulipwa maslahi yao kama posho zao kwa mujibu wa sheria hiyo na hakuna Diwani yoyote wa Zanzibar ambae hapati stahiki zake zilizopo kwa mujibu wa Sheria. Lakini kwa wale Madiwani ambao wanahitaji usafiri kama wa vipando utaratibu umewekwa ndani ya Mabaraza hayo namna gani wanaweza kupatiwa vipando kama tunavyopatiwa vipando sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kiwango cha uwezo wa posho zao.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mameya ambao wamechaguliwa hivi karibuni wa Manispaa ya Magharibi (A) na Magharibi (b) wanaendelea kupata stahiki zao kama utaratibu wa kisheria unavyoruhusu.

Kuhusu suala la magari naomba nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba Magari ya Waheshimiwa Mameya yatanunuliwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018 na hivi sasa Mameya wanafanyiwa utaratibu wa kuazimiwa gari za Serikali ili waweze kupata usafiri wa kufanya shughuli zao. Ahsante sana.

Nam. 75

Utunzaji wa Makumbusho Chambani

Mhe, Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:-

Kumekuwa na kumbukumbu katika Jimbo la Chambani kama vile Mgagadu ambako ipo miembe ya makumbusho mjini Chambani na Jambangome.

Je, Mhe. Waziri unazijua kumbukumbu hizi na kama unazijua Wizara yako inachukua hatua gani katika kuhamasisha utunzaji wa kumbukumbu hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Bahati Kombo Khamis wa Jimbo la Chambani swali lake swali lake nambari **75** kama ifuatavyo:-

Ni kweli maeneo aliyoyataja Mheshimiwa kuna kumbukumbu nyingi, na ndio Serikali ikayatangaza rasmi kuwa maeneo yanayo hifadhiwa kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imechukuwa hatua kadhaa ya kuyaendelea maeneo hayo kwa kushirikiana na vikundi vya kijamii vya uhifadhi wa Mambo ya Kale kwa ajili ya kuimarisha na kutunza kumbukumbu zetu.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mfano katika eneo la Chambani kuna kikundi cha uhifadhi wa eneo hilo la kihistoria na waliwahi kupata msaada wa Mradi wa *MACEMP/TASAF* kwa ajili ya kuimarisha na kutunza kumbukumbu hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni matengenezo ya Msikiti mkongwe na Makaburi yalifanywa na kikundi cha uhifadhi cha Chambani kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zetu kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Vile vile kituo cha elimu kilijengwa katika eneo hilo la Chambani kwa ajili ya kuweka Makumbusho ndogo itakayoendeleza historia ya eneo hilo kazi ambayo inaendelea kufanyiwa utafiti zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya tafiti mbali mbali, kwa ajili ya kupata ushahidi wa kutosha wa baadhi ya maeneo hayo ya kihistoria likiwemo eneo la Miembe ya kihistoria la Mgagadu ili iweze kupata taarifa rasmi na sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, Kazi hizi za tafiti kwa upande wa maeneo ya Jambangome na Mgagadu zinaendelea, pamoja na kuhamasiha wananchi ili waelewe ya kwamba maeneo ya kihistoria ni rasilimali ya Taifa letu kwani bila utafiti huwezi kutoa maelezo ya kina.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza Mhe. Waziri katika jibu lake mama amesema kwamba katika eneo hilo la historia Chambani waliwahi kupata mradi wa *MACEMP/TASAF*.

a) Je, Mhe. Waziri ni kiasi gani cha fedha walizozipata kutoka *MACEMP* na *TASAF*.

b) Kutokana na hali ilivyo lilivyo hivi sasa jengo hilo la historia umejipanga vipi kuliimarisha na kuonekana kweli ni jengo la Historia.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu mama kwamba kikundi kile kimepata msaada kutoka *MACEMP* na Idadi ya Fedha ambazo wamezipata kutoka *MACEMP/TASAF* ni Milioni 18 kwa ajili ya kuendeleza jengo lile, lakini pia na barabara inayoelekea katika maeneo yale ya kihistoria, msaada huu waliotoa ni *MACEMP* lakini wamewakabidhi *TASAF* kwa ajili ya usimamizi wa fedha hizi.

b) Mhe. Mwenyekiti, katika kuyaendeleza makumbusho haya Wizara ina mpango wa kuyaimarisha kwa kupitia vikundi vile ambavyo vipo katika maeneo yale ya kihistoria, lakini pia ina mpango wa kuyapatia hatimiliki kwani inaonekana kwamba maeneo yetu yote yale ya historia wananchi wanavamia na kwa kuwa hatuna hatimiliki wakati mwengine inakuwa ni vigumu kuwazuia.

Lakini vile vile Wizara pia ina mpango wa kuyatangaza maeneo haya ya historia kupitia sehemu ya utalii kwa kuyatangaza na kufanya *program* maalum kuyatangaza katika sehemu zetu za usafiri kama kwenye mashirika yetu ya ndege, yanayofanya kazi hapa Zanzibar na kwenda nchi za nje Wizara ina mpango wa kuandika matangazo na matangazo yale yatawekwa katika ndege zile ili wataalii wapate taarifa zile hatimae kufuatilia historia zetu.

Lakini vile vile napenda nichukue fursa hii nimpongeze Afisa Mdhamini Pemba kwa kuhakikisha kwamba sasa hivi ana mpango maalum na anasimamia makumbusho haya kwa kupanga programu maalum ambayo inasimamiwa pia na Mkuu wetu wa Idara ya Magofu na mambo ya kele kule Pemba, wametenga muda maalum yaani program ambayo wameipanga kila mwezi wanakuwa wanakwenda katika maeneo yale na wanachukua wafanyakazi wetu na kuyafanyia usafi maeneo yale ahsante.

Mhe. Hamida Abdulla Issa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza. Katika majibu yako Mhe. Waziri umesema kwamba kuna utafiti ambao unaendelea

katika maeneo ya Chambani na Jambangome. Je, utafiti huo umefikia wapi kwa sasa na lini utamalizika ili kutupatia ripoti kamili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ni kweli kwamba nimesema kuna tafiti ambazo zinatajwa kwa sehemu hizi mbili, kwa hivyo namuomba Mheshimiwa Mwakilishi kwamba utafiti kwa kawaida unakuwa na mpango maalum na hawa watafiti wetu pale wanapokuja suala la utafiti linakuwa la muda mrefu kidogo. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba utafiti huu utakapokamilika na wale watafiti watakapotuandikia ripoti nitahakikisha kwamba nimempa ripoti hii na yeye pia aione.

Mhe. Yussuf Hassan Idd: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa fursa ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwa eneo hilo la Makumbusho halijapatiwa hati miliki je ni lini Serikali itapata hatimiliki ya eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Kama nilivyoeleza kwamba sasa hivi tuna mpango wa kuyapatia maeneo haya ya kihistoria hatimiliki, naomba nimjibu kwamba, kwa kuwa Serikali ina taratibu na vyombo ambavyo vinashughulikia hatimiliki pia vina taratibu zake. Taratibu hizi zitakapokamilika kwani siwezi kumpa jibu nikamwambia ni lini hadi utaratibu ukamilike, nitahakikisha kwamba nitampatia maelezo au hati hizi nitakuja nazo kwa ajili ya ushahidi wa kutosha ahsante.

Nam. 81

Udhibiti wa Vitendo vya Udhalilishaji

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Zanzibar inajitahidi kuzuia matendo ya udhalilishaji kijinsia hasa kwa watoto na wanawake lakini hata hivyo mambo hayo kwa sasa yamekithiri.

(a) Je, Serikali imeweka mipango gani ya kuzuia au kumaliza kabisa udhalilishaji
huo.

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipiga marufuku kwa watoto wasiofikia miaka 18 kutembea nje ya nyumba yao baada ya saa 2 usiku. Je Sheria hiyo bado ipo na kama haipo tena ilifanya hivyo kwa madhumuni gani.

(c) Je, Serikali haioni kuwa kuwaachia watoto kutembea usiku ni kuongeza vitendo vya kubakwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-
Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti kwanza kabisa natanguliza shukrani zangu kwa Mhe. Mwakilishi kwa kutambua juhudi za Serikali inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein ya jitihada zinazochukuliwa na kuzuia matendo ya udhalilishaji wa kijinsia hasa kwa watoto na wanawake.

Mhe. Mwenyekiti kama tujuavyo na kwa nia njema kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein tarehe 06 Disemba, 2014 alizindua Kampeni ya Kupinga Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Kampeni hiyo ilikuwa na malengo yafuatayo:-

- Kukuza uelewa wa jamii juu ya suala la ukatili na udhalilishaji.
- Kuimarisha uwajibikaji kwenye ngazi mbali mbali katika kukabiliana na aina zote za ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.
- Kuimarisha uwezo wa taasisi na jamii katika kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, na .
- Kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za kupambana na ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Jimbo la Chake Chake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara yangu imeweka mipango madhubuti ya kuzuia na kumaliza kabisa udhalilishaji huo kwa kuandaa mpango wa miaka mitano wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hapa Zanzibar. Mpango huo utatoa matokeo ya aina tatu ambayo misingi yake mikuu ni kukinga, kutoa suluhisho la kudumu na mazingira wezeshi ya kuondokana na matendo hayo.

Mhe. Mwenyekiti mafanikio ya mpango huo yanahitaji ushirikiano wa pamoja wa taasisi zinazosimamia masuala ya udhalilishaji wa kijinsia,

jamii na sisi wanasiasa kwa kutoa taaluma ya kinga kwa wapiga kura wetu ili wasikizane na Sheria. Aidha suala la kutoa ushahidi linaonesha kuzorotesha kwa mienendo ya kesi hizo. Hivyo natoa wito kwa jamii kushirikiana kwa kutoa ushahidi katika kesi za udhalilishaji pale inapohitajika.

(b) Mhe. Mwenyekiti kuhusu Serikali kupiga marufuku kwa watoto wasiofikia miaka 18 kutembea nje ya nyumba zao baada ya saa 2:00 usiku ni kwamba Serikali haijapiga marukufu kwa watoto wasiofikia miaka 18 kutembea nje ya nyumba yao baada ya saa hizo.

Mhe. Mwenyekiti Serikali kupitia Wizara ya Elimu ilisitisha utoaji wa mafunzo ya ziada kwa wanafunzi *(tuition)* mwaka 2008 kutokana na sababu mbalimbali mpaka itakapotoa utaratibu rasmi wa kuendelea na mafunzo hayo. Toleo hilo lilisambazwa kwa Walimu Wakuu wa Skuli zote Unguja na Pemba na linaendelela kufanyakazi, bado halijafutwa.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna Sheria inayopiga marufuku kwa watoto wasiofikia miaka 18 kutembea nje ya nyumba zao baada ya saa 2.00 usiku, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kipindi hicho alichukua uamuzi huo ili kuzuia matendo maovu kwa wanafunzi na mambo mengine yanayofanana na hayo. Aidha matangazo kama hayo pia yamewahi kutolewa na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini wa Magharibi hasa kwa siku za sikukuu na kadhalika, Wizara yangu inaunga mkono matangazo hayo ili kuepusha vitendo vya uzalilishaji wa kijinisia hasa kwa wanawake na watoto. Pia nachukua fursa hii kutoa wito kwa wazazi na wazee kuwasimamia watoto ili wasizurure ovyo wakati wa usiku.

c) Kuhusu watoto kutembea usiku ni kuongeza vitendo vya kubakwa ni kwamba Serikali kupitia Wizara yangu inatambua kuwa watoto kutembea usiku ni kiashirio cha matendo ya kubakwa. Hata hivyo vyanzo vya taarifa vinaonyesha kuwa matendo ya ubakaji yanatendeka zaidi wakati wa mchana ambapo wazazi na walezi wako kwenye harakati nyengine za maisha. Aidha ukimya masafa marefu ya kufuata masomo vyuoni na mashuleni pamoja na mazingira ya pori yanachangia kufanyika kwa matendo hayo. Aidha hadaa kama vile fedha na zawadi mialiko ya maeneo mbali mbali na makaazi nayo huchangia kutendeka kwa matukio hayo zaidi wakati wa mchana.

Mhe. Mwenyekiti, majibu yangu hayo hayahalalishi watoto kuachiwa kutembea usiku tahadhari inahitajika kwa wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi lazima nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu la nyongeza ambayo katika majibu yake ni kwamba katika ukumbuko wa maisha yangu ya utoto serikali hii hii ilikuwa ikiwakamata watoto kufika saa mbili za usiku kwamba wasionekane ikiwezekana hivyo utamkuta mtoto wako katika vyombo vya sheria. Suala hili amelijibu kwamba lilikuwa si sheria au lilikuwa halipo kama lilikuwa si sheria na kama lilikuwa halipo.

(a) Je, yeye suala hili kama ni kuona kwamba ni moja ya vichocheo ataleta lini mswada huu wa kubadilisha ili hii iwe sheria angalau kupunguza matatizo haya.

(b) Mheshimiwa hili la uvaaji wa nguo. Uvaaji wa nguo ni moja wa mambo ambayo hata Uisilamu na hata katika dini zote umebinya sana kwamba wanawake wajifunike vizuri sana ili kupunguza hamu na mambo mengine ambayo yanaweza kuvutia. Sasa ili kuondoa tatizo hili ambalo linasababisha sana mambo ya bilisi ni atatoa tamko la atakaevaa nguo ambayo haikidhi haja atakutana na vyombo vya sheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, Mheshimwa Mwakilishi kwanza amesema ni lini tutaleta sheria hapa nataka nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi.

(a) Tutakaa na kuangalia tukiona kwamba ipo haja ya kuleta hiyo sheria anayoitaka basi hatutopinga tutaleta sheria hiyo ipitishwe iweze kufanya kazi.

(b) Kuhusu suala mavazi ndio yanayosababisha kutokea kwa vitendo hivi. Mimi nataka kumwambia Mheshimiwa Mwakilishi kwamba nafsi ya mtu huwezi kuizuia hata ukavaa nguo vipi ikiwa mtu huyo ni mkorofi basi haiwezi kufanya sababu ile ya nguo ikamfanya mtu yule akaepukana na lile tendo. Kwani tunaona na tunashuhudia kwamba wengi humu wanavaa nguo za heshima na wanajisitiri lakini hatima yake wanafikwa na matendo kama hayo. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri tatizo la udhalilishaji wa watoto hapa kwetu Zanzibar linaongezeka siku hadi siku na kwa kuwa taasisi binafsi na watu binafsi wamefanya kazi ya ziada na ya kujitolea kupita ziara mashuleni Unguja na Pemba na kuwatambua wale baadhi ya watoto waliofanyiwa kadhia hiyo.

(a) Je, serikali lini imefanya ziara mashuleni na vyuoni kuwatambua watoto waliofanyiwa kadhia hiyo

(b) Watu gani ambao wamewafanyia kadhia hiyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu tayari imeshaanza hiyo kazi ya kupita kwenye maskuli na kuwatambua wale watoto ambao wamefanyiwa mambo hayo ya udhalilishaji.

Mheshimiwa naomba kidogo urudie suala la pili.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, ni lini mmepita maskulini na kuwatambua watoto lakini pia na hatua gani mmechukuwa kwa hao waliowafanyia watoto vitendo hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, swali la mwanzo kama nilivyojibu kwamba wizara yangu tayari imeshaanza hiyo kazi ya kupita maskulini kwa kushirikiana na Wakuu wa Wilaya pamoja na walimu wakuu wa skuli hizo. Kuhusu suala la hao wanaofanya vitendo hivyo, ni kwamba tayari wameshajulikana na wako kwenye vyombo vya sheria tunaiachia sheria ichukuwe mkondo wake.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukuwe fursa hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini swali la udhalilishaji ni suala ambalo linatuumiza sana wazazi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri katika majibu yake amesema wizara tayari imendaa mpango ambao utaweza kutoa majibu ya aina tatu. Lini mpango huo utaanza ili kuondosha kabisa vitendo hivi vya udhalilishaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nakubalina na Mheshimiwa kwamba suala la udhalilishaji watoto linamuumiza. Napenda na mimi nimuhakikishie kwamba wanawake wote hili suala linatuumiza na kama alivyoniuliza kwamba ni lini mikakati hiyo tuliyoipanga wizara lini itaanza kufanya kazi. Nataka nimuhakikishie

Mheshimiwa Mwakilishi kwamba mara tu baada ya kukamilika vizuri mpango wetu wakati wowote suala hili litaanza kufanyiwa kazi. *Inshaallah*.

Utaratibu

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Kifungu 66(1)(a) na 135(3)(b) Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kuomba utaratibu katika vifungu hivyo Mjumbe Mhe. Jaku Hashim Ayoub hakutimiza matakwa ya kanuni hizo na naomba Mhe. Mwenyekiti, kiti chako kitoe muongozo.

Ukisoma Kanuni ya 66(1)(a) inamtaka kila Mjumbe ajenge heshima ya chombo hichi. Lakini ukisoma Kanuni ya 135(3)(b) inamtaka Mhe. Mjumbe namna ya mavazi ya kuvaa katika kujenga heshima ya chombo chetu. Mhe. Mjumbe ameshindwa kuendana na kanuni hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Waziri kwa bahati sijapata vizuri Kanuni uliyoitumia.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimeomba utaratibu Mhe. Mjumbe ukisoma Kanuni ya 66,(1)(a) inataka Mjumbe alinde heshima ya chombo hichi. Ukisoma Kanuni ya 135(3)(b) imeelezea mavazi. Mhe. Mjumbe amekuja amevaa Kaunda Suti bila ya kuvaa buti. Kwa mujibu wa Kanuni anatakiwa avae buti, unapovaa Kaunda Suti na hutakiwi kuvaa viatu vya wazi isipokuwa utakapokuwa umevaa kanzu kofia na koti, Mhe. Mjumbe ameshindwa kuendana na Kanuni kama utaratibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Waheshimiwa Wajumbe naomba utulivu kidogo. Mjumbe aliyetajwa kama yupo atoke nje kwa kwenda kutimiza masharti ya Kanuni.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mtaje Mjumbe muhusika.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza Mjumbe mimi aniombe radhi, Waziri kwa kunidhalilisha vyenginevyo sitokubali mimi. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub kaa kitako. Mhe. Jaku Hashim Ayoub fanya utulivu. Waheshimiwa Wajumbe utulivu upatikane katika ukumbi. Naomba utulivu tusipoteze muda.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimedhalilishwa sasa hivi na wananchi wamenichagua kwa kuniamini kuja hapa, kama hakuniomba radhi Waziri huyu anaongoza wizara hii mimi sitokubali.

Nimechaguliwa na wananchi na nina dhamana kwa wananchi sikupata jimbo Ikulu mimi. Kwa hivyo Waziri asimame aniombe radhi huku ni kudhalilishana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub kaa kitako. Wajumbe tunaendelea. Waheshimiwa naomba utulivu. Mhe. Jaku Hashim Ayoub nakuomba ukae kitako usubiri kwanza.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, niliposimama nilisimamia Kanuni ya 66(1)(a) na nikakuomba sana Mhe. Mwenyekiti na naomba niinukuu:-

Mjumbe pamoja na wajibu alionao chini ya vifungu vya Katiba atakuwa pia na wajibu wa mambo yafuatayo:-

a) Kulinda hadhi ya Baraza la Kamati zake na kutojiingiza kwa namna yoyote ile katika vitendo vya makusudi ya kutoliheshimu Baraza na kusababisha Baraza na Kamati zake kudharauliwa.

Na niliponukuu kanuni ya 135(3)(b) nikamaanisha mavazi. Mhe. Mwenyekiti, mimi sijapata matatizo ya kutokuona vizuri nimemuona kwa macho yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameingia ukumbini amevaa viatu vya kubadhi, kwa maana ya kuwa viatu vya wazi. Kilichotendeka ni mambo ya kitoto kabisa katika kuliondoshea heshima Baraza lako.

Kwamba Mjumbe mwenzake anavua viatu vyake anampa Mhe. Jaku Hashim Ayoub ili aendane na Kanuni huku si kumsaidia ni kumpotosha na hulipotoshi tu Baraza, unaipotosha nchi na chombo hichi. Kwa sababu chombo hichi kipo kwa mujibu wa Katiba na ndio maana nikanukuu Kanuni ya 61(1) kwa kujenga

heshima ya chombo hiki ukitenda kinyume maana yake unalivunjia heshima Baraza lako Mhe. Mwenyekiti.

Hapa hatukuja kushindana lazima tuongozane kwa msingi wa kujenga heshima, nidhamu na utulivu. Taswira yetu sisi Wawakilishi ndio watu tunaowaongoza wanavyopata kuona namna gani tunaweza kuiongoza nchi huwezi ukatufanyia mambo ya kihuni kwa kuja kuvaa makubadhi kinyume na utaratibu. Ukitaka kuvaa makubadhi vaa mavazi yanayoendana kwa mujibu wa kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, sikusudii kuwa tuko Mahakamani kwamba mwenzangu atafute ujanja wa kuingiza wakili, ujanja wa kushinda kesi hapana si utaratibu Mhe. Mwenyekiti, kwamba mtu atoke kule aje mbele hii sehemu ya kulivujia heshima Baraza lako na mategemeo yangu kwamba kiti chako kitalisimamia vizuri. Tumekuchagua kwa heshima, tumekuchagua kwa kutambua uwezo wako na tunaomba Mhe. Mwenyekiti usimamie kanuni katika kuongoza chombo hichi. (*Makofi.*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub sijakuruhusu naomba ukae. Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri alizungumzia suala la nidhamu na ni sahihi kama kitendo hicho kilifanyika ni kitendo cha kukilaani kabisa. Kama Mjumbe aliazimwa au amefanya vipi lakini Mhe. Waziri aliona hicho kitu na ndio akakitolea ufafanuzi. Kwa hivyo, ili tusiendelee na mjadala huu naomba tuendelee. (*Makofi*)

Nam. 57

Kuzuiwa Wavuvi Kuvua Majongoo na Kome

Mhe. Suleiman Makame Ali - Aliuliza**:-**

Kumejitokeza tatizo kubwa kwa wananchi wetu ambao ni wavuvi wa majongoo na makome kwa kuzuiwa kuvuwa mazao hayo wakati ambapo kazi hiyo inategemewa na watu wengi katika kuwapatia kipato na kupambana na maisha yao ya kila siku.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia kazi nyengine wananchi hao ambao wanategemea bahari na wanavua uvuvi huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake nambari 57 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti**,** Wizara yangu kupitia Sheria Namba 7 ya 2010 imekataza matumizi ya mitego ya juu, vifaa vya umeme na vifaa vya kuzamia ikiwemo chupa za gesi, viatu vya baharini na matumizi ya vioo vya baharini, hii ni kwa sababu ya kuzuia uvunaji haramu wa rasilimali zinazotoweka baharini na uharibifu wa matumbawe ya baharini. Ili wananchi wapate kazi za ziada katika kipindi ambacho hawaruhusiwi kuzamia.

Na kwa kuvuna rasilimali za majongoo na makome, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia sheria nilioitaja haikupiga marufuku ufugaji wa Mazao hayo ya baharini yakiwemo majongoo, kaa samaki na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, Ili kuthibitisha ninayoyasema Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi hadi hivi sasa imeweza kuhamasisha mpango huo wa ufugaji kwa vikundi 16 vinavyojishughulisha na ufugaji wa mazao hayo, kati ya hivyo 6 wanafuga majongoo na wanapewa vibali vya kusafirisha wakati wowote wanapotaka.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba hawajazuia lakini mimi nasema wamezuia kwa sababu hawavui mimi ni shahidi kule Ndagoni wamekuja kunifuata na wakanieleza hili suala na mimi mwenyewe ni shahidi wa hilo. Lakini pia nataka kujua ni Majongoo aina gani ambayo kwamba yanastahiki kufugwa, kwa sababu kuna jongoo wengine hawastahiki kufugwa kwa sababu kuna Jongoo wengine hawastahiki kufugwa ni jongoo wa aina gani aweze kunambia Barango, Tairi, Mweupe au Kijino ni jongoo wa aina gani anastahiki kufugwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema majongoo hayajakatazwa kuvunwa isipokuwa kwa majongoo maalum na kwa vile vifaa na yule ambaye anafanya *diving* hao ndio wanakatazwa.

Vile vile majongoo ambayo yanayoruhusiwa kufugwa ni *holothuria nobilis, Thelenota Ananas. holothuria lessoni and holothuria scabra* hao ndio wanaoruhusiwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa majibu yake mazuri. Asili ya Wazanzibari wanaoishi ukanda wa Pwani wanategemea bahari kwa uvuvi

mbali mbali. Lakini moja wapo Mheshimiwa suala la uvuvi wa majongoo kuna wachuuzi na wavuvi wengi wanalalamika kwamba imezuiliwa kabisa.

Je, kwa kuwa hili Mheshimiwa anasema halipo na mimi nahakikisha lipo Mhe. Waziri yuko tayari akakutane na wavuvi na wanunuzi majongoo wanalalamika kwamba wamefungiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema vibali hatujakataza vya kusafirisha majongoo na vile vile nipo tayari kuonana na wavuvi hao ili tuweze kujua ni kweli wamekatazwa ama laa.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifungo na Uvuvi. Mhe. Waziri alipojibu suala mama alizungumzia kama yeye bado hajazuia uvuvi wa majongoo wala makome na mengineyo. Lakini hapa alizungumzia kama amezuia uzamiaji kwa kutumia miwani na vifaa vyengine vya *gas* lakini haoni kama anapozuia miwani kuigilia katika bahari, huoni ndio amezuia vifaa vyote kutumia katika bahari kwa uvuvi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama nimemuelewa vizuri Mhe. Mwakilishi swali lake tulichokizuia ni uharibifu wa matumbawe na uharibifu wa matumbawe watu wanatumia kwa ku-*dive* ndani ya maji. Vile vile tumekataza ile miwani ya kioo kuingia nazo pamoja na kuvaa vile viatu, hicho ndio tulichokikataza na tumekikataza kwa sababu ya kuharibu matumbawe ya samaki pamoja na mazingira ya bahari, ili tuweze kupata mazao mazuri basi lazima tuyatunze matumbawe yetu. Majongoo tumeruhusu yafugwe halafu yavunwe sio waende waharibu matumbawe. Ahsante.

Utaratibu

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 37 inasema, "Waziri wa Mjumbe yoyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi. Isipokuwa kwamba, swali aliloulizwa Waziri mmoja anaweza kulijibiwa na Waziri mwengine au na Mwanasheria Mkuu".

Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba wavuvi ambao wanavua majongoo hawajakatazwa kama alivyosema Mhe. Makame pale lakini sasa ili uvue

jongoo uvae ile miwani. Je, mvuvi huyo maji pima 20 atakwendaje kuvua jongoo na ulisema Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimesema majongoo yanafugwa na wanaruhusiwa kuvua. Tunachokikataza sisi ni yale matumizi ya kuvaa vile viatu na ile miwani ya kioo kwenda kuharibu matumbawe ya samaki na vifaa vyengine vya baharini.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Hii inaonesha wazi pamoja na kuwa tunamuona ni mwanamke lakini ana taaluma tosha kabisa ya mambo ya bahari.

Mhe. Mwenyekiti, alichokizungmza Mhe. Naibu Waziri ni sahihi. Kuna uvuvi ambao unatumia bunduki, unatumia vioo, unatumia hizo *clippers* ambazo unavaa ili ukafanye uvuvi ule. Lakini uvuvi ule ni uvuvi mkubwa sana ambao umepigwa marufuku kwenye sheria ya uvuvi hapa Zanzibar. Huo ndio Mhe.Waziri aliyoueleza wazi kwamba uvuvi huu umezuiliwa kuvua na uvuvi ule wa majongoo wazi ni kwamba lazima uvae kioo ili uweze kwenda kulichukua lile jongoo. Lakini uvuvi ule umehalalishwa ndani ya sheria. Kwa hivyo alichokizungumza Mhe. Naibu Waziri ni sahihi kabisa kwamba, watapovua uvuvi wa majongoo vioo ni lazima wavae ili kuliona lile jongoo kule chini. Lakini atapotumia vioo vyake na *clipper* zake ka kwenda kuvua uvuvi ambao umepigwa marufuku kwenye sheria uvuvi huo ndio uliokatazwa na ni wazi unaharibu matumbawe, unaharibu uzalishaji wa samaki na unaharibu mazingira ndani ya bahari.

Kwa hivyo hilo jibu alilolitoa Mhe. Naibu Waziri nilikuwa nataka kuliunga mkono kwamba liko sahihi.

Utaratibu

Mhe. Simai Mohammed Said: Nasimamia Kanuni ya 63(1) Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa wakati Mhe. Waziri anatoa majibu yake alitanguliza kauli moja ambayo kwa kweli kwa njia moja au nyengine haiendi sawasawa na Kanuni zetu. Moja ni kwamba alitamka ingawa mwanamke hii sio utaratibu wetu na hapa kama wenzangu mtakuwa mmemsikia hapa inabidi afute hiyo kauli na aliombe Baraza lako alitake radhi kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai sijakusikia neno lako la mwisho.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Waziri ameingia kumsaidia mchango au majibu aliyotoa Mhe. Naibu Waziri kwenye kauli yake alipoingia kati kati alisema ingawa mwanamke, hili neno haliendani kabisa na kwa kweli jinsi ya *spirit* ya Waheshimiwa Wajumbe kutoka humu ndani. Juzi hapa Mjumbe mmoja aliomba radhi na bila wasiwasi Mjumbe wenyewe ni pembeni yangu Mhe. Suleiman. Kwa hivyo neno alilotamka ingawa mwanamke haliko sawa kwa hivyo afute kauli aliombe Baraza radhi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijaona tatizo naona kanisifia kwa sababu anajua kwamba mimi sio mtu wa ku-*dive* na ndio maana akanambia vile, sijaona kama kuna tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe kwa sababu muhusika yeye mwenyewe hajaona kama ni udhalilishaji basi na kwa kweli aliitumia kwa nia safi kabisa, Kwa sababu Mhe. Waziri alitumia neno hilo si kwa udhalilishaji na muhusika hajaona kama ni udhalilishaji. Kwa hivyo tuendelee.

Nam. 35

Taratibu za Kupunguza Mmong'onyoko wa Ardhi

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Aliuliza:-

Kwa kuwa Miundombinu ni muhimu sana katika kukinga majanga mbali mbali yenye athari kubwa kwa maisha ya binaadamu. Na kwa kuwa ubunifu na uangalifu mkubwa huhitajika ili kuwa na miundombinu stahiki inayokidhi haja ya mahitaji ya kimaendeleo hasa kwa nchi kama yetu yenye ardhi ndogo inayoathiriwa sana na mmong'onyoko kupitia maji ya bahari na mvua ambayo husababisha mafuriko na hivyo kuleta hasara kwa Serikali na jamii.

(a) Je, Wizara yako ina utaratibu gani wa kupunguza au kuondosha tatizo hili la mmong'onyoko kwa kujenga miundombinu itakayosaidia kuihami ardhi hii.

(b) Je, kuna mpango gani utakaowezesha kutatua tatizo la mmon'gonyoko mkubwa unaoathiri makaazi ya wananchi kutokana na mafuriko na hata kuhatarisha miundombinu ya barabara ambayo inaelekea kupata athari za kubomolewa na maji yanayotiririka kwa kasi kuelekea daraja la Garagara katika Jimbo la Mtopepo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Dr. Makame Ali Ussi swali lake nambari 35 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kabla ya kumjibu swali hilo napenda kuungana na Mheshimiwa Mwakilishi kuwa Miundombinu ni muhimu sana katika kukinga majanga mbali mbali yenye athari kubwa kwa maisha ya binaadamu. Ni kweli ubunifu na uangalifu unahitajika ili kuwa na miundombinu stahiki inayokidhi haya ya majitaji ya kimaendeleo hasa kwa nchi kama Zanzibar ambayo ina ardhi ndogo inayoathiriwa na mmong'onyoko wa fukwe na mafuriko ambayo huleta athari mbali mbali za kimazingira, kiuchumi na zile za kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya maelezo hayo machache sasa naomba kumjibu swali lake kama ifuatavyo:-

a) Serikali kupitia Wizara husika imekuwa ikifanya juhudi kubwa za kujenga miundombinu ya mitaro ya maji ya mvua katika sehemu mbali mbali ili kuondoa maji hayo kwenye makaazi ya watu kwa lengo la kupunguza mmong'onyoko wa ardhi unaosababishwa na maji hayo na pia kuondoa mafuriko ambayo huleta maafa makubwa ya binaadamu, miundombinu na hupelekea kupotea kwa mali. Hivi sasa Serikali kupitia Mradi wa Huduma za Miji inaendelea na kujenga mitaro yenye ukubwa wa wastani wa kilomita 19.6 katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hayo Serikali pia inaendelea kadri ya uwezo unavyojitokeza kujenga kuta kwenye fukwe kwa ajili ya kuzuiwa mmong'onyoko wa fukwe. Katika maadhimisho ya Sherehe ya Mapinduzi za mwaka huu, Serikali ilizindua ukuta uliojengwa katika eneo la Mizingani wenye urefu wa mita 340. Aidha, Serikali pia inaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa watu mbali mbali wanaojenga kuta katika maeneo yao ya fukwe kwa ajili ya kukinga mmong'onyoko wa fukwe. Kwa kuwa sio kila ujenzi wa kuta za fukwe utakuwa unazuia mmong'onyoko wa fukwe naomba nichukue nafasi hii kuwaomba wananchi na wawekezaji wote ambao wanataka kujenga kuta za kuzuia mmong'onyoko wa fukwe basi wawasiliane na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya kupewa muongozo husika.

b) Kwa kuwa suala hili ni maalum katika eneo lake, naomba nilichukue suala hili kwa ajili ya kufaanya ziara ya pamoja na Mheshimiwa Mwakilishi husika pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ili kuona hali ilivyo kwa hatua zinazofaa.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mahiri na makini kama nilivyoomba anijibu. Nasema visiwa vyetu vya Zanzibar kwa kweli ni visiwa vidogo sana. Ukiangalia matokeo ya tabia nchi hivi sasa duniani, huko *North Pole* huko juu huko ambako kuna barafu inayopoza dunia sasa hivi inayayuka kwa kiwango kikubwa. Maji yale ya barafu yanayayuka kutoka huko *North Pole* yanakwenda pwani, kina cha bahari kinaongezeka. Isitoshe wenzetu wanafukia ardhi siku hizi kwa wingi sana, ukienda Dubai kuna Kisiwa cha Mtende wamefukia bahari, ukienda Uholanzi kuna sehemu zimefukiwa bahari mashamba makubwa makubwa wanajenga majumba na kadhalika. Ni kwamba maji yale yote yaani kufukia bahari na hayo maji yanaongezeka yote yanatafuta pa kwenda.

Sasa sisi hapa Zanzibar kwa kweli utaratibu wa kuzuia mafuriko ya aina hiyo haujakuwepo, mwaka wa 1980 nakumbuka

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa twende kwenye swali.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Nafafanua ili aweze kujua swali apate kunijibu vizuri. Ni kwamba bahari inakula kwa wingi sana ardhi yetu lakini sisi kile kiwango cha ku-*reclaim* ile ardhi ni kidogo sana. Kwa hivyo mimi ninaishauri sana Wizara hii ya Ardhi ifanye utafiti wa kutosha ili kujikinga na majanga haya ya mafuriko. Sasa likija likitokezea hilo tuwe tumejikinga ipasavyo kabisa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa uliza swali.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mimi ilikuwa wangu ni ushauri tu kwamba tujitahidi.

Mhe. Mwenyekiti: Hapo si pahali pake.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Mpendae ni moja lililoathirika na

mabadiliko ya tabia nchi sehemu ya Kilimani. Vile vile maeneo haya yamekumbwa na bahari kwa kiasi kikubwa. Tumefanya ziara mbali akiwemo Waziri wa Ardhi, Waziri wa Miundombinu na Wakurugenzi wao wote na kutoa ahadi mbali mbali kuwa tayari tutaweza kujenga ukuta lakini na kuona mmon'onyoko uliotokea utarejebishwa. Nataka kuuliza ni lini Serikali itakuwa tayari kuwaonea huruma wananchi wa Shehia ya Kilimani kwa maafa makubwa ambayo yanawakuta.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la nyongeza hili la pili naomba niseme kwamba nimechukua ushauri wa Dkt. Makame Ali Ussi Mwakilishi wa Mtopepo na baada ya hapo basi napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Mpendae kwamba kama alivyosema Serikali imekwenda kuangalia na haikwenda tu bure imekwenda kwa dhati kwa sababu ya kukabiliana na matatizo ambayo tunayo ya kimazingira na nimwambie miongoni mwa mambo ambayo yatafanywa au maeneo ambayo yatafanywa ni Magomeni, Mpendae, Kwabinti Amrani, Migombani, Kilimani tunategemea mita elfu nne mia sita ishirini na nane zitajengwa.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafsi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza ninampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuanzisha mradi wa majumba kule Fumba Town, juzi nilikwenda kutembelea zile nyumba, nilipofika nilijionea kama kuna nyumba ambazo zimeanzishwa kwa ujenzi wa *cyprus* pamoja na manila kwenye viambaza. Je, Wizara yako kwa kuwa hali ya mmon'gonyoko wa ardhi inasababishwa na wajengaji wengi ambao wanachimba mchanga. Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwashajiisha wananchi kuachana na hali ya kutumia matumizi ya uchimbaji wa mchanga na badala yake waanze kutumia *cyprus* na manila kwa ajili ya kujenga majumba yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, niseme tumesikia ama nimelichukua lakini Wizara ya Kilimo ndio itakuwa na nafasi nzuri zaidi na imekuwa ikitoa maelekezo ya namna ya hali ya mchanga nchini. Lakini pia napenda kufahamu kwamba namna ya nyumba nyengine ambazo zinajengwa ni mbadala ya matumizi ya mchanga lakini jibu la kuridhisha kwenye masuala ya mchanga basi Wizara ya Kilimo ndio wana nafasi zaidi ya kulijibu.

Nam. 37

Ubovu wa Barabara ya Kwenda *CRDB* – Mkunazini

Mhe. Omar Seif Abeid: (Kny. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini) - Aliuliza:

Barabara iendayo Benki ya *CRDB* Mkunazini ni *"One-way".* Hilo ni wazo zuri katika kupunguza msongamano wa gari.

Kwanini Barabara inayo kwenda Benk ya *CDDB* ni mbovu na ina mashimo mengi tofauti na inayotoka Benki hiyo ya *CRDB.*

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini Mwakilishi wa Jimbo la Dimani swali lake Nambari 37 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, barabara aliyoitaja Mjumbe ni miongoni mwa barabara zilizo chini ya majukumu ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mujibu wa Sheria. Kwa kuwa Mfuko wa Barabara umekuwa na utaratibu wa kutupatia fedha za matengenezo ya barabara japo kwamba suala hili liko huko lakini mimi naweza kumwambia pale hali inaporuhusu basi tutaingalia namna gani ya kuifanyia kazi barabara ile. *(Makofi)* Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti pia naomba nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini pamoja na majibu yake hayo nina swali (a) na (b).

Barabara ya kutoka *CRDB* mpaka Mkunazini nakumbuka kipindi kilichopita fedha zake zilitolewa pia na Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo na katika miaka ya karibuni nikasikia kwamba Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe alisusa kuchukua hela za maendeleo ya Jimbo jee mwakilishi wa sasa yuko tayari kuzichukua na kutumia kwa shughuli ya maendeleo ya jimbo hilo.

Pili naomba nijue hivi karibuni tuliona Naibu Waziri na Kiongozi mmoja wameenda katika barabara zao na kujenga kwa madai kwamba ni utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais, lakini yapo majimbo yana ahadi za Rais kuliko barabara tatu hazijatengenezwa ikiwemo ya Mfenesini na bahati nzuri mimi na

wewe Mhe. Naibu Waziri tulitembelea barabara ya Kihinani mpaka Kijichi, Meli kumi mpaka kambi za K.M.K.M na J.K.U na Mwakaje hadi Mwachealale hizi zote zinaahadi za Marais wawili ni lini alau barabara moja kati ya hizo zikatengenezwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mwakilishi aliyepita aliziacha pesa nyingi tu sana ambazo kusema la ukweli zingetusaidia sana katika maendeleo, miye nikiwa mwakilishi wa Jimbo la Malindi nachukua ahadi kwamba nitazitumia pesa zile ipasavyo kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wangu wa Jimbo la Malindi na *Inshaallah* kwa uwezi wake Mwenyezi Mungu watayakuta maendeleo ya kila siku katika Jimbo hilo.

Swali lake kuhusu ahadi za Mhe. Rais na Marais waliopita sisi tunazitambua ahadi hizo na napenda kumuarifu kwamba tumekuwa na utaratibu sasa hivi katika kuhakikisha kwamba kila ahadi ya viongozi wetu basi tunaipangia Mpango Kazi ili kuhakikisha katika kipindi hiki cha 2015 mpaka 2020 zile ahadi zote tume tumezikamilisha na pale ambapo tutashidwa kuikamilisha basi tutakuwa na sababu maalum. Lakini namuahidi Mhe. Mwakilishi atupe muda bado tuna muda na Inshaallah tutazikamilisha ahadi zote hizo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kujua kipimo gani wanatumia katika kuzitengeza barabara za ndani kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, nimeona barabara za mjini zimekuwa zikingenezwa kwa kiwango kikubwa pahali ambapo mjini *facility* zote anazohitaji binadamu zinapatikana kirahisi. Magharibi kunakoishi watu wengi barabara zake mbovu na mbaya kiasi ambacho mama zetu na dada zetu bado wanazalia huko huko mashamba, barabara hazipitiki barabara kama Welezo, Mwanakwerekwe na mwengineko lakini barabara za mjini tumeshuhudia zikiwa zinatengezwa. Jee kipimo gani wanatumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Kusema la kweli sisi vipimo tunavyotumia kwanza kuangalia ahadi zilizotolewa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM, pili tunaangalia ahadi za viongozi wetu na tatu tunaangalia vile vile hali ya fedha inaporuhusu kwa hiyo tunajenga barabara kwa mujibu wa ahadi zilotolewa, barabara za

Wilaya ya Magharibi zipo ambazo sasa hivi zishaanza utaratibu wa kutaka kutengenezwa.

Kwa hivyo mimi namuomba atupe subra na jana hapa lilijibiwa hapa suala la Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Idara Maalum za SMZ kwamba kuna barabara ambazo zina urefu wa kilomita 50 sasa hivi zimo katika uchambuzi yakinifu, ili baadae hizo barabara zifanyiwe kazi ya kujengwa. Kwa hiyo, atupe muda na baadaye atakuja kusema ni kweli tunafanya kazi sisi bila upendeleo wowote kwa ajili ya wananchi wetu wa Unguja na Pemba. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Utaratibu

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kuhusu utaratibu 63, 37 Mhe. Mwenyekiti, suala langu kipimo wanachotumia kwa nini hawazitengneezi barabara za Magharibi kwenye watu wengi wanatengeneza barabara kuna *facility* zote kipimo wanachotumia.

Mhe. Mwenyekiti: Waziri majibu ya kipimo kinachotumika ndiyo swali hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nimeeleza vizuri kwa ruhusu yako na kwa niaba na Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumwambia kwamba barabara zote tunazitengeneza kwa mujibu wa ahadi tulizozitoa katika ilani ya Uchanguzi na vile vile ahadi au maagizo ya viongozi wetu na vile vile kuna barabara nyengine nilivyosema barabara za ndani ziko Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais na Tawala za Mikoa na jana lilijibiwa vizuri hili suala. Hata katika kikao cha bajeti kuna barabara isiopunguza kilomita 50 zinafanyiwa uchambuzi yakinifu. Baada ya hapo saa huo uchambuzi yakinifu ndio inakuwa ni kipimo chetu cha kujua barabara ipi na mahitaji zaidi ya dharura itengenezwe na barabara ipi iwekwe muda mwengine, lakini zote tunakusudia kuzingeneza hizo barabara. Namuomba tena Mhe. Mwakilishi avute subra baadaye ikiwemo ahadi yake ya Welezo tutazitekeleza pale pesa itaporuhusu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Utaratibu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Kanuni ya 27 nanukuu kusema kwamba jana haikutajwa kilomita hamsini jana kilomita 0.5 ambayo alitaja Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za

SMZ. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Naibu hajasema sawa jana zimetajwa kilomita 0.5 za Pemba.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri umelifahamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, 0.5 kwa utaratibu ni mita 500. Sasa mimi nina hakika hakukusudia 0.5 alikusudia kilomita 50 zipo katika uchambuzi yakinifu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Kwa hivyo afute kauli yake *Hansard* ili ikae sawa kwa mujibu wa maelezo kasema 0.5 na sisi sote mashahidi katika hicho.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri weka sawa suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako naomba kutoa majibu ya nyongeza yaliyojibiwa na Mhe. Naibu Waziri na kabla ya kutoa majibu hayo ya nyongeza kwa mujibu wa majibu yetu ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum tuliyoyatoa jana.

Kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi kwa majibu yake aliyoyasema. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu majibu ya nyongeza jana najibu la msingi alisema kwamba Serikali kupitia Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum itajenga jumla ya kilomita 50 ambazo tayari zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu na katika kuzijenga kilomita hizo itategemea upatikanaji wa fedha na bajeti tuliyonayo ambayo imepangwa na serikali. *(Makofi)*

Ile 0.5 ilikuwa ni barabara tayari tumejenga sasa nafikiri akenda akitafuta *Hansard* ataona hilo jibu liko hivyo, lakini kuhusu suala la vigezo ambalo amelitaka Mhe. Hassan Mwakilishi wa Welezo.

Kigenzo cha kwanza, ni mahitaji ya wanachi na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Kigezo ya pili, ni umuhimu wa ile barabara yenyewe kutokana na fedha ambazo zipo.

Tatu, ni zile ahadi za Viongozi wetu wa Kitaifa.

Nne, ni mpango wa maendeleo wa bajeti ya wizara husika. *(Makofi)*

Katika kipindi kilichopita Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilikuwa na mpango wa kuijenga barabara ya Magogoni, Mwanakwerekwe Makaburini hiyo iko Wilaya ya Magharibi B na bado kwa sababu ya vikwanzo ambavyo tulivipata katika utekelezaji wa barabara hiyo Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum itajenga barabara kutoka kwa Mabata hadi Kijito Upele bado iko Wilaya ya Magharibi. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Hassan swali lake sote tungependa kuzijenga barabara hizi kwa haraka sana katika kijacho cha mwaka wa fedha kama nilivyosema jana kwamba itategemea barabara gani ambayo tutakuwa tunaiona tuipekipau umbele kutokana na mahitaji halisi tutaijenga. Ikiangukia barabara yake ile ya Welezo tutafanya hivyo, ikiangukia barabara nyengine yeyote ya Kama, Mfenesini tutafanya hivyo, ikiangukia barabara ya Muanda, Donge tutafanya hivyo. Yaani tutaona namna ya bajeti tulivyoipata na fedha zilivyo ndipo tutakapojenga na ahadi hiyo yetu itakuja ndani ya Baraza la Wawakilishi tuna mpango wa kujenga barabara gani. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda wa maswali umemaliza na maswali yapo, kwa hivyo tunamaliza muda uliopangiwa maswali.

Utaratibu

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nasimamia kwa kanuni ya 63(1) na 59(8) nasoma 59(8) kwamba 8(a) kutumia lugha ya matusi au kashfa, lakini Mhe. nazungumza kwamba tusibebane lakini tutumie utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, mwanamke anakuwa ni wanawake mtu anakuwa na jina lake moja lakini wanawake wanakuwa wengi Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa wote hasa hizo Jumuiya za Kimataifa sasa hivi wanawake na wanaume ni sawa kwa sawa na nguvu sawa na kila kitu sawa.

Mhe. mwanamke hatumpeleki tena katika masuala ya kumwambia kwamba alikuwa mwanamke alikuwa hivi, tunamtaja kama ni waziri wengine huko Marekani wanaomba Urais na Maspika wetu wengi hapa washakuwa viongozi wakubwa wanakuwa wanajiweza kweli kweli sio tena kuwaita mwanamke.

Kwa hiyo Mhe. Waziri wa Habari aliyesema neno ni mwanamke kwa niaba ya wanawake wanaojiamini pamoja na mke wangu ambaye anafanya kazi nyengine miye siziwezi aombe radhi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nimekusikia Mheshimiwa mjumbe lakini swali hili limemaliza tumeshakata.*(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti nakuomba sana katika utaratibu wa kudhalilisha kitu hiki hakipo, utaratibu Mheshimiwa nimeujenga na kashfa kaifanya na kama wote hawataki mke wangu basi mimi amuombe radhi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. jambo hili limeshapita nyuma kwa mujibu wa utaratibu nao tayari sasa hivi nimelifunga na limeshamalizika kwa hivyo, nasema nachukua nafasi yangu niliyonayo tunaendelea. *(Makofi)*

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu 39, ahsante Mhe. Mwenyekiti, hiki chombo kina utaratibu wake ndio sikurukia nikasurubiri amri yako, sirukii gari tu miye nisiyoijua mwendo wake, inaweza kuja kukutoa meno.

Utaratibu wa kuuliza swali 39 wakati ambapo swali limeingizwa katika orodha ya shughuli Spika atamwita mjumbe ambaye ameleta swali hilo au kama Spika atakubali mjumbe mwengine aulize. Hoja yangu iko namba 3 naomba Mhe. Mwenyekiti kwa heshima kabisa iangalie.

Endapo swali limeorodheshwa katika orodha ya shughuli halikufikiwa hadi wakati wa kipindi cha maswali kumalizika, sikiliza vizuri Mhe. Mwenyekiti, Spika anaweza kuongeza muda ikiwa kujibiwa suala hilo kwa muhimu kwa manufaa ya Taifa na mradi na muda unaongezwa usiozidi robo saa.

Suala la afya ni muhimu na hili Baraza chakula chake ni maswali na majibu ndio chakula na ndio msingi wa chimbuko hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nimekufahamu na kanuni inasema hivyo ni sawa lakini pia tuna jambo muhimu nalo ambalo kuwa liko mbele yetu la kuchangia hotuba ya wenyeviti ambapo wachangiaji ni wengi.

Kweli swali lako ni la msingi lakini nakuomba tuliendee na masuala haya yataweza kuwekwa pahali pengine kwa utaratibu unaofuata. *(Makofi)*

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaaifa ya mwaka 2016/17

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Majadiliano tunaendelea sasa ni zamu ya Mhe. Bi Hindi Hamad Khamis

Utaratibu

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kwa heshima kubwa jana sikumaliza nikaambiwa nitaendelea leo asubuhi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Sijakuelewa

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kwa heshima kubwa jana nilikuwa sijamaliza nikakatishwa nikaambiwa nitaendelea leo asubuhi Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan kwa kuwa ulilianza suala lako wakati muda wako uliutumia nakupa dakika 5 uwe umalizie.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mheshimiwa naomba uniongeze kidogo Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa dakika chache kuendeleza Mhe. Mwenyekiti nitaanza pale nilipomalizia jana.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar inakumbwa na janga kubwa la watu kuleta unga, Mhe. Mwenyekiti, uletaji wa unga si ajali ni *man made* ni mambo yanayoletwa na binadamu *is not an accident* si ajali ni mambo yanayofanywa na mwanadamu.

Mhe. Mwenyekiti, nitayazungumza mambo ambayo yanasababisha majanga kuhusu unga, Mhe. Mwenyekiti, wizi unasababishwa na unga, ukimwi unasabishwa na unga, mauaji yanasababishwa na unga, udhalilishaji wa wanawake na watoto unasababishwa na unga.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti inatu *cost* katika kujenga *sober house* Mhe. Mwenyekiti kujenga *sober house* ni maana kama huu unga sisi tumeukubali, pesa chungu nzima tunatumia katika kuwalinda na kuwaweka wale watu wa *sober house*, Mhe. Mwenyekiti hili jambo halikubaliki.

Mhe. Mwenyekiti, cha kuchangaza na cha ajabu ukienda jela Mhe. Mwenyekiti wanaotumia unga wako watatu lakini mletaji na muuzaji unga majela hawako. Mhe. Mwenyekiti wala mbakaji na mdhalilishaji watoto jela wako wawili wako watatu kama sikosei.

Mhe. Mwenyekiti janga la unga ni kubwa kutokana na athari zake zinazojitokeza, Mhe. Mwenyekiti imefika wakati sasa nasema waziwazi hii Tume ya maswala ya unga ivunjwe kwa miaka minne tume hii haijafanya kazi. Naomba ivunjwe tume hii haina kazi inayoifanya na isipewa pesa hata moja kwa sababu majanga ya unga baada ya tume kushughulikia kuthibiti unga, unga unazidi kujaa nchini kwetu na Tume ipo na ina watu na inapewa pesa.

Maana yake Tume hii imefeli, *this* Tume *is failure* haiwezi kuendelea kuwahudumia wakulima na wakwezi wanamapinduzi wa nchi hii kwasababu unga Zanzibar umekuwa mwingi na Tume ipo.

Mhe. Mwenyekiti badala Tume kuvunjwa naomba nguvu hizi na *power* hizi zipelekwe katika Wakuu wa Wilaya ili majembe hayo yaweze kudhibiti unga. Naamini Wakuu wa Wilaya tulionao sasa hivi kwa mfano wa Kusini na Wilaya zote nchi hii unga wanaweza kuuthibiti kulikoni Tume hii. Tume hii baada kuzuia unga usiingie nchini imekuwa kama kifungulio cha unga kuingia nchini.

Mhe. Mwenyekiti kwasababu ya muda ulinipa nitakwenda moja kwa moja Idara ya maafa niliizungumza nitakwenda moja kwa moja katika Afisi ya Rais Ikulu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti ahadi za Rais tarehe 24 kazi moja Ofisi ya Faragha ya Ikulu ni kufanya ahadi za Mhe. Rais na kuna msemo mmoja aliusema Wilson Churchile alisema hivi *his wishes is other people's command*, na Mhe. Rais anaposema linakuwa ni agizo, aliwaagiza tarehe 24/04/2014 barabara ya wananchi wangu wa Welezo itekelezwe. Sina mengi ya kusema naomba kuwakumbusha Ofisi ya Rais Ikulu kwamba Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar alitoa agizo kutengezwa kwa barabara ya wananchi wa Welezo ya Hawai.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine linaloniudhi na kunisikitisha ukifungua mitandao ya kijamii, vyombo binafsi vya kijamii vingi utavikuta vinaandika maneno ya istizai, maneno mabaya dhidi ya Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, nitatoa mfano kuna mtandao mmoja unaandika siku zote kwamba aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Haya ni maneno mabaya wako watu nchi hii wanautafuta urais tangu wamezaliwa hawajaupata, Rais tunaye, Rais tumemuapisha Amani, kapigiwa mizinga, kapigiwa saluti kila mtu kajua leo Rais kaapishwa. Lakini kuna mtandao bado unaandika aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, hii haikubaliki kumkejeli Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar anayewaongoza wana Mapinduzi, haikubali hata kidogo. Naomba sana Idara ya Mawasiliano Ikulu na wote wanasheria wanayo haki kutumia *either National* au *International forms* za sheria kuishtaki mitandao hii. Haki za kushtaki mitandao zipo wazi tuishtaki na tuifungie inawezekana Mheshimiwa jambo hili, hatuwezi kuwaachia *space* ya kudhalilishwa Rais wetu tuliyemchagua wananchi sote.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba kusema kwamba hii Idara ya Maafa isikae kusubiri maafa wahenga wamesema kwamba, "*prevention is better than cure*". Wazibe maafa yasitokezee wasiwe kama wachimba makaburi kazi yao kukaa kusubiri maafa waya-*manage* haiyumkiniki Mhe. Mwenyekiti. Kwa sababu itakuwa kazi yao wao kuombezea maafa yaje wapate kuyafanyia kazi, wawe na jukumu jengine Mhe. Mwenyekiti la kuyalinda maafa yasitokezee, ndio maana wahenga wakasema "kinga ni bora kuliko tiba".

Mhe. Mwenyekiti, kuna Idara ya Walemavu wana ukosefu wa vitu vingi masikini ya Mungu. Naomba sana idara hii ipewe meno, ipewe nyenzo kwa sababu hawa ni watu wa Mwenyezi Mungu amewapa ulemavu hawakuomba. Naomba sana serikali iendelee kuwapa uwezo, kuwapa nyenzo zote.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kuhusu unga, hii mamlaka inayoshughulikia unga ivunjwe kwa sababu haina kazi inayoifanya, unga wameendelea kuletwa, watu hawafungwi, majela matupu kuhusu watu wenye unga hamna mtu hata mmoja mleta unga, wala muuza unga jela hayupo. Mhe. Mwenyekiti, hatufurahishwi katika nchi ya Kimapinduzi unga umejaa na hakuna kesi yoyote. Baada ya hayo machache naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi moja kwa moja niende katika uratibu wa udhibiti wa madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii imechangiwa na wajumbe wengi, na ni haki yetu kwamba sehemu hii tuichangie.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili hapa nchini kwetu Zanzibar limekuwa kubwa, zito na kila siku linaendelea kuzidi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba wakati huu tulionao jambo hili la madawa ya kulevya kila mtu limemgusa kwa upande wowote, na athari yake ni kubwa. Mimi nataka niseme kwamba kila upande wa Zanzibar athari hii ipo na limeshaenea mpaka sehemu za vijijini huko tena hakusemeki.

Sasa mimi nataka niiombe serikali umefika wakati kwa kukaa sehemu mbali mbali. Kwa mfano, kama kwenye Baraza hili na sehemu nyengine kujadili suala hili muda umekuwa mkubwa. Sasa ni tukaanza kuchukua hatua ya makusudi ili kuona kwamba tatizo hili la madawa ya kulevya linapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, imefika wakati sasa na sisi tukaaza kuchukua hatua za makusudi ili kuona kwamba suala la madawa ya kulevya linapatiwa ufumbuzi wa haraka iwezekanavyo, kwa sababu hatari, hatari, hatari. Vijana wetu na wao sasa wengi wameanza kusinzia majiani, utamuona mtu kasafiri bado yupo hapo hapo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa maoni yangu mimi nasema kwamba wale wote wanaoshakiwa na kwa sababu hii ni kwamba sote tunaishi vijijini, tunaishi mijini watu wanajuulikana. Kwa nini hatua hazichukuliwi kama wenzetu wa Tanzania Bara. Huu si wakati tena wa kuoneana huruma kwa sababu tukilifumbia macho tatizo hili athari yake ni kubwa, wizi utazidi, ubakaji utazidi mambo mengine ya vitendo vibaya yatazidi tutamlaumu nani. Sasa hapa tulipofika si pahala tena pakusubiri subiri, ni kweli kwamba wale wote wanaohusika au wanaojihusisha na madawa ya kulevya wachukuliwe hatua mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo sasa na mimi nije nizungumzie Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kwamba chombo hiki ni chombo kikubwa sana, na sisi tuko katika jamii, sisi Waheshimiwa Wawakilishi ni vioo vya jamii, sisi wajibu wetu ni kwamba tuoneshe mfano kwa wale ambao tunawaongoza.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukajisahihisha sana, sana tunapokuwemo katika chombo hiki. Mimi juzi nimemuona Mheshimiwa mmoja na nilistaajabu sana humu ndani alikuwa amevaa vyengine lakini alipotoka hapo nje tu anaingia kwenye gari nikamuona kabadilika kama kinyonga nikajiuliza humu ndani ana ghala ya kubadilisha nguo. Ni vyema tukalinda heshima yetu na Mhe. Mwenyekiti kuanzia Spika na Wenyeviti na wao wanatakiwa kwamba kauli zao ziwe za uhakika.

Nataka nitoe mfano kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub pale kauli ya kuwa atoke nje bado ulikuwa uwe na msimamo ule ule, toka nje basi toka nje. Tukifanya masuala mengine basi hili Baraza litaenda sio katika mwendo mzuri, hadhi inapotea lazima tujenge heshima ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka niseme hilo kwa sababu sisi ni kioo cha jamii isifike humu kila mtu akawa ana lake au anaona hivi au kama kukomoana hivi, haijengi sisi sote ni wamoja tusikomoane twende vizuri ili na jamii nayo ione kwamba Baraza linakwenda vizuri. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka niseme hayo kwa kipengele hiki, au ikiwa bado tunataka tupate semina basi Baraza itufanyie semina tena ili tuendelee vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo vile vile niende kwenye Mfuko wa Jamii wa *TASAF*. Mhe. Mwenyekiti, mfuko huu ulipoanza ulianza vizuri, na ulianza katika miradi mingi ya maendeleo ujenzi wa maskuli, vituo vya afya na mambo mengine. Lakini sasa mradi huu umejikita katika masuala ya Kaya Masikini.

Mhe. Mwenyekiti, kuna manung'uniko hivi sasa kwamba katika kuendeleza mradi huu kwenye Kaya Masikini kuna wale watu wanaostahiki hasa kusaidiwa kwenye Kaya Masikini hawakupata mradi huu, wamepewa watu wasiostahiki wanaostahiki wameachwa. Sasa mimi naomba kwamba manung'uniko haya yafuatiliwe ili haki itendeke. Kwa sababu manunguniko yamekuwa mengi na sio utaratibu miradi ile imeletwa kwa ajili maalum. Kwa hivyo, nadhani serikali iko haja ya miradi hii kufatilia manung'uniko ya wananchi yana ukweli gani, ikiwa watu wameachwa wale wanaostahiki kupewa ule msaada basi wapewe wale, wale waliokuwa hawastahiki waachwe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kipengele hicho vile vile niende kwenye Mfuko wa Jimbo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza imekuwa ni muda mkubwa mfuko huu waheshimiwa hatujaupata, na huko kwenye majimbo yetu kuna manung'uniko kwamba kwa nini Waheshimiwa Wabunge wao wameshamaliza matumizi wawakilishi nyinyi vipi mnasinzia tu huko.

Sasa ni vyema ule mfuko tukaingiziwa na Mhe. Mwenyekiti tuna masikitiko mwanzo tumeambiwa kwamba tukafungue *account*, tukenda tukafungua muda mkubwa tumerejesha marejesho kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na tukawapa *account* zetu. Lakini hii leo tunaambiwa hazifai ilikuwaje? Muda wote tuliopeleka ilikuwa kama kuna matatizo *account* zile hazifai basi ilikuwa tuambiwe mapema tuanze ule utaratibu, lakini leo tunaambiwa mambo tayari huku tunaambiwa mlivyopeleka hazifai. Ilikuwaje muda umeshapita kwa nini tusielezwe na mapema kwamba *account* mlizofungua hazifai zinazotakiwa ni hizi, tukarekebisha na mapema.

Lakini kama hilo halitoshi vile vile tunaambiwa kwamba huenda sisi wengine kwenye majimbo yetu pesa za majimbo tusitiliwa, kwa nini? Kwa sababu waheshimiwa waliopita marejesho hayajarudi, akah! Ina maana kosa la mtu mwengine aadhibiwe mtu mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo haiwi si vizuri Mheshimiwa aliyepo kwenye jimbo hivi sasa ina maana hiyo pesa aingiziwe yeye, na yeye ataonekana vipi atazitumia, ikiwa atafanya kosa yeye basi na yeye aadhibiwe kwa mujibu wa utaratibu uliopo. Kwa hiyo, tunaiomba serikali kwamba ikiwa kuna makosa ya waheshimiwa waliopita basi sheria ichukue mkondo wake. Asipewe adhabu hiyo au wasinyimwe wananchi mfuko huo kwa wakati huu kwa sababu ya mtu aliyekwishapita.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani mimi naiomba serikali sana, sana, sana na naiomba kwa mara hii kwa vile imebadilishwa sheria ya mfuko huu kwa hivyo majimbo yote au waheshimiwa wote wa majimbo kila mmoja aingiziwe pesa kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo vile vile napenda niseme kwamba kuhusu Viongozi Wakuu wa Serikali na hapa tunamzungumza zaidi Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwamba mle wanamotembelea wakaweka ahadi, tunaomba kwamba zile ahadi zitekelezwe. Kwa mfano, kama mimi jimbo langu la Kiwani Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alitembelea mwaka 2015…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umebakia dakika moja.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Sawa. Alitembelea katika Shehia ya Kiwani na pale kuna vijana aliwaahidi mambo mengi tu lakini mpaka hii leo mambo yale hayajatekelezwa. Kwa hivyo, naomba serikali wale viongozi wakuu

wanapoweka ahadi zao basi zitekelezwe. Na vile vile naiomba serikali zinafanyika sherehe za kitaifa lakini kama sisi waheshimiwa tunayo haki ya kupata ratiba kabla ya ule wakati haujafika. Lakini tunasikia tu kwenye vyombo leo utakuwa ufunguzi hapa, utakuwa ufunguzi hapa wa miradi lakini bado kama sisi waheshimiwa tunaomba tuzipate zile ratiba kabla ya ule wakati kufika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba na mimi niunge mkono kamati hii kwa uwasilishaji wake na naunga mkono mia juu ya mia. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kulingana na orodha yetu ya wachangiaji bado ni kubwa sana, na kamati iliyo mbele yetu inatakiwa imalize leo. Kwa hivyo, wajumbe waliobakia niwaombe sana waweze kuchangia kwa maandishi, kama mtu anaona bado kulingana na mada haijazungumzwa yake yeye au kama ishazungumzwa kama anaona achangie basi achangie kwa maandishi mumpelekee Mwenyekiti ili na yeye apate muda kuweza kujitayarisha kuja kuweka sawa jambo hili. Kwa hivyo, kwa nafasi ya mwisho sasa hivi nitatoa watu wawili na baadae atakuja Naibu Spika, kunipokea hapa tutaendelea na mjadala kama itakavyoona inafaa. Ahsante.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Kamati ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inayohusiana na Viongozi Wakuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hii nikaweza kusimama hapa nikaweza kuchangia ripoti ya kamati hii. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu umesema muda ni mdogo nitachangia machache tu ili na mimi niweze kusikika kuchangia kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja kwenye Idara ya Maafa. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli idara hii ipo lakini pia kwa mapendekezo yangu na ushauri wangu idara hii kwa sababu tunajua iko kwenye Wilaya zote za Unguja. Mhe. Mwenyekiti, iil kuweza kuwa na ufanisi zaidi Idara hii ya Maafa iweze kushirikiana na wananchi kuanzia kwenye shehia na vijijini, sababu ya kusema hivyo yanapotokea maafa huwa taarifa hazifiki kwa hatua ambayo inastahiki kwenye Wilaya na kwenye Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, kulitokea tukio moja ambalo lilitokea Mkoa wa Kaskazini Pemba, Wilaya ya Micheweni kulikuwa na msitu Shumbaviamboni ukaungua lakini…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba nikukatishe kidogo ukae aingie Mhe. Naibu Spika, nakuomba ukae kwanza kidogo.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kuja kukaa kwenye kiti hicho ili sote wanawake tupate nafasi ya kuchangia.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea msitu wa Shumbaviamboni ulitokewa na maafa makubwa, lakini kwa sababu ya taarifa ambazo zinawafikia walengwa kwa maana ya kuweza kuokoa hatua zile huwa hazifiki haraka, msitu ule uliungua na kwa kweli kiasi fulani ilitokea hasara kubwa.
Mhe. Naibu Spika, nikiendelea hapo hapo kwenye Idara ya Maafa matokeo mengi yanayotokea kwenye wilaya zetu pamoja na shehia kwa kweli naomba idara hii iweze kushirikiana na shehia husika na hata kuunda kamati nyengine ambazo ziko kwenye shehia kwa kushirikiana na wanavijiji.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kwenye kamati hii kuna mambo mengi ambayo tunatakiwa tuyachangie nitaingia kwenye Tume ya UKIMWI. Mhe. Naibu Spika, UKIMWI ni janga kubwa la taifa na hususan unaingia pahali ambapo hapastahiki. Lakini pia waathirika wakubwa ni vijana wetu. Mhe. Naibu Spika, kwa kusema hivyo tume hii iweze kushirikiana na wilaya na majimbo pamoja na shehia ili kutoa elimu zaidi na kuelimisha vijana na janga hili.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nitakwenda kwenye Ofisi ya Uratibu ya SMZ ilioko Dar es Salaam. Ofisi hii kwa kweli ni ofisi ambayo inashirikisha Tanzania Bara na Zanzibar. Mapendekezo yangu kwenye kamati pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iweze kutoa elimu tosha inayohusiana na maendeleo ya Muungano. Mhe. Naibu Spika, hili ni suala ambalo hata wanafunzi wetu watajua maendeleo ambayo yanatokana na Muungano.

Mhe. Naibu Spika, kwa kundelea mbele nije kwenye *TASAF I*. Kwa kweli *TASAF I* ilitoa muamko mkubwa kwa jamii na tukapata miradi mbali mbali, lakini kuna miradi ambayo ilikufa. Naiomba wizara ile miradi iliyokuwa imekufa waweze kujumuishwa masheha pamoja na wananchi ili kutoa taaluma zaidi kwa sababu kuna miradi ya *TASAF III* inayoambatana na kaya masikini.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele kwenye kaya masikini. Kkaya masikini ni mjumuisho wa watu ambao wanaishi kwenye mazingira magumu, huwa

kunatolewa pesa kwa ajili ya kujikwamua na umasikini lakini pia walengwa wanaokusudiwa waweze kufuatiliwa ili waweze kufanya majukumu yao ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono ripoti hii ya kamati kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe bado nina majina ya watu wengi wa kuchangia na muda hautotutosha kwa leo. Kwa hiyo, nitataja majina mengine mawili ya mwisho watu watachangia kuna ambao wameniomba watachangia kwa dakika tano tano na nitawapa fursa hiyo wachangie kwa dakika tano kama walivyosema ikizidi nitamsitisha, tukimaliza hapo sasa tutata nafasi kwa mawaziri ambao wametaka na wao kuchangia ili baadae Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika na wizara hizi waje wafanye majumuisho pamoja na Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu chini ya kiongozi wake Mwenyekiti mahiri Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niende kwenye kaya masikini. Jana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii alipowasilisha hapa alitwambia kwamba Zanzibar kaya masikini ni 204, hapa kidogo nilipata hofu kwa sababu mimi najua kule Ndagoni tu kuna mia tatu na zaidi, kwa hiyo nikataka kujua hapa kwamba ni 204 kaya masikini au shehia. Nataka nijue hilo.

Pia niende kwenye suala la madawa ya kulevya ambalo hili limezungumziwa na wengi kwa sababu ni kilio cha taifa. Lakini cha kushangaza Mhe. Naibu Spika, hapa Zanzibar sijui tuseme tuna nini, uyakhe umekuwa mwingi, kuoneleana huruma na imani. Wenzetu kule Tanzania Bara wameshathubutu kufanya hivyo lakini sisi humu tunajua yanamouzwa, yanamotoka na wanaochukua lakini hakuna hatua yoyote ambayo inachukuliwa. Sasa mimi nashangaa kuona suala hili tunashindwa kulitekeleza na kulisimamia, tuondoeni muhali, tuwe ni kitu kimoja ili kulitokomeza suala hili kama wenzetu kule Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, niende pale pale kwenye kaya masikini, wale wanaopata pesa niulize kidogo, kamati nataka wanambie kwamba vipi wanawafuatilia kwa sababu kuna malalamiko baadhi ya wengine hukatwa pesa bila ya utaratibu.

Kwa hivyo, hili kamati kama hawalijui walifahamu na walifuatilie na waweze kufuatilia kwenye wale wanaopokea zile pesa.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ahadi za viongozi wakuu wa serikali. Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali wakati mwengine huwa hazitekelezwi, nyengine hutekelezwa lakini nyengine husahaulika kabisa. Kwa mfano, kule jimboni kwangu kuna kijiji cha Birikau, wale waliahidiwa na Mhe. Dkt. Abeid Amani Karume kutengenezwa barabara ile alitoa ahadi na hadi leo barabara ile haijaulizwa chochote, ahadi ile nasema imesahaulika. Mhe. Naibu Spika, vile vile niende katika Jimbo la Bububu kuna sehemu ya Dole, Mbuzini, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi aliahidi hapa kutoa hati za mashamba kwa wananchi wale, wengine wamepata wengine hadi leo hawajapata.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki niseme mengi kwa sababu muda hautoshi isipokuwa naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Lakini ningeomba kwenye suala hili la kaya masikini ningepata ufafanuzi watu hawa 204 ni kwa Zanzibar, Shehia au ni wale wanaopokea kaya masikini wananchi wenyewe?

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ambayo nilikuwa naitaka toka jana, nilifikiri siipati lakini nashukuru kwamba nimeipata.

Pili Mheshimiwa niseme tu kwamba nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri hasa tukizingatia kwamba Ofisi za Viongozi Wakuu wa Serikali ni muhimu na shughuli zao lazima tuzipongeze kwa mazuri wanayoyafanya, kama kuna kasoro basi tuwaelekeze. Lakini wakubwa hawana kasoro isipokuwa tuwaongezee kazi tu zaidi ya kuwapa ufanisi katika shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba naipongeza Ofisi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anazozifanya mwenyewe Rais na watendaji wake wote. Rais wetu tunajua kwamba ana kazi nyingi na rais ndiye anayetafuta keki ambayo inatumika na watu wote, yaani serikali nzima kwa wananchi wote. Kwa hivyo, juhudi yake hiyo lazima tuipongeze na kila analolifanya tuliwekee rikodi kwamba kalifanya na litangazwe lionekane.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa upande wangu namshukuru Mhe. Rais alikuja kuifungua skuli yetu mpya Kwarara ambayo ni skuli ya kileo kabisa na bahati nzuri katika ahadi yake moja aliyoitoa kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwamba barabara ya Kwarara ijengwe kwa kiwango cha lami.

Nampongeza sana na najua ahadi hiyo itatekelezwa. Mfano huo ninautoa kuna kijiji kinaitwa Mgonjoni Wilaya ya Kaskazini 'B' mpaka na Kilombero.

Mhe. Naibu Spika, Mgonjoni kilikuwa ni kijiji ambacho hakitambuliki hapa katika historia yetu ilikuwa mafichoni, lakini bahati nzuri Mhe. Rais baada ya kupata kilio cha wananchi wa eneo hilo alikwenda bila ya kupiga hodi na alipofika akatoa maagizo watoto wa Mgonjoni wanataka kujisikia kama wako katika eneo lolote la kileo, katoa amri skuli imejengwa, hospitali imeanza kujengwa, barabara imejengwa, Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kaifanya kazi kubwa sana nampongeza sana kwa juhudi yake hiyo ambaye kasimamia mambo yoe ambayo Rais aliyaahidi nafikiri katika hotuba yake alisematu kwamba haya yote nitayasimamia.

Jengine niseme, kuna Idara yetu ya Usalama wa Serikali (*GSO*). Mheshimiwa mimi nawapongeza sana wenzetu hawa na nasema kwa sasa hivi tangu ninakotoka lakini mpaka sasa hivi wazidishe bidii hasa tukizingatia kwamba usalama ni uhai wa jambo lolote katika nchi yetu. Kwa hivyo, nasema nampongea Mhe. Rais, nakipongeza kitengo hiki na nayapongeza yale mazuri yote waliyotangulia wenzangu kuyasema kwa sababu taratibu zote za Baraza hutakiwi urudie lakini kwa kweli nawapongeza wenzangu wote walioniangulia na waliyosema nayaunga mkono kwa ajili ya maendeleo yetu.

Kwa ufupi kabisa jengine ni Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi ni roho ya nchi na tunaitegemea kwa usalama wa nchi yetu baada ya kuendesha uchaguzi vizuri. Kwa mwelekeo wa sasa hivi baada ya kupitisha sheria mpya tunaamini kwamba tutakuwa na wilaya zetu zina kazi maalum za kufanya na zitakuwa na ofisi zake. Naipongeza serikali kwa hilo, lakini pia Makao Makuu ya Tume kupewa jengo lile ambalo lipo karibu kuongeza nguvu litengenezwe ili wapate ofisi nzuri.

La mwisho Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Mhe. Naibu Spika, idara hii ina kazi nyingi na idara hii inalea watu wa aina mbali mbali, niwaombe sana wahusika kuanzia mkurugenzi na wenzake wawatembelee wenzao katika majimbo. Bado tuna walemavu wengi katika maeneo yetu wanataka misaada mbali mbali. Kuna taarifa huwa wanazisikia tu kwamba kuna vikundi vina-*drive* wao hawajui. Kwa hivyo, taaluma wapewe ili na wao wajielewe kwamba wamo katika nchi yetu hii wanafaidika na rasilimali ya serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa leo baada ya hayo machache mimi naunga mkono ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na

ninawatakia kheri wenzetu waendelee na shughuli zao katika kazi zao ili kuimarisha maendeleo ya nchi yetu. Nashukuru Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nashukuru. Waheshimiwa Wajumbe naomba mnaponiletea vi-*note* vya kutaka kuchangia mniandikie majina yenu kamili napata tabu sana wakati mwengine kumjua ni nani, wengine wanasahau kuandika majina. Sasa tunaanza na manaibu waziri baadae tutakwenda na mawaziri na mwisho kabisa tunampa mwenye hoja ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati na yeye atachangia.

Waheshimiwa kuna Naibu Waziri kaniletea anataka kuchangia lakini simjui nani kaniandikia yeye Naibu Waziri, kama hayupo naendelea na Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Mheshimiwa karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ni mimi lakini nimeandika jina.

Mhe. Naibu Spika: Hujaandika jina lako Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ipo mpaka sasa hivi naomba uniruhusu.

Mhe. Naibu Spika: Tunaendelea unataka kuchangia, haya changia basi. Umeniomba dakika tano.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, na mimi napenda nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya dakika tano na *Inshaallah* nitazitumia vizuri ili niweze kukidhi muda na matakwa ya taratibu.

Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja niseme kwamba naipongeza sana kamati kwa kazi nzuri na juhudi ambayo wameifanya mpaka wakapata kuibua haya ambayo wametwambia. Lakini vile vile mimi moja kwa moja niende katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), hususan katika kipindi hiki cha awamu ya tatu.

Mhe. Naibu Spika, niseme mimi nafurahishwa sana na mwenendo mzima wa mpango huu wa utekelezaji wa miradi hii ya *TASAF* hususan katika kipindi hiki cha mradi unaotekelezwa katika awamu hii ya tatu. Mradi huu tumeshuhudia kwamba katika utekelezaji wake ni kwamba ni mpango ambao unaendeshwa

Tanzania nzima na kila sehemu unakwenda kwa mujibu wa utaratibu ule ule pasina tofauti yoyote. Pamoja na ripoti iliyoeleza kwamba kujifunza Tanzania Bara ni jambo moja zuri sana na mimi nakubaliana nalo, lakini licha ya hayo mpango huu kwa upande wa Zanzibar pia tumeona mafanikio makubwa hata wale wenyewe ambao wanasimamia walipokuja wameridhishwa na mwenendo mzima wa utekelezaji wa mradi huu.

Kwa upande wa changamoto. Changamoto ambazo zipo au ambazo zimejitokeza mara nyingi sana zinasababishwa na jamii yenyewe na sio kwenye mpango husika. Mheshimiwa ukweli ni kwamba wananchi katika utekelezaji wa mpango huu bado inaonekana hawajawa na uelewa wa kutosha, ni jukumu ambalo kwa kweli kwa kiasi fulani linakuwa likirudisha nyuma katika juhudi mbali mbali za serikali katika suala hili. Kwa mfano, wako watu ambao wameingia katika mpango wakiwa katika hali duni sana ambao walikuwa na vigezo, kamati zile ambazo zimeundwa za *CMC* ziliweza kuwatambua wale ambao wana vigezo ambavyo vina uashiria wa umasikini na vigezo hivi vilitokana na mpango uliotokana na sensa ya matokeo ya mwaka 2012.

Mhe. Naibu Spika, lakini la kusikitisha wananchi wale ambapo waliitwa kwenye mikutano inaonekana wengi wao katika vijiji husika hawakuwea kushiriki ipasavyo na baadae kwa vile utaratibu huo ulikuwa unaidhinishwa kwa kupitia mkutano mkuu wa kijiji, hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa lakini hatimaye walengwa walipatikana lakini baadhi ya walengwa sasa hivi inavyoonekana wameshafikia malengo. Kwa sababu malengo ya mpango mtu anaweza akaingia ni masikini lakini baadae akaonekana tayari amepiga hatua na mpango vile vile uanze kuangalia watu kama wale iweze kuwatoa. Lakini kwa bahati mbaya sana kuna wengine ambao walikuwa na sifa hawakuweza kushiriki katika zoezi hili kikamilifu na hatimaye malalamiko ndivyo ambavyo katika jamii zetu yanakuwa yakizunguka sana. Kwa hivyo, wako ambao kwa sasa hivi wameshapiga hatua kiasi fulani wamesha-*improve* familia zao kama vile malengo ambayo yamekusudiwa katika suala zima la elimu na suala la afya.

Mhe. Naibu Spika, mimi nipongeze sana mpango huu wa serikali ambao umeweza kuzihaulisha fedha katika kuzihudumia kaya hizi masikini, lakini bado kuna tatizo kubwa la uelewa na hususan mashirikiano madogo wenzetu ambao watu wanotekeleza mpango huu wanayoyapata.

La mwisho ningeomba tu, kwamba katika kuzungumzia suala la jinsi madawa ya kulevya kwa ufupi. Suala la madawa ya kulevya ni kero ndani ya nchi yetu kweli lakini bado na sisi wananchi hatujawa tayari katika kuona kwamba

tunashirikiana vya kutosha na serikali katika kupiga hatua katika kutokomeza jambo hili. Kwa mfano, zipo taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa juu ya watu ambao wanatuhumiwa, lakini pale ambapo wanaitwa na Jeshi la Polisi kwenda kuhojiwa kwa tuhuma unakuta wananchi pamoja na viongozi tunakuwa tukilalamika sana juu ya taratibu zile ambazo zinafuatwa.

Mimi naamini tu kwamba Jeshi la Polisi ni chombo ambacho kinafanya kazi zake kwa uadilifu lakini wanafuata taratibu, hawezi kutiwa mtu hatiani ambaye atakuwa hana hatia. Hivyo basi, ningeshauri sana Waheshimiwa Wajumbe pamoja na viongozi na wananchi kwa ujumla tuendelee sana kuwapa mashirikiano serikali pale ambapo kwa kweli kuna jambo ambalo linafanyiwa kazi basi tuache utaratibu uendelee na pale ambapo itaonekana kwamba kuna mtu hana hatia basi nadhani hakuna hatua nyengine itakayoendelea kama itakuwa ndio hivyo.

La mwisho kabisa naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa jinsi walivyochangia, aliwaona jinsi wanavyofanya kazi vizuri. Ni kweli kazi zinafanywa vizuri, lakini miongoni mwetu huwa mara nyingi sana tunapenda kubeza juhudi nyingi za serikali zinazokuwa zikifanyika.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi za kuchangia Mswada huu wa Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Sheria. Kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pia kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa jitihada kubwa ya kusimamia harakati zote hizi zinazotakiwa ziendeshwe na serikali.

Vile vile nachukua nafasi hii kuwapongeza Wawakilishi wote kwa hatua ambazo wanazichukua ndani ya Baraza hili katika kuielekeza serikali na katika kuongoza kwa masuala ambayo yanawafanya Wazanzibari wajue kwamba Baraza lao liko imara. Ni ukweli usiofichika, Baraza hili naweza nikasema kwamba ni tamu kuliko Mabaraza yote. Nakusudia kusema tamu maana yake ni zuri kupindukia, sababu ya kusema hivyo kwamba ndani ya Baraza hili hakuna upinzani, ndani ya Baraza hili kuna hali ya kuielekeza Zanzibar kwenye ....

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu namba 59(3) Mjumbe yeyote anapokuwa akisimama Barazani atawajibika kwa sababu za msingi kwamba maelezo anayotoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au yakubahatisha na Spika, au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka mjumbe huyo anayoyasema atoe uthibitisho na usemi wake. Mimi nimshukuru tu Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum kama kajiunga na CCM atwambie tupate kumjua, atuthibitishie hilo vyenginevyo aombe radhi.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, napenda kumwambia Mhe. Mwakilishi kwamba mara baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuamua kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na ikaingizwa ndani ya Baraza hili maana yake ni kwamba Zanzibar Serikali yake haina ipinzani watu wanatakiwa wote kwa pamoja watekeleze ilani ya Chama cha Mapinduzi. Unapotekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi maana yake wewe sio mpinzani.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mwakilishi mimi pamoja na Waheshimiwa Wengine tunatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na tutaendelea kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim, kaa kitako.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum): Ukweli ni kwamba tuliapa kwamba tutalinda na kutetea katiba ya Zanzibar, tutamshauri Rais kwa hekima na busara. Sasa kama wewe ni mpinzani utamshauri Rais kwa hekima na busara, kama wewe ni mpinzani utaapa kuilinda katiba. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, ningetaka niseme tu kwamba darasa linahitajika kwa baadhi ya Wawakilishi wasiojua nini kinachotendwa na serikali hii.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kurudia tena kuwapongeza Wawakilishi kwamba ni wakati muwafaka sisi kama viongozi tunaosimamia maendeleo na matakwa ya Wazanzibari, kushikamana na Serikali iliyoko madarakani kwa misingi ya kuhakikisha kwamba tunampa nguvu Mhe. Rais wa Zanzibar kuteleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mmezungumza mengi Waheshimiwa Wawakilishi, yakiwemo madawa ya kulevya mapungufu mbali mbali ni haki yenu na ni haki ya msingi. Kwa sababu, kama hatukushikamana tukaisukuma serikali kwenye mwendo unaotakiwa na wananchi waliopiga kura kuiweka madarakani, tutakuwa hatukutenda haki.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kusema kwamba ni wajibu wetu sisi sote kwa pamoja kujenga ari ya kurudisha ile ari ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, tukijenga ari ya kurudishwa yale yaliyotekelezwa au yaliyoendelezwa na Mapinduzi yetu ya mwaka 1964 haya matakwa yote ya Wazanzibari tutayafikisha pale wanapoyataka. Mhe. Naibu Spika, napenda kuwawambia Wawakilishi wote kwamba kimsingi sisi ndio tunaotakiwa tusimamie harakati za Mapinduzi ya Zanzibar, kwa vile kila tunachokiona kina kasoro ni wajibu wetu kukileta hapa tukakizungumza kwa pamoja kasoro ile ikaondoka ili serikali ikapata nafasi ya kuendesha harakati zake na tukampa nafasi Mhe. Rais, tukampa nafasi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuhakikisha maendeleo ya Wazanzibar yanafika pale yanapotakiwa.

Mshikamano wetu ndugu Wawakilishi juu ya kuisimamia harakati za Mapinduzi ya Zanzibar ndiyo yatawezesha uchaguzi wa mwaka 2020 CCM kushinda tena kwa vishindo. Sasa mimi nataka niwaambie kwamba mimi sikuja humu kwa maana ya upinzani, nimekuja humu kwa matakwa ya kuwatumikia Wazanzibari. Sasa kama mtu ana tafsiri sio darasa linahitajika kwake.

Mhe. Naibu Spika, asante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Said Soud Said kwa kutoa darasa zuri hongera.

Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi kunipa nafasi kidogo kuweza kuchangia na kutoa baadhi ya maelezo kidogo ya ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza niungane na nikubaliane sambamba na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kuanzia Mwenyekiti wa Kamati hii ya Kusimamia Viongozi wa Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao lakini pia kwa ripoti ambayo imetoa uhalisia katika zile idara na taasisi zilizokuwepo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwa uchache bila ya kuwataja ambao wamechangia natumai Mhe. Waziri atawataja lakini nizungumze katika zile idara ambazo Wajumbe wengi wamekuwa wakizigusia. Nianze na Idara ya Kukabiliana na Maafa, tukubaliane nao ndugu Wajumbe lakini idara hii tujue kwamba ina jukumu, baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wamesema idara ipo tu mpaka kusubiri maafa yatokee. Lakini bado idara ina jukumu la kuelimisha watu wote, kabla ya matokeo hayajatokea lakini pia tutambue Kamati hizi za Maafa zipo katika

ngazi zote kuanzia ngazi za Mkoa, ngazi za Wilaya mpaka ngazi za Shehia, hata elimu inapotoka watu wote hawa wamekuwa wakielimishwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, pia ilitoka rai kwa Mhe. Masoud Abrahmani kuhusiana na kadhia iliyokuwepo katika eneo la Kizimbani, baadhi ya watu ambao wamejenga katika maeneo yale na ile kadhia kubwa ya minazi. Jukumu kubwa ambalo tuendelee kumuomba Mheshimiwa Mwakilishi husika asikae na watu wake angalau kwenda kutoa taarifa katika ngazi stahiki na uhatarishi wa minazi ile ili kuweza kuiondoa ili kuweza kutoa ile hali ya hatari iliyokuwepo katika mazingira haya.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika Idara nyengine ya Tume ya Uchaguzi. Tupokee pongezi za Waheshimiwa Wajumbe na tukubaliane na Kamati baadhi ya zile changamoto ambazo ameziainisha katika ripoti yao, lakini tumpe pongezi sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein kwa kuwa na dhamira ya dhati ya kutatua changamoto nyingi ambazo wenzetu wa Tume ya Uchanguzi wamekuwa wakikabiliana nazo. Bahati nzuri sana mpaka hivi sasa baadhi ya changamoto nyingi ambazo Kamati imeziainisha ile ya upungufu wa majengo na kile kiwanja ambacho amekisema tayari Mhe. Rais ameshatolea ufafanuzi jambo hilo kwa sasa limeshatatuliwa haraka.

Lakini pia upo baadhi ya ushauri ambao baadhi ya ushauri ambao baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wameutoa kwamba ni vyema na hili lilizungumzwa na Mhe. Muhammedraza kwamba ni vyema inapofika wakati wa uchaguzi mikutano ya kisiasa hasa katika vyama vikubwa vya kisiasa *at least* ifanywe katika siku tofauti. Nimwambie Mheshimiwa Mjumbe kwamba wazo lake tumelichukua, tutalifanyia kazi wakati utakapofika tutaona haja na tija namna gani ambavyo tutaendelea kulikabi.

Mhe. Naibu Spika, pia tuzungumze suala zima la *TASAF* ambalo Waheshimiwa Wajumbe wengi wamekuwa wameligusia kwa namna moja ama nyengine. Mhe. Naibu Spika, hili naomba tuliseme tena kwa masikitiko tunaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, tunaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wa Majimbo, ambao kwa namna moja ama nyengine wanufaika wengi wa *TASAF* wamekuwa wakitokana katika majimbo yetu na Shehia zetu. Kwanza tumsahihishe Mhe. Suleiman Mwakilishi wa jimbo la Ndagoni kwamba kilichoainishwa pale si kaya ni jumla ya Shehia ambazo wamekuwa wakinudaika na mradi huu wa Kaya Masikini kwa Unguja na Pemba.

Ingawa tunakiri kwamba sio shehia zote zilizokuwepo katika mpango, jambo kubwa ambalo tuwaombe Waheshimiwa Wajumbe watusaidie kwenda kutoa elimu kwa watu wetu sambamba na kuwaomba sana ndugu wananchi kwa ujumla kwamba tunapofika wakati wa kufanya upembuzi wa mambo haya ni vyema wananchi wakawa wakweli katika kutoa taarifa zilizokuwa sahihi maana taarifa zinapotoka sahihi inapelekea na wao wenyewe kuja kupata stahiki sahihi.

Lakini wapo watu ambao walitoa taarifa ambazo hazikuwa sahihi kuhofia wale walikwenda kuuliza baadhi ya zile taarifa, lakini matokeo yake wamekuwa watu ambao wana maswali mengi baada ya kuona namna ambavyo mgawanyo wa fedha zinazotoka huwa wao hawanufaiki wakati uhalisia wa familia zao zipo tofauti. Lakini bado tumekuwa tukiwaomba mnapopata jambo lolote katika mgao ule wa fedha za TASAF kuna fomu ya malalamiko omba, jaza, madhali ipo kwenye mradi taarifa zao zitahakikiwa, zitarekebishwa na mambo yao yataendelea kuwa sawa. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wajitahidi sana kushirikiana na nao.

Mhe. Naibu Spika, tukiri katika jambo ambalo wananchi wengi wanatushukuru sana na katika jambo ambalo wananchi wanaishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni mradi huu wa TASAF. Wananchi wengi wamenufaika na wananchi wengi wameweza kutoka katika hatua moja kwenda katika hatua nyengine ya kupunguza ule ukakasi wa umasikini katika kaya zao.

Mhe. Naibu Spika, tukubaliane na tunapokea mawazo ya kamati kwamba baadhi ya waratibu wetu na Waratibu wa Dar-es-Salaam, tunakubali na tunakiri, bahati nzuri tulipokwenda Dar-es-Salaam na mimi tuliambatana nao, tumeona tuliyoyaona na tumejifunza tulichojifunza. Lakini tunastahiki tuwaambie Waheshimiwa Wawakilishi kwamba mradi wa *TASAF* Zanzibar ni miongoni mwa sehemu ambayo umekuwa na mafanikio kuliko Mikoa yote Tanzania. Kwa hivyo tuwaambie tu waheshimiwa pamoja na changamoto nyingi zilizokuwepo lakini tunapofika kuzungumzia mradi wa *TASAF* hata wale wenzetu wa Makao Makuu wanatwambia nyinyi mmewezaje kufanya yote haya. Katika Kaya nyingi, ukenda katika *TASAF I, TASAF II* na hata sasa hivi tupo katika *TASAF III*.

Lakini hata katika suala zima la ulipaji wa fedha za Kaya masikini pia bado kwetu kumekuwa kuna urasimu mdogo kuliko katika maeneo mengine. Kwa maana hiyo Waheshimiwa Wajumbe pamoja na changamoto ndogo

mnazozipata katika maeneo yote tukiri tu kwamba mradi huu umekuwa na manufaa makubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Suleiman wa Ndagoni alimazia kwa kuzungumzia suala la Wananchi wa Kijichi, Bububu mpaka maeneo ya Nguruweni kwamba kuna watu ambao walipata hati na kuna watu ambao hawakupata hati. Mhe. Naibu Spika, tuombe tu kwa kulieleza Baraza lako tukufu pamoja na kuwaambia wananchi wa shehia zile husika kwamba kauli ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ilikuwa tayari sekta husika iende ikatoa hati baada ya kukubaliana kwa masharti yote baina ya Wizara na Wananchi wale kwa ujumla.

Taarifa zilizokuwepo kwamba hati kwa hatua iliyofikia kwamba hati zimetoka. Sasa hili kwa bahati kuna baadhi ya wananchi hawakupata hati bahati mbaya ilikuwa halijafika rasmi. Lakini kwa sababu sasa limefika tutarudi tutatizama tatizo liko wapi ili kujua sasa tamko la viongozi wetu linapotoka, wakati mwengine liweze kufanyiwa kazi kwa muda mfupi.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie suala zima la wakala Wachapishaji *Press.* Waheshimiwa Wajumbe tunaokubaliana nao na tunapokea baadhi ya michango yao ya ushauri wao katika hili, lakini tukubali tu kwamba serikali imedhamiria kuboresha kuwa katika kiwango kikubwa sana wakala huu wa uchapishaji. Idara nyingi na taasisi nyingi za serikali na hata zile zisizokuwa za serikali zimekuwa zikichapishiwa kwenda kufanya kazi zake wa wakala.

Bahati nzuri wakala amekuwa akifanya kazi kubwa na ya kizalendo hasa kusaidia jamii zetu. Lakini suala zima baadhi ya wajumbe wamezungumzia baadhi ya idara za serikali kuwa hazilipi madeni. Hili Mhe. Naibu Spika, Wakala kupitia idara husika wameweka utaratibu mzuri wa kuwa wanarudisha hayo madeni ili kuweza kukipa uhai kiwanda chetu. Dhamira kwamba kiwanda kile kiendelee kufanya kazi vizuri na hata kupokea kazi nje ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lakini ilizungumzwa kwamba mpaka sasa kiwanda ama *Press* mpaka sasa hakijafanikiwa kuchapisha gazeti la Zanzibar Leo. Mpaka sasa idara kupitia na wizara pamoja na Wizara ya Habari kwamba tumeshafikia katika hatua nzuri ya kufanya makubaliano ili kuweza kuchapisha gazeti la Zanzibar Leo. Kilichokuwepo sasa na kilichobaki kwamba ni hatua tu ya wenzetu watu wa Wizara ya Habari kukubali zile gharama ambazo watu wa Wakala wameziwasilisha kwao wakikubali basi kiwanda kitaanza kuchapisha gazeti la Zanzibar Leo kama ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wamekuwa wanahamu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie moja ambalo fupi ingawa Mhe. Waziri atalitolea maelezo ya kina. Mheshimiwa tukiri kwamba kadhia hii ya madawa ya kulevya kama ambavyo Wajumbe wengi wameisemea, hakuna mtu ambaye anafurahishwa nalo katika taifa hili. Sisi kama wizara tumekuwa tunafanya mipango mingi na tunaitekeleza kadri ambavyo sheria imekuwa ikituongoza katika kukabiliana na hili. Lakini tunakubaliana na baadhi Waheshimiwa Wajumbe lakini hatukubaliani moja kwa moja na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe kwamba serikali imekuwa ikijenga *Sober House* lakini hazikuwa na tija.

Dhamira ya kujenga *Sober House* sio tu kwamba serikali inataka kuhalalisha suala zima la madawa ya kulevya hapana. Kuwekwa na kuendelea kujenga *Sober House* ama kuzishughulikia *Sober House* ni dhamira ya kwamba serikali kutaka kuwasaidia wananchi ambao tayari wameshaathirika na janga hili kubwa. Sio jambo zuri na la busara kuwaacha watu wale kuzagaa katika maeneo ya mitaani, wakatu tunauwezo wa kuwa-*rehab* na kurudia katika hali zao za kawaida.

Sasa tuwaombe Waheshimiwa Wajumbe wakati mwengine serikali inakuwa ina nia njema na nzuri hasa katika kujenga *Sober House*, tulifananishe hili Mhe. Naibu Spika, serikali inatoa dawa za ARV bure pamoja na dawa za Ukimwi, haimaanishi kwamba kutoa dawa zile bure kwamba pia inakubali baadhi ya mambo yale au maambukizi yale yapate kuenea. Lakini dhamira ni kutaka kukabiliana nalo pia niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe katika kadhia hii ni vyema hii tukabeba ile *national identity* maana sote tutakapoungana kila mmoja kwa nafasi yake kila mmoja tuwajibike katika kupiga vita hii mbaya na ya hatari ya madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri malizia.

Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba tutakapoungana kwa pamoja na tutakapotoa mashirikiano kwa pamoja na kuacha kusema baadhi ya maneno ambayo hayawi na tija ya kuleta mabadiliko katika kupigana na vita kubwa hii ya madawa ya kulevya. Zaidi ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ripoti hii ya Kamati kama ilivyowasilishwa.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Mchangiaji wetu wanayefuata ni Mhe. Issa Gavu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti

wa Baraza la Mapinduzi, na baadae atachangia Mhe. Mohamed Aboud Mohamed Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Karibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukuwe nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kutoa mchango wangu, katika ripoti hii ya kamati kama ambavyo Mwenyekiti ameiwasilisha.

Awali kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa namna hekima, busara na uwezo mkubwa aliouonesha katika kutuongoza sisi wananchi wa Zanzibar, ni imani yangu kwamba tutafikia malengo ya maendeleo kama vile ambavyo chama chetu kimeweza kuahidi kwa wananchi wetu.
Pili Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa kamati, nimshukuru kwa sababu kubwa mbili. Kwanza yeye pamoja na kamati kwa ujumla tumekuwa tukifanyakazi kwa pamoja, maeleweno na mahusiano mazuri. Pili nawashukuru kabisa kwa kuweza kutusaidia kwa namna moja ama nyengine kuweza kuonesha katika hamasa na chachu ya kuharakisha maendeleo katika sekta ambazo wanazisimamia.

Mhe. Naibu Spika, jambo la tatu naomba niahidi tu kamati kwamba kwa kupitia ofisi ambayo naisimamia, niwaahidi kwamba waliyosema yote tutayachukua kwa niaba ya serikali. Niwaahidi utekelezaji wa maagizo yao tutawaletea na nina hakika tutafanikisha yale ambayo wameyakusudia.

Mhe. Naibu Spika, mambo makubwa yaliyozungumzwa ni takriban mambo saba. Jambo la kwanza ambalo limezungumzwa na wachangiaji wengi, lilikuwa linahusiana na ahadi za Mhe. Rais pamoja na viongozi wengine wa kitaifa. Niwaahidi tu Mhe. Naibu Spika, pamoja na Baraza lako tukufu kwamba ahadi zote za Waheshimiwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa, tutaendelea kuratibiwa, kufanikishwa kwa kila sekta. Imani yangu ni kwamba kadri uwezekano wa kupatikana fedha utekelezaji wa mambo hayo yatakuwa yanaendelezwa kutekelezwa mwaka hadi mwaka, hadi pale kipindi cha uongozi kitakapoondoka na kama Rais mwengine ajaye ni wajibu wake kuchukua ahadi hizo na kuziendeleza, kwa sababu serikali itaendelea kuwepo daima na dawamu. Wataondoka viongozi lakini wanaokuja wataendelea kurithi matunda mema yote yaliyoanzishwa na viongozi waliotangulia kabla yao.

Suala la pili Mhe. Naibu Spika, lililojitokeza lilikuwa ni suala zima la viongozi wetu wakuu wanaposafiri. Niombe tu Mhe. Naibu Spika, kwamba jambo hili nalo ni mamlaka za viongozi hawa, kuwaacha watumie busara na hekima zao, kwa kuona kwamba katika safari zao hizi wataweza kuwashirikisha wale watu ambao watakuwa na umuhimu na ulazima wa kuambatana na wao katika safari ile. Sio busara kwamba kila safari kumlazimisha kiongozi aweze kumchukua mtu fulani.

Ni hekima na busara pamoja na mahitaji ya safari husika ndio yanayomuongoza kiongozi kwa kuona nani wa kukutana naye katika kufanikisha jambo ambalo anaazimia kwenda kulifanya. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wataelewa kwamba viongozi hawakuwa na desturi hiyo na itaendelea kila inapotokea haja ya kuona katika ujumbe wao wanachukua watu kwa ajili ya kwenda kuwasaidia yale malengo waliyokusudia katika safari husika.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, lilizungumzwa suala la bajeti, hasa katika kitengo chetu cha *GSO* pamoja na Idara ya Mawasiliano, niwahakikishie kwamba tutajitahidi kadiri ya upatikanaji wa *resource* ya fedha, mambo haya nayo tutayazingatia. Lakini katika hili la mawasiliano, imediriki kusemwa hapa kwamba labda tuko nyuma katika sekta ya mawasiliano, kutokana na mabadiliko ya technolojia ilivyo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, inawezekana ikawa kuna mabadiliko ya leo na jana, ambayo hatujaweza kuya-*capture*, lakini Idara yetu ya Mawasiliano iko vizuri katika msingi wa maendeleo, hasa kwa upashaji wa taarifa. Kama kuna mapungufu yatakuwa ni mapungufu madogo sana. Mhe. Naibu Spika, napenda kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba idara yetu imeweza kupata vifaa vya kisasa na muhimu katika utendaji, tunaamini kwamba tuna nafasi ya kuendelea kuwakuza na kuwaendeleza wafanyakazi wetu katika kuwaimarisha hasa katika sekta ya mawasiliano, hasa mawasiliano ya kisasa kwa maana kwamba IT.

Ni hivi majuzi tu Mhe. Naibu Spika, tumeweza kupata *camera* ya kisasa kabisa, *camera* ambayo wame-*launch* kule Marekani katika mwaka 2017, ndio *camera* ambayo wanatumia watu wetu wa idara ya mawasiliano, *camera* ambayo Mhe. Naibu Spika, unao uwezo wa kupiga picha kwa namna tatu. Unao uwezo wa kupiga picha za *still*, unao uwezo wa kupiga picha za *video*, lakini pia unao uwezo wa kutengeneza picha katika mfumo ule wa mubashara, kwa maana kwamba *live screen* katika *facebook, twitter, Whatsapp* na mambo mengine kama hayo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine lililozungumziwa lilikuwa suala zima la ukaribu wa Mhe. Rais, pamoja na jamii kwamba labda kuna kizingiti, hapana. Mhe. Naibu Spika, jambo kubwa na muhimu ni kufuata taratibu za kuweza kukutana na Mhe. Rais. Sote ni mashahidi, Mhe. Rais amekuwa mtu wa karibu sana na jamii, na watu anaowaongoza. Mhe. Rais anashiriki misiba, anashiriki shughuli za kijamii, ikiwemo harusi. Kwa bahati nzuri kuna mjumbe mmoja alizungumzia hapa, nadhani alighafilika kwa sababu yeye mwenyewe ni shahidi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais tulikwenda kwenye harusi moja usiku na mjumbe huyu alikuwa ni miongoni mwa wasimamizi wa shughuli ile. Lakini Mhe. Rais anashiriki katika michezo, mazoezi, shughuli za kitaifa, anashikiri katika shughuli za kijamii nyengine, ni imani yangu kwamba yeyote anayetaka kumuona Mhe. Rais kwa kutumia utaratibu uliopo, hakuna kipingamizi kinachomtenga Rais na jamii, au wananchi anaowaongoza.

Msingi ni kufuata taratibu, maelekezo ambayo utapewa na wasaidizi wake, na matarajio yetu ni kila mmoja atapata nafasi ya kukutana na Mhe. Rais kufanya mazungumzo yake, kupeleka ombi lake, kupeleka kilio chake na Mhe. Rais ni msikivu atamsikia na kama kuna vya kumuelekeza atamuelekeza.

Jengine Mhe. Naibu Spika, lililozungumzwa kwa mapana ni suala zima la ujio wa viongozi wakuu wa kitaifa au wa kimataifa wanapokuja nchini kwamba wanaishia upande wa pili wa Dar es Salaam. Suala hili tumelichukua na sisi kama serikali tutaweza kuona namna gani tunaweza kuliona jambo hili linaleta taswira ya waasisi wa Muungano wetu, kwa kuona kwamba kiongozi yeyote wa nje anapokuja lazima afahamu kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina pande mbili, upande wa Tanzania Bara na upande wa Zanzibar na ni wajibu wake kwamba taasisi ama sekta husika, hasa Wizara ya Mambo ya Nje kulizingatia hilo na matarajio yetu kwamba wenzetu watalipa uzito unaostahiki kwa kuona jambo hilo linafanyika kama vile ambavyo lilikuwa likifanyika awali, litaendelea kufanyika na kipindi hiki na litaendelea kufanyika kwa siku zijazo za usoni.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache na mimi naomba niseme kwamba. Jengine nimekumbushwa hapa lilikuwa ni suala zima la ukarabati wa majengo yetu, hasa kutokana na matatizo ya mmong'onyoko, niahidi tu kwamba mambo haya tutayachukulia uzito unaostahiki na tutakapokuja na taarifa mambo haya tutakuwa tumeyaeleza, pamoja na lile suala zima la jengo letu analotumia Mhe. Rais kwa upande wa Dara es Salaam, jengo la Laiboni.

Jengo lile tulichelewa kulipata kwa maana kwamba kumilikishwa, ahadi yetu kwamba baada ya kumilikishwa mwaka 2015 mwishoni, matarajio yetu sasa tutaona namna gani serikali tutajipa kipaumbele maalum katika kutenga fedha ili kuweza kufanya marekebisho mazuri, kujenga taswira na haiba ya Mhe. Rais hasa kwa kuzingatia mazingira ya mtaa ule ambao anaishi pale Dar es Salaam.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba na mimi naunga mkono hoja hii ya Mwenyekiti, niahidi kwamba utekelezaji wa yale atakayoyatoa katika kamati hii basi na sisi tutaleta majibu kwa maandishi. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Sasa nimkaribishe Mhe. Mohamed Aboud Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, na baada ya hapo ajitayarishe Mwenyekiti wa kamati.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutukutanisha na kutuwezesha kuendelea na shughuli zetu katika Baraza letu hili tukufu.

Aidha, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Pia niwashukuru viongozi wetu wakuu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa namna wanavyotuongoza katika kutekeleza majukumu yetu, wanatumia hekima na busara kubwa ili tuweze kupata nafasi nzuri ya kutimiza wajibu wetu.

Aidha, nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, kwanza kwa uwasilishaji mzuri wa ripoti ya kamati hii. Lakini pia niwashukuru wajumbe wote wa kamati hii, kwa namna ambavyo ripoti yao ilivyokuwa imekamilika vizuri na imetayarishwa vizuri, nawashukuru sana na nawapongeza sana. Vile vile niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, ambao walipata nafasi ya kutoa michango yao, michango ambayo ilikuwa na nia ya kurekebisha na kutupa mwanga zaidi katika utekelezaji wa majukumu yetu, nao pia niwapongeze sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa ufupi sisi kwa upande wetu tunaipokea ripoti hii tutaifanyia kazi na yako yale ambayo nitayatolea ufafanuzi kidogo, lakini kwa ujumla wake tutakwenda kuifanyia kazi kama maelekezo ya kanuni yanavyotaka mwezi wa Septemba tutatoa taarifa yetu kwa maana ya kujibu kila hoja iliopo katika taarifa hii. Kwa sababu ni utaratibu wa sasa ambao tumejiwekea huo kwa mujibu wa kanuni.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda nisisitize jambo moja ambalo Mhe. Mussa Foum alilizungumzia, kuhusu suala la nidhamu katika chombo chetu hiki kikubwa. Wananchi wote wa Zanzibar, Tanzania na dunia inakiona chombo hiki. Kwa hivyo, jambo lolote lile ambalo linatutoa katika mstari, katika utaratibu wa kanuni zetu basi huwa sio jambo zuri kufanywa na Waheshimiwa Wajumbe ambao wameaminiwa kwa kiasi kikubwa kuendesha chombo hiki kuwa ni sehemu ya uongozi wa nchi yetu. Kwa hivyo, napenda sote tuwajibike vizuri katika kufanya mambo yetu, ili chombo chetu hiki kiendelee kujijengea sura na taswira ya heshima yake ambayo tumeanza nayo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo niseme kwamba kwa ujumla ofisi yetu hii ilichangiwa sana katika maeneo yanayohusu Tume ya Kuthibiti Madawa ya Kulevya, Tume ya Uchaguzi, suala la kukabiliana na maafa, suala la uwakala wa uchapaji, kero za Muungano na vile vile masuala ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, nianze suala hili la madawa ya kulevya. Kwa sababu ndio lililozungumzwa kwa kiasi kikubwa sana na kwa ushabiki mkubwa. Lakini yaliyozungumzwa maana yake wajumbe wanaonesha au wanatoa kilio chao kiweze kusikika kwa serikali, kiweze kusikika kwa jeshi la polisi, kiweze kusikika kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, kiweze kusikika kwa ofisi ya *DPP*, kiweze kusikika katika mahakama, kiweze kusikika kwa wapelelezi wetu na wananchi wote waliloonesha *concern* yao na masikitiko yao ya namna ambavyo matokeo yanayoendelea nchini kwetu katika masuala haya haramu ya madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niwaunge mkono sana, jambo hili sote linatugusa na ni wajibu wetu kwa pamoja, sio la mtu mmoja mmoja kushirikiana, kupambana nalo na kuliondoa katika nchi yetu. Nataka niseme wazi kwamba Mhe. Rais wetu yuko mstari wa mbele katika mapambano haya, na tayari ametoa maelekezo ya hatua mbali mbali za kuchukuliwa dhidi ya wahusika wote wa uhalifu wa madawa ya kulevya. Nataka nimpongeze pia kwa kuendelea kumteua Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuwa Mwenyekiti wa tume hii inayosimamia madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kamanda wetu huyu tutakuwa naye kwenye mapambano hayo na nina amini ataliendesha vizuri jahazi letu. Kwa hivyo, Mhe. Rais yuko mstari wa mbele, kinyume na dhana ya wengine ambao wanayo kichwani mwao. Lakini viongozi wetu wakubwa hawa wana hekima, busara na wana taratibu zao katika kuongoza kwao, cha msingi utekelezaji ufanyike kama inavyofaa. Sasa yeyote yule ambaye hakutekeleza maelekezo hayo maana yake ajue hicho ni kipimo cha kazi yake aliyonayo, ikiwa kiongozi, ikiwa askari, ikiwa unatoka

kwenye ulinzi na usalama, hata ukitoka kwenye ofisi ya *DPP* na wengine wote, tunatakiwa tuwajibike tufanyekazi zetu vizuri, ili tutekeleze wajibu wetu kwa msingi wa kuwatumikia wananchi wetu. Kwa hivyo, kwa upande wa serikali, sisi mapambano yameanza na tutaendelea kupambana na kila muhalifu katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, lakini nataka niseme kwamba tumeridhika sana na maoni ya Waheshimiwa Wajumbe, na sisi tuko tayari kushirikiana nao ili tuondoshe kadhia hii katika nchi yetu, isiendelee kutokea na wale wote wanaohusika, ama wanaosaidia, ama wanaoshirikiana nao, ikiwa kiongozi, ikiwa askari, ikiwa Ofisi ya DPP, ukiwa kutoka mahakamani, basi wote mkondo wa sheria uchukuwe nafasi yake na wao wapate adhabu kwa mujibu wa sheria. Hakuna waziri wala hakuna yeyote yule ambaye atashiriki au kusaidia vitendo hivi na yeye mkondo wa sheria utamchukua.

Mhe. Naibu Spika, kwa ufupi ni jambo ambalo sote tunatakiwa tushirikiane, hakuna suala la papa wala dagaa wote watakumbana na mkondo wa sheria. Cha msingi hapa ni kupeana taarifa tunapoyaona mambo haya, wananchi wana wajibu wa kutoa taarifa, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu katika majimbo yenu, mnao umuhimu mkubwa wa kuongoza mapambano hayo katika majimbo. Maana huko kwenye jamii ndio mambo yanatokea, hivyo tushirikiane, tuambizane, tusaidiane ili kazi hii ifikie hatua nzuri kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, lile suala ambalo limezungumzwa katika kujenga *Sober House*, sisi tunaendelea kusaidia madawa sio dhana yetu. Wale ambao tayari wameathirika wanapelekwa kwenye *Sober* kwa sababu ya kupata *counselling* ili kuacha na warudi kuwa raia wema, washirikiane na wanachi wenzao.

Matatizo ya msingi ni kwamba hawa vijana wetu wamefikia kuwa kama magoigoi, kama wendawazimu kutokana na mambo haya ya hatari kabisa kwenye maisha yao. Kwa hivyo, kinachofanyika ni kumrekebisha sio kumuendeleza akafanya masuala ya madawa ya kulevya. Ndio maana zile *sober* ambazo hazifuati taratibu tunazifungia, na tutaendelea kuzifungia *sober* yoyote ambayo haifuati masharti kama haya. Kupitia kwao tuna taarifa nyingi, wanatupa taarifa za namna ya kuweza kuwashughulikia wahusika wa madawa ya kulevya. Nawahakikishia wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba kila muhalifu hatoogopwa, wala hatutomuonea huruma na shughuli itafanyika kwa mujibu wa sheria ili kila mmoja apate adhabu ya sheria.

Waheshimiwa Wajumbe, kuhusiana na upekuzi katika *Airport* na bandari, utaratibu umeshawekwa na vyombo husika vitafanya kazi zao kwa mujibu wa taratibu zilizopo. Kwa hivyo, naomba tu tuendelee kushirikiana vizuri, ili jambo hili sote kwa pamoja tuwe ni washiriki na tupambane.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na kazi za tume. Kuna baadhi ya wajumbe walichanganya kidogo kwenye kazi za tume hii ya madawa ya kulevya. Kazi za tume zaidi ni za kisera, kutoa muongozo kwa namna ya kuratibu, na namna ya kudhibiti madawa haya ya kulevya, na utekelezaji vipo vyombo vinavyohusu utekelezaji. Mtekelezaji namba moja ni Jeshi la Polisi, ndio anatakiwa afanye upelelezi, akamate, atoe ushahidi sahihi na apeleke katika ofisi ya *DPP*, na ofisi ya *DPP* itengeze sasa ushahidi vizuri, itengeneze utaratibu wa kuifikisha kesi hiyo mahakamani, ule ushahidi unaotolewa na polisi uwawezeshe *DPP* kutengeneza sasa namna nzuri ya kesi ya kuiwasilisha mahakamani, na mahakama ndio sasa itatoa hukumu kutokana na maelezo mazuri atakayotoa *DPP* na *DPP* atakavyoweza kuitetea kesi hiyo hapo mahakamani.

Kwa hivyo, tume inatekeleza wajibu wake, yeye sio mtendaji, vyombo vitatu vikubwa hivi kila mmoja vina wajibu kwa mujibu wa sheria. Polisi ndio namba moja kwa maana ya kwenda kupeleleza na kuwakamata, ili waende katika vyombo vya sheria. Ofisi ya DPP ndio inatengeneza utaratibu sasa kutokana na ushahidi wa polisi, kuweza kuwasilisha kesi hiyo mahakamani. Naamini yapo mashirikiano mazuri katika sekta hizi tatu ambazo kwa sasa mapambano haya yataweza kufanyika vizuri. Nawaamini sana kwa namna walivyojipanga shughuli hii itafanyika vizuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini tume hii ina vitendea kazi vya kutosha vya kuweza kufanya wajibu wake na wajibu wao wanaufanya vizuri sana. Maana wajibu wao wanatoa kila taarifa, kila wanachokipata na miongozo ambayo inawawezesha hawa watendaji kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, tume hainyimwi nafasi ya kufanya kazi zake inayo nafasi nzuri ya kufanya kazi zake, hapa imeelezwa kwamba wamekosa hata magari Tume hawajakosa magari wanayo magari yao ya kufanya kazi zao na vitendea kazi vyengine vya kufanya kazi zao.

Suala la Mawaziri kupewa magari ni stahiki zao na nataka niseme hakuna Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwenye gari linalofika milioni 200 hata nusu yake ya fedha hizo hawana, katazameni magari ya Mawaziri wengine Duniani hapa Tanzania Bara tu mtawaona kwa hivyo muone kwamba Mawaziri wetu hawa wako tayari wazalendo kutumika nchi yetu, na wao hawana ulazima wa kupata gari nzuri wana ulazima wa kupata gari ya

kufanyia kazi zake. Kwa hivyo si vizuri mambo mengine tukiyasema kwa sababu wananchi wanayasikia huko wanadhani Mawaziri hapa wanakula viyoyozi tu wako katika kazi na ni stahiki yao ya kupata hivyo. Kwa hivyo ni vizuri Waheshimiwa Wajumbe tukashirikiana kufanya mambo ya msingi mambo ambayo yataunganisha wananchi na Serikali yao, mambo ambayo yatawezesha kujenga umoja na maelewano katika nchi yetu kwa maslahi yetu pamoja. Mimi nataka nikubaliane na nyinyi kwamba kila atakayeshiriki katika jambo hili tushirikiane tumtie mbaroni ili mkondo wa Sheria uchukue nafasi yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya Uchaguzi malalamiko mengi yalikuwa kuhusu majengo ya Tume ya Uchaguzi pale katika Ofisi Kuu ya Tume, nataka niwahikikishie sana Waheshimiwa kwamba wajumbe wa Baraza hili pamoja na wananchi kwa jumla kwamba Mhe. Rais ametoa maelekezo mazuri sana kuhusu Ofisi za Tume, hivi karibuni alitembelea pale akaona yale majengo kwanza ameunda kamati maalum au ametoa maelekezo kwa Mawaziri husika kuhakikisha kwamba Tume wanapewa majengo yale walioko sana yanakuwa ni yao, lakini pia kuna jengo la ziada wameliomba nalo linashughulikiwa ili pia wakabidhiwe Tume ya Uchaguzi.

Kwa msingi huo watakuwa na majengo yanayotosheleza kwa mahitaji yao ya kazi na pia kama ghala la kuwekea vifaa vyao muhimu kwa shughuli zao za Tume ya Uchaguzi. Hata ule wasiwasi wa kiwanja jirani cha mtu binafsi basi jambo hilo pia limewekewa utaratibu wake na namna nzuri ya kushughulikiwa ili maeneo yale yote yaweze kudhibitiwa na Tume kwa ajili ya usalama wetu na usalama wa Tume yenyewe. Kwa hivyo nataka nimshukuru sana Mhe. Rais kwa maelekezo yake nataka niwakikishie wajumbe na Tume yenyewe ya Uchaguzi kwamba mambo yamepangwa vizuri, kwa hivyo kwa upande wa Ofisi kuu pale kila kitu kinakwenda sawiya. Kwa upande wa Ofisi za Wilaya tayari tunayo maelekezo ya namna gani ya kushughulikia zipatikane Ofisi za Wilaya za Tume ili Tume katika kila Wilaya ziwe na ofisi yake nzuri waweze kutenda kazi zao vizuri. Halikadhalika na upande wa magari ufafanuzi umetolewa na utaratibu umewekwa nataka niwahikishie kwamba Tume mengi ya mambo yao yatatekelezwa ili wafanye kazi zao kwa ufanisi kwa maslahi ya watu wote wa nchi hii.

Kuhusu masuala ya kampeni namshukuru sana Naibu Waziri amelitolea ufafanuzi vizuri jambo hili nina hakika aliyoyasema ni sahihi kabisa, sisi tutahakikisha tunafanya uchaguzi huru haki na salama kama kawaida yetu tunavyofanya chaguzi zote. Mianya yote itazibwa ya wale wakorofi wanaofanya mbinu kuharibu uchaguzi halafu wanalalamika lalamika mianya

hiyo tutahakikisha inazibwa na tume ili tuwe na uchaguzi huru na salama na amani.

Kuhusu wa wakala wa uchapishaji lengo hapa ni kuimarisha kiwanda hichi, Mhe. Naibu Waziri kasema vizuri nataka niwahikishie Waheshimiwa jambo moja ambalo ni muhimu sana kuwa nalo katika kuendeleza kiwanda kile ni suala la wataalam au watendaji katika kiwanda, tayari tangazo la kuajiri wataalam limetolewa na wakati wowote taratibu zitakapokamilika tutapata baadhi yao. Kwa wale wataalam maalum tumepewa ruhusa na Serikali kuajiri kwa mujibu wa mkataba na wapo baadhi ambao tayari wameajiriwa, nia na dhamira kiwanda kile kijiendeshe vizuri, kitoe huduma bora kwa wakati na kiweze chenyewe kujitegemea kisitegemee Serikali kijiendeshe kwa faida, na huduma za Serikali izafanywe kwa wakati na kwa uzuri na ubora wake.

Kwa msingi huo kila hatua ya maana itakayohitajika itachukuliwa ili kuhakikisha kwamba kiwanda kile kinatoa huduma bora na kwa wakati na kinajiendesha kibiashaha. Na ule ushauri mliotupa kwamba tukitangaze tayari kuna makakati maalum wa namna gani ya kukiimarisha kiwanda kile ili kiweze kuingia katika soko vizuri, nawashukuru sana kwa ushauri na maelekezo yenu.

Kwa upande wa Kamisheni ya Maafa Mhe. Naibu Spika, dhamira na nia ni kuimarisha huduma za kujitayarisha ili yanapotokea majanga tuweze kuyakabili vizuri tupunguze maafa yanayoweza kutokea hiyo ndio hatua inayochukuliwa kila wakati, kulitolewa ushauri hapa wa kuwa na eneo maalum kujenga jengo maalum kwa ajili ya waathirika wa maafa yanapotokea, si jambo rahisi kusema ujenge mahala fulani jengo la kuweka waathirika wa maafa yanapotokea.

Maana yake kwa ufupi mara nyingi yametokea maafa sana kwa hapa Mkoa wa Mjini wa Unguja sehemu ya mjini, kwa hivyo ndio maana tukatumia skuli za mjini hapa Unguja kwa ajili ya kuweka wale waathirika, sasa ukisema ujenge hapa mjini lakini maafa Mungu atupishie mbali yametokea Kojani utamtoa Kojani mlete hapa mjini ni tatizo, cha msingi hapa ni kununua vifaa na mahema maalum ambayo tutaweza kuyatumia mahala popote litakapotokea tatizo kuyapeleka ili kustiri watu wetu ndio jambo la msingi hatuwezi kujenga mahala. Lakini kuna maeneo ambayo kwa upande wa usafiri wa baharini hayo yameonekana ni hatarishi kama vile Malindi, Nungwi, Chake-Chake, Wete, Mkoani mle mmeamuliwa kujengwa vituo maalum ili kutoa huduma za dharura pale matatizo yanapotokea, hivi sasa tunaimarisha sehemu yetu ya mawasiliano pale Maruhubi ili kuwa urahisi zaidi kuifikia hii Kamisheni ya Maafa na iweze kutoa huduma zake.

Kwa upande wa mfuko wa Maafa tayari Sheria imeshatoa nafasi na mfuko umeshaundwa na utaratibu utatokana na zile fedha zinazokusanywa katika mfuko wa miundombinu, katika fedha za mfuko wa miundombinu asilimia 25 itakwenda kwa mifuko mbali mbali ikiwemo Mfuko wa Maafa, Mfuko wa Ukimwi na kadhalika. Kwa msingi huo sasa mfuko huu utaratibu unafanywa ili uanze kupata hizo fedha kwa mujibu wa sheria ili sasa tupunguze tatizo hilo ambalo mara nyingi limekuwa likijitokeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla Serikali imeendelea kuchukua hatua ya kuimarisha zile sekta muhimu zinazoweza kutoa huduma za haraka yanapotokea maafa kama vile kikosi chetu cha KMKM, kikosi chetu cha Zimamoto na Uokozi vimepiga hatua kubwa na bado Serikali ina mipango kabambe ya kuimarisha vikosi hivi ili kuweza kutoa huduma za dharura pale zinapohitajika kwa nia ya kuokoa na kwa nia ya kusaidia panapohitaji msaada huo. Kwa ufupi Serikali itaendelea kutoa kila msaada kuhakikisha wananchi wetu wanahifadhika na kuepukana na majanga ambayo yanaweza kuleta athari kubwa mbele yetu. Kwa ufupi suala zima la elimu kwa umma na mashirikiano litahitajika ili kufanya mambo haya kwa pamoja, tulipewa ushauri hapa wa namna ya kushirikiana na Wilaya na Shehia huo ndio utaratibu wenyewe tuna kamati katika kila ngazi za utawala kwa msingi wa kupambana na maafa yanapotokea.

Suala la Tume ya UKIMWI Mhe. Naibu Waziri amelieleza vizuri sina haja ya kurudia.

Kuhusu Ofisi ya Uratibu Dar es Salaam Serikali ina mpango mkubwa wa kuimarisha ofisi hii sio kufanyia ukarabati jengo lile, lakini jengo lile litajengwa upya la kisasa ili ofisi yetu pale ionekane ya aina yake na hadhi ya ofisi ile Serikali imeshatoa maelekezo iwe na hadhi maalum na kwa sasa ofisi imeshaanza kupata magari kwa kuanzia, kwa hivyo waheshimiwa viongozi sasa mtakapokwenda Dar es Salaam mtaanza kupata huduma hizo kwa kiasi fulani, lakini bado tutaendelea kutafuta magari ya ziada kwa ajili ya kutoa huduma zake. Hapa cha msingi ni kwamba ofisi ile itaendana na hadhi ya eneo lile na hadhi ya sura ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa upande wa ajira katika vyombo vya Muungano ukiondoa vyombo vya ulinzi na usalama kwenye sekta nyengine za mambo ya Muungano tulishakubaliana muda mrefu kwamba asilimia 21 ni kwa wananchi wa Zanzibar na asilimia 79 kwa upande wa Bara. Kwa hivyo hili jambo limeshaamuliwa na maamuzi yamefikia hamna haja ya kulirudia. Waziri wa

utumishi hapa Mhe. Haroun ananikumbusha kwamba wameshakutana kuweka mipango vizuri zaidi hongereni sana.

Kuhusu tatizo la magari na tatizo la bidhaa kwenda Dar es Salaam Mawaziri wa Fedha wameagizwa jambo hilo wanalishughulikia na muda sio mrefu tatizo hili litamalizika. Dhamira ni kuondoa kero zote katika Muungano wetu ili kuimarisha Muungano wetu. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu na Waheshimiwa wananchi wote waelewe dhamira njema za viongozi wetu wakuu kwa maana ya Rais Dkt. Ali Mohammed Shein na Rais Dkt. John Pombe Magufuli dhamira yao ni kubwa kwenye Muungano wetu, dhamira yao ni kuondosha kila aina ya tatizo, dhamira yao ni kujenga Muungano mzuri utakaofanya Watanzania wanaishi kwa furaha katika nchi yao kwa maendeleo makubwa, kwa hivyo sote tuunge mkono juhudi hizo za viongozi wetu hawa wakubwa na tuwaombee ili mambo yao yaende vizuri zaidi.

Kuhusu kufungua *Consulate* hapa Zanzibar, uamuzi wa kufungua *Consulate* ni wa nchi yenyewe tunayo *Consulate* ya Oman hapa, tunayo ya India, Tunayo ya China, tunayo ya Egypt, tunayo ya Msumbiji na kadhalika. Kwa hivyo kila anayetaka ni uamuzi wa nchi husika na utaratibu unafanywa na anaruhusiwa kufungua *Consulate* wala hatuna matatizo ya aina yoyote.

Kwa upande wa *TASAF* ilizungumziwa kwamba watu wenye ulemavu wanabaguliwa sisi hatubagui yoyote na tunapaswa kuwasaidia zaidi watu wenye ulemavu kupata huduma hii ya *TASAF*. Kwa hivyo nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba tutazidi kuweka kipaumbele maalum kuona wenzetu wenye ulemavu wanasaidiwa vipi katika miradi hii ya *TASAF* ili waweze kupata huduma hizi kama wanavyopata wananchi wengine, mpaka sasa mradi huu wa *TASAF* kwa upande wa Zanzibar umeshatumia zaidi ya bilioni 13.6 kwa ajili ya kusaidia kaya masikini elfu 33,042 ambazo kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri za Shehia 204. Kwa hivyo ni mradi ambao una umuhimu mkubwa na tunaupongeza sana ili uzidi kuendelea.

Kuhusu kulea ile miradi iliyoanzishwa na *TASAF 1* na *TASAF 11* sasa hivi tunafanya tathmini hiyo kwa msingi ya kuwa miradi ile iwe endelevu na sekta husika zichukue nafasi yake katika kuendeleza miradi hii ili fedha zile ambazo zilitumika kutokana na miradi ya *TASAF* zizipotee, kwa hivyo naunga mkono sana na ushauri wenu tunaushukuru ili shughuli hii ifanyike vizuri.

Kuhusu Idara ya Watu wenye ulemavu tunapokea ushauri na tunajitahidi kila mara kutafuta vitendea kazi yakiwemo magari ili Idara hii iweze kupiga hatua. Lakini pia suala la kuwa na mazingira rafiki kwa miundombinu na majengo huo ndio msimamo wa Serikali kwa hivyo ushauri wenu tunazidi kuupokea na Serikali inafanyia kazi jambo hili ili kujenga mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu waweze kupata huduma bora katika nchi yetu, ili na wao wajisikie kama wanavyojisikia raia wengine.

Kwenye suala la sheria na maadhimisho ushauri tumeupokea hatua za kuimarisha idara hizi zinaendelea na nataka kuwahakikishia kwamba tunafanya kila njia kuijenga idara hii vizuri ili iweze kutoa huduma bora kwa wananchi na kwa Serikali.

Kuhusu mfuko wa Jimbo kwanza niseme fedha za mfuko wa jimbo zipo tayari Wizara ya Fedha wameshatenga fedha, kwa sasa fedha sio tatizo sasa utaratibu ni marejesho kwa mujibu wa utaratibu wa sheria unapofanya marejesho unakuwemo katika orodha ya kupata hizo fedha. Sasa fedha lazima ufuate utaratibu. Fedha za jimbo ni za jimbo sio za Mwakilishi, Mwakilishi ni Mwenyekiti wa Kamati, kamati inatakiwa iwe kamati endelevu kusudi leo akiwepo kesho hayupo bado kamati iwepo na iwe endelevu iweze kutimiza matakwa ya Sheria ili fedha hizi zitoke vizuri zitoe huduma kwa wananchi.

Lakini kwa sababu kumelalamikiwa sana wa wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, tutaangalia ushauri wao ili Waheshimiwa Wawakilishi waweze kupata fedha hizi haraka iwezekanavyo, cha msingi tuheshimu na ile sheria iliyopo. Kwa sababu ipo siku Waheshimiwa Wawakilishi sheria ile itakuja kuwasuta, *CAG* anakuja hapa na ripoti yake watakuja kuambiwa Mheshimiwa fulani ka-*misuse fund* maana yake utapelekwa katika mkono wa sheria, Mheshimiwa mzima kupelekwa Mahakamani unashitakiwa kwa matumizi mabaya haiwi jambo zuri, tunachokifanya hapa ni utaratibu wa kutulinda sote.

Kuhusu A*ccount* lazima ziwe *Current Account* hatuwezi kufungua *Saving Account*, *Saving Account* ni ya mtu, ile ni *Account* ya umma lazima iwe *Current Account* katika majimbo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda unakwenda sana na Mhe. Mwenyekiti anakuja kujumuisha hoja hii iliyo mbele yetu na kwa sababu sisi kama Serikali tutawasilisha taarifa yetu Mwezi wa Septemba kama kanuni inavyotaka tutafanya hivyo, lakini niseme kwamba mashauri yaliyotolewa na kamati

tunaunga mkono, ushauri uliotolewa na Wajumbe tunaunga mkono. Ahsateni sana na mimi naunga mkono hoja hii.

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya Kamati yetu ya ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, sina budi na mimi tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukakutana na nachukua nafasi hii pia kuwapongeza wachangiaji wote ambao wameichangia ripoti ya kamati yetu, ripoti yetu ya Kamati ya Kusimamia viongozi Wakuu wa Kitaifa ilitakiwa ichangiwe na watu 29 kama si upungufu wa muda, hii ni kuonyesha wazi jinsi ya wajumbe walivyoipokea, walivyoifikiria na kuisoma na baadae kutoa maoni mbali mbali ambayo yametupa mwanga katika kazi zetu, ambao hatimae ni mwelekeo mzima wa Baraza letu la Wawakilishi na wa taifa kwa jumla Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya hapo napenda kuwatambua wachangiaji kwa ruhusa yako ambao wamechangia kwa maandishi kwa kusema na wale ambao wamechangia kwa maandishi, lakini nitaanza na wale waliochangia kwa kusema ni:-

1. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
2. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
3. Mhe.Mohammedraza Hassanali Mohammedali
4. Mhe.Abdalla Maulid Diwani
5. Mhe.Simai Mohammed Said
6. Mhe.Asha Abdalla Mussa
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8. Mhe. Bahati Khamis Kombo
9. Mhe. Sheha Hamad Matar
10. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
11. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
12. Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata
13. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
14. Mhe. Mussa Foum Mussa
15. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
16. Mhe. Suleiman Makame Ali
17. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)

18 Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni pamoja na:-

1. Mhe. Shaibu Said Ali
2. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
3. Mhe. Juma Ali Khatib Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum
4. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
5. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
6. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
7. Mhe. Mussa Ali Mussa
8. Mhe. Panya Ali Abdalla

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwenyekiti na Mhe. Mwantatu nafikiri kachangia na ameleta kwako

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Naomba pia kuwatambua na *Hansard* isome kuwatambua wachangiaji hawa ambao nimewasahau. Pia nachukua fursa hii kuwatakaradhi ambao sikuwataja ambao nimewasahau na tunathamini sana michango yao.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku bwana usitupotezee muda.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sasa utaratibu, msitupe kanuni.

Mhe. Naibu Spika: Wewe kila saa unataka ...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Msitupe kanuni mimi hakunitaja.

Mhe. Naibu Spika: Hapana sitaki, unanipotezea muda, sitaki kaa kitako sitaki, kaa kitako. Tunaendelea Mhe. Jaku huna sababu ya msingi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi sikutajwa nataka kanuni...

Mhe. Naibu Spika: Hapana Mheshimiwa sitaki kukusikiliza kaa kitako sitaki kukuzikiliza, Mheshimiwa endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi sikutajwa.

Mhe. Naibu Spika: Haya kama Mheshimiwa keshasema wale wote ambao hawakuchangia, nisikilize basi, amesema wale wote ambao hawakuchangia ...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Msikilize mtu kwanza shida yake Mhe. Naibu Spika, mmetupa utaratibu huu mtu hakutaja na nimechangia hansard zipo.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa endelea.

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuendelea hata huyo Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambaye anasema sikumtaja na nilitangulia kusema naomba samahani kama nimemsahau mimi ni binaadamu. Kwa hivyo napenda kumtambua Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Paje.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo sina la kusema isipokuwa ni shukurani kubwa kwa wajumbe ambao wameonyesha ukomavu wao wa uchangiaji. Mheshimiwa mengi yamesemwa na mengi michango yao ni yenye thamani kwa sababu michango yao ni imani yangu kwamba italisaidia taifa hili.

Mengi yamezungumzwa na Mawaziri, Mawaziri mimi leo nilikuwa sitaki niongeze neno kwa sababu nitakaloliongeza mimi nitakuwa nakwenda kinyume wakati Mawaziri wametoa ufafanuzi wa kutosha juu ya mambo yanayohusiana na Kamati. Nawaomba Wajumbe tukubaliane na turidhike na yale ambayo ufafanuzi wake umetolewa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Ni ukweli usiopingika kwamba kamati yetu imefanya kazi nzuri chini ya mashirikiano ya Wizara zilizo chini ya Kamati hii. Kama tulivyoeleza katika ripoti yetu kwamba tumefanya kazi hapa katika mizunguko sita ambayo inaonyesha katika ripoti yetu. Isipokuwa mimi kuna moja ambalo napenda kuliongezea juu ya mchango wa Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Naibu Spika, mchango wake Mheshimiwa nauthamini sana ni mchango wenye maana, lakini nitakata Mjumbe atambue kwamba siku ya tarehe 20/9 tulifanya semina kubwa ya nchi za *SADC* kuhusiana na madawa ya kulevya. Jambo ambalo limeipa sura nzuri Zanzibar ni kuwepo kwa Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Wenzetu wa nchi za *SADC* wameahidi kwamba watakuja

Zanzibar waone jinsi gani sisi tunavyofanya na serikali yetu. Mimi nachukua fursa hii adhimu kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa utaratibu wa kuianzisha hii idara ya udhibiti wa madawa ya kulevya.

Lengo ni nini? Lengo sio kwamba Mkurugenzi au ile taasisi yenyewe ina zuia na ndio maana tukapendekeza kwamba iongezewe meno kwa kupewa sheria itakayosaidia nguvu ya kisheria ile Tume. Tutakaposema kwamba tufute hiyo Tume, kwanza tume yenyewe hivi sasa ilikuwepo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, sasa hivi kwa mujibu wa sheria ni lazima ipatikane Mwenyekiti, Rais hajamteuwa ninavyofikiria mpaka sasa hivi, kama nitakuwa nimekosea naomba *hansard* isichukue hilo.

Lakini kwa sasa hivi ninavyojua kwamba Rais hajakamilisha uteuzi wake, tumsubiri Rais akamishe ndiyo ifutwe. Leo haijamaliza tutafuta nini wakati kitu hakijafuta. Kwa sasa iko chini ya Makamu wa Pili wa Rais. Mimi namuomba sana Mhe. Hassan akubaliane na aridhike kuwepo kwa hii Tume kwa sababu hii tume inatusaidia sisi sote.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa taarifa ndogo tu kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tayari ameshateuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kusimamia Madawa ya Kulevya. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Sawa naomba na mimi *hansard* ichukue kama Makamo wa Pili wa Rais.

Utaratibu

Mhe. Hassan Hamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, kifungu 37 mimi ni Mjumbe halali wa Baraza hili nina haki ya kusema na kusikilizwa.

Mhe. Naibu Spika: Mnajua nyinyi mnapoteza muda kila saa utaratibu, utaratibu, sasa hiyo ndiyo ina maana gani, mnatupotezea muda tu. Mheshimiwa endelea fanya majumuisho.

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa kujali muda mimi sitaki kuongeza kwa niaba ya Tume na kwa kuthamini michango mizuri ambayo imetolewa na Wajumbe na kwa sababu ripoti yetu imeonyesha

upembuzi mwingi napenda kutambua mchango mzuri uliotolea na Mhe. Maudline Cyrus Castico kuhusiana na upatikanaji, kuhusiana na majengo na kutoa kipaumbele na serikali ichukue umuhimu wa kuzuia huo mmong'onyoko.

Kama alivyojibu Mhe. Waziri kwamba suala hili tayari limeshafanyiwa kazi na jambo la mwisho ni maoni ya Mhe. Juma Ali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) aliyetaka undwaji wa Tume ya Uchaguzi mara hii utakaofanyika kwenye sheria izingatie ajenda. Mimi napongeza mawazo hayo na mawazo yote ni mazuri na tutayachukua na tutayawasilisha serikalini. Ni imani yetu kwamba serikali itayachukua na itayafanyia kazi kwa mujibu wa itakavyoona.

Baada ya haya mazuri natamka kwamba naomba kutoa hoja Mhe. Naibu Spika.

Utaratibu

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Naibu Spika, wakati nachangia kuna suala langu nililizungumzia na nikamuomba Mhe. Waziri anipe jibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri ameshamaliza kujibu.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Aaa! no lakini.....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri ameshamaliza kujibu na amesema, Mhe. Zulfa, Mhe. Mwenyekiti kakae. Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea. Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea, naomba tuendelee.

Waheshimiwa Wajumbe sasa nakuhojini wale wote ambao wanakubaliana na majumuisho ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa Wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. Tunaendelea.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawla Bora na Idara Maalum

Mhe. Machano Othman Said: (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa muhtasari wa hotuba ya uwasilishaji wa ripoti ya kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum pamoja na muhtasari huu naomba Mhe. Naibu Spika, ripoti yetu yote yenye kurasa 42 iingie kwenye Hansard ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitumie nafasi hii adhim kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake, kwa kutupa neema ya uhai na uzima katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku kwa hali ya amani na utulivu.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati yetu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, Ripoti ambayo inawasilisha shughuli zetu zote ambazo tumezitekeleza kwa kipindi kilichopita.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar, Toleo la 1984 na Kanuni ya 106(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, Toleo la 2016 na kuainishwa majukumu yake chini ya Jadweli la Kwanza la Kanuni hizo la mwaka 2016.

Mhe. Naibu Spika napenda kuchukua nafasi hii muhimu kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha kamati yetu kufanya kazi zake kwa ufanisi na uzoefu mkubwa. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1.	Mhe. Machano Othman Said	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis	-	Makamo M/kiti
3.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
4.	Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf	-	Mjumbe
5.	Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mohammed Said Mohammed	-	Mjumbe
7.	Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Mjumbe
8.	Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu
9.	Ndg. Ali Alawy Ali	-	Katibu.

Mhe. Naibu Spika, katika utaratibu uliowekwa katika utekelezaji wa kazi za Kamati kwa muda wote uliopita, Kamati yetu ilipanga kufuatilia utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara zifuatazo:-

i. Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

ii. Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita (6) ambapo kwa upande wa Unguja ilitumia wiki nne (4) na Pemba wiki mbili (2). Muda huo ulikuwa mdogo sana kwa namna ya wizara hizi zilivyo na ukubwa wa Idara zake.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, kamati inawapongeza sana na kuwashukuru viongozi wa Wizara hizo wakiongozwa na Mawaziri wao, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Makamishna, Wukurugenzi, Maafisa Wadhamini Pemba na watumishi wao wote kwa ushirikiano wao mkubwa waliotuonesha katika kufanikisha majukumu yetu, licha ya kuwepo kwa changamoto mbali mbali zinazowakabili na kufanyakazi katika mazingira magumu na yenye upungufu wa nyenzo lakini waliweza kutekeleza majukumu yao ya kazi kadri hali ilivyokuwa inaruhusu.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa uniruhusu nieleze kwa ufupi kabisa baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika kazi za Kamati kwa Wizara kama ifuatavyo:-

Wizara ya Nchi Ofisi ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inazo Idara na Taasisi mbali mbali ambazo zinafanya kazi kwa mujibu wa malengo yaliyopangwa chini ya Wizara hii. Hivyo, katika kukamilisha majukumu ya Kamati yetu tulifanikiwa kuzitembelea Idara na Taasisi kadhaa ambazo zimeunda Wizara hii na kujionea shughuli zao mbali mbali ambazo zimekabiliwa na changamoto kubwa kutokana upungufu wa vitendea kazi na udogo wa ukomo wa Bajeti.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaipongeza sana Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Serikali kwa juhudi zake za kuanzisha Mahkama ya watoto Mahonda, ambayo imefunguliwa hivi karibuni na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, hivyo Mahkama hiyo inatarajiwa kupunguza idadi ya kesi za udhalilishaji na ukatili dhidi ya watoto kwani vitendo hivyo vimeshamiri sana katika Mkoa huu wa Kaskazini Unguja. Ni matumaini yetu kuwa uanzishwaji wake utasaidia sana katika uendelezaji wa kesi zote zinazohusu watoto na kurahisisha upatikanaji wa haki za mtoto katika Mahkama zote za watoto ikiwemo Vuga na Chake-Chake kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katika ziara zake imebaini uwepo kwa changamoto kubwa ya vyombo vya usafiri

katika Idara na Taasisi mbali mbali zilizochini ya wizara hii, jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi zao katika utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, changamoto hii inaikabili zaidi Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa, ambapo hadi sasa wana gari moja tu na kutokana na uhaba huo wameona wanunue vespa moja, wakati Tume ya Utumishi Serikalini hawana hata gari moja la kuwasaidia, hivyo huenda katika majukumu yao ya kazi kwa kutumia usafiri wa Daladala jambo ambalo ni kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhamini Pemba inajitahidi sana katika kusimamia na kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha wameenda sambamba na malengo ya wizara na Serikali kwa ujumla. Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya Idara kutoingiziwa fedha za matumizi moja kwa moja isipokua fedha hizo huingizwa katika kurugenzi zao kuu ziliopo Unguja kitu ambacho kinasababisha Ofisi Kuu Pemba kutumia fedha zake kwa ajili ya kuendeleza Idara hizo. Aidha, kutokuwepo kwa baadhi ya Taasisi Pemba ikiwemo ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Tume ya Kurekebisha Sheria, Tume ya Utumishi Serikalini na Ofisi ya Serikali Mtandao *(E-Government)* kunasababisha kuzorota kwa kazi za Taasisi hizo muhimu za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaagiza kuchukuliwa kwa hatua zinazofaa suala la kutoingizwa fedha za matumizi moja kwa moja katika baadhi ya idara zilizopo Pemba na kufanyiwa haraka uwepo wa Taasisi zinazokosekana Kisiwani Pemba ili kuondoa changamoto zinazojitokeza kwa kukosekana ofisi hizo.

Mhe. Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuona kwamba Idara na Taasisi zake zinafanikiwa katika utekelezaji wa majukumu yao na zinaleta ufanisi katika kuleta maendeleo kwa nchi yetu.

Aidha, Kamati imegundua kuwepo kwa changamoto kubwa ya vitendea kazi kwa upande wa Mahkama zote zilizopo Unguja na Pemba jambo ambalo kwa kiasi kikubwa linachangia kurudisha nyuma na kurundikana na kuchelewa kwa uendeshaji wa kesi katika Mahkama zetu. Vile vile, tatizo hili linaonekana kuwa kubwa zaidi katika Taasisi ya *ZAECA, CAG* na Idara ya Nyaraka. Taasisi ambazo zina jukumu zito la kulinda na kusimamia rasilimali za Serikali ili zisipotee kwa watu wabadhirifu na watu wasiokuwa na imani na maendeleo ya Nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inasisitiza tena kwa mara nyengine na kuishauri Serikali kwamba juhudi za makusudi zifanyike za kuwapatiwa vitendea kazi ili

kuhakikisha malengo ya Taasisi hizi yanafikiwa kwa mujibu wa taratibu zilizopangwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hii kwa upande wa Chuo cha Utawala wa Umma, Zanzibar, Kamati inashauri katika bajeti inayokuja Chuo hichi kizingatie mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kuboresha miundombinu ya majengo ili iweze kuwa rafiki kwao. Vile vile kamati inaagiza chuo kuajiri wakalimani ambao watasaidia wanafunzi wenye ulemavu wa uziwi kupata nafasi ya kujifunza kwa uhakika na kwa urahisi zaidi tofauti na ilivyo sasa kutokana na uhaba wa vitendea kazi na wataalamu. Kamati pia inakitaka Chuo hiki kujiimarisha Tawi la Pemba kwani hivi sasa yupo mtumishi mmoja tu wa kudumu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati imesikitishwa sana na maendeleo ya baadhi ya Taasisi zetu ambazo zinatuongoza na kulinda haki za raia wa nchi hii, huku tukiamini kwamba baadhi ya Taasisi hizo ni mihimili mikuu katika kuchunga na kulinda haki za wananchi. Ni dhahiri kuwa mazingira mazuri na salama kwa watendaji wa Taasisi hizo ndio yatakayoleta tija kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuwepo kwa uchakavu na ubovu wa majengo ya Mahkama kwa Unguja na Pemba kunarudisha nyuma sana nguvu na ari ya utendaji katika mazingira yao ya kazi. Kamati ilifanya ziara katika Mahkama ya Mfenesini na Mwanakwerekwe na kuona hali ya majengo yake hayafai kabisa, hayana nafasi, lakini hadi leo bado Mahakama ya Mfenesini wana choo kimoja ambacho wanatumia Mahakimu, Makarani, mahabusu na wananchi wanaokuja katika kufatilia kesi zao; hali hii pia ipo katika Mahkama ya Mwanakwerekwe.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Mahkama ya Wete nayo hairidhishi katika mazingira yake ya kazi kwani jengo lake ni bovu na halina nafasi ya kutosha pamoja na miundombinu mibovu ya maji. Mahkama hii pia inakabiliwa na ukosefu wa vitendea kazi kama vile makabati ya kuhifadhia majalada, ukosefu wa kompyuta ambapo ofisi nzima inayo kompyuta moja tu, lakini hata meza na viti vimechakaa kiasi ambacho havifai kwa matumizi ya Mahkama.

Mhe. Naibu Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa ongezeko kubwa la kesi za ubakaji na udhalilishaji na jamii kutokana na uelewa wa kutosha juu ya kesi hizo, lawama kubwa ya ikiwahusisha Mahkama na Waendesha Mashtaka wa Serikali na Jeshi la Polisi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaagiza kufanyiwa kazi suala zima la kesi za udhalilishaji katika jamii kwani limekua ni changamoto kubwa inayoikabili

jamii yetu na hata kukosekana imani kwa chombo cha Mahkama na jamii. Adha, Kamati inasisitiza kuwepo kwa mashirikiano mazuri wakati wa uendeshaji wa kesi za udhalilishaji kwa Jeshi la Polisi, Ofisi ya DPP na Mahkama kwa kuhakikisha wanasimamia vyema upatikanaji wa ushahidi ambao utawatia hatiani watendaji wa kesi hizi bila kujali ufatiliaji wa suala linalopelekwa Mahakamani. Pia, ni vyema Serikali kuziangalia na kuzifanyia marekebisho sheria ili adhabu ya wabakaji iwe kubwa kuliko ilivyo sasa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, Kamati inaagiza ofisi ya Mufti kuimarisha mashirikiano yake na ofisi ya DPP katika kuangalia kesi za Walimu wa Madrasa ili kuweza kujua na kupata taarifa juu ya kesi hizo. Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti itoe maagizo ya barua kwa Maimamu wote Unguja na Pemba ili watoe elimu ndani ya Miskiti yao kwa lengo la kuisaidia jamii juu ya kuepuka na janga la vitendo vya ngono za jinsia moja na kudhalilisha watoto. Mhe. Naibu Spika, Kamati inaziagiza Idara na Taasisi ambazo hahazijafungua Ofisi zao Kisiwani Pemba zifanye hivyo katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inahisi kuwa pamoja na juhudi za Serikali kusimamia utekelezaji wa majukumu ya watumishi wake, bado kuna changamoto ya wataalamu katika Idara na Taasisi mbali mbali za Serikali kitu ambacho kinaleta ukakasi katika ufanikishaji wa malengo ya maendeleo. Mhe. Naibu Spika, kutokana na changamoto hii Kamati inaishauri wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwasomesha watumishi wake katika ngazi mbali mbali za kielimu pamoja na kuajiri watu ambao ni wazalendo na wenye sifa za kutosha katika maeneo husika.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu imebaini kuwa lipo tatizo la upatikanaji wa ajira pamoja na tatizo sugu na la muda mrefu la wafanyakazi waliofikia umri wa kustaafu kutokufanya hivyo. Kamati inashauri kwamba Serikali iweke wazi Kada ambazo zitaruhusiwa kuongezwa muda wa kazi wafanyakazi wake watakaofikia umri wa kustaafu badala ya kuangalia umaarufu wa mfanyakazi au sehemu anayotokea. Hatua hii itasaidia kutoa ajira kwa vijana wapya ili nao watoe mchango wao katika ujenzi wa maendeleo ya Nchi yao.

WIZARA YA NCHI (OR) TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR:

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaundwa na kusimamiwa ni Idara na Taasisi mbali mbali zilizogawika katika maeneo manne makuu katika kutimiza

majukumu yake pamoja na Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba. Aidha, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuweza kuwapatia fungu la bajeti kwa asilimia kubwa katika Taasisi na Idara zake zote tofauti na miaka ya nyuma. Kamati yetu imebaini kwamba Taasisi zote za wizara hii zimepatiwa bajeti kwa zaidi ya asilimia 95%.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kuleta mfumo mpya wa Ugatuzi wa Madaraka Mikoani ambao utatumika kuendeshea Taasisi hizi. Hivyo, katika kukabiliana na changamoto ambazo zitakuja kuwa ni kikwazo cha majukumu yao, Kamati inaagiza Serikali za Mitaa kuwapa elimu watumishi wake na watendaji wakiwemo masheha, madiwani na wafanyakazi wa kawaida kulingana na mabadiliko ya sheria za mazingira hali ya utekelezaji wa sheria hizo katika mfumo wa Ugatuzi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati imegundua katika baadhi ya Mabaraza ya Miji pamoja na Halmashauri zake kuwepo kwa tatizo la ukusanyaji wa Mapato pamoja na usiamamiaji mbovu uliopo kwa wafanyakazi na wamiliki wa mahoteli. Hali hii imejitokeza kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A na B kwa Unguja na Baraza la Mji Wete na Mkoani kwa Pemba. Kamati inaagiza Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa wanafikia malengo waliyojipangia na wamesimamia vyema ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyake mbali mbali na kuhakikisha hakuna mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, katika uanzishawaji wa mfumo wa Madaraka kwa Wananchi (Ugatuzi) ni vyema Taasisi zitakazo husika na Mfumo huu kupewa elimu ya kutosha juu utoaji wa huduma kwa wananchi badala ya kujikita katika uzalishaji wa mali pekee kama ilivyoeleweka kwa baadhi ya Halmashauri na Mabaraza. Vile vile, Kamati inashauri Serikali za Mitaa kusimamia vyema utoaji wa huduma za kijamii na kuhakikisha kila mmoja zimemfikia na kwa kiwango chenye ubora kutokana na mapato wanayokusanywa kupitia vyanzo vya vya mapato.

Mhe. Naibu Spika, katika ziara ya Baraza la Mji Chake-Chake, Wete na Mkoani, Kamati imeona wamekabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa wataalamu kama vile wahandisi, maafisa mipango na maafisa wa manunuzi na ugavi. Kamati inashuri kuwa Mabaraza haya na yale yenye matatizo sawa na haya kuhakikisha wameajiri wataalamu wa fani mbali mbali ambao wanahitajika ili kusaidia kuleta ufanisi wa majukumu yao.

Mhe. Naibu Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya Masheha ambao uwezo wao wa kazi umepunguwa kutokana na ugonjwa au umri mkubwa, hivyo Kamati yangu inaiagiza wizara kufanya mabadiliko ya haraka kwa Masheha ambao uwezo wao wa kazi umepungua kutokana na ugonjwa, umri mkubwa au kukosa maadili katika utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, Kamati inaona ni vyema kuchukuliwa hatua za haraka kwa Askari Jamii wanaobainika vitendo vyao haviendani na maadili ya uaskari au wanatumia vibaya majukumu waliyopewa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na kusababisha kuitia Serikali doa kwa wananchi na wageni wanaoingia nchini, hususan maeneo ya Mji Mkongwe ambako ni kioo cha nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ilifanya ziara ya kutembelea vikosi vyote vitano (5) vya SMZ kwa upande wa Unguja na Pemba na kujionea shughuli zao mbali mbali za kizalendo na kuleta maendeleo ndani ya nchi yetu.

Aidha, Kamati inapongeza sana juhudi zinazofanywa na wapiganaji wetu wa vikosi hivyo kwa sasa ingawa hali yao ya kazi ni ngumu na nzito wanazozifanya kulinda usalama na kuhakikisha kwamba wanadumisha uwepo wa amani na utulivu katika Nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Sambamba na hayo, Kamati katika ziara yake hiyo imeweza kubaini changamoto mbali mbali zinazorudisha nyuma maendeleo ya Idara hizi kama vile:-

Kuwepo kwa maslahi madogo ya wapiganaji, kuwepo kwa majengo na vitendea kazi ambavyo havikidhi haja ya askari wetu, ukosefu wa sare (*uniform*) za askari pamoja na kuwepo kwa ukosefu wa Hatimiliki za maeneo yao kwa upande wa Kambi za Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Tatizo la ukosefu wa mahanga ya askari vituoni ni changamoto kubwa katika kufanikisha majukumu ya vikosi vyetu kwa unguja na Pemba, kwani vipo baadhi ya vikosi ambavyo havina makaazi ya askari wake na wanalazimika kutumia majengo yao ya ofisi kama mahanga ya kulala kwa muda wa usiku. Hali hii imejitokeza zaidi katika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Mwanakwerekwe, Wete na Uwanja wa Ndege wa Chake-Chake Kisiwani Pemba ni jukumu la Serikali kuwapatia na kutokuwaachia vikosi peke yao.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kutafuta majengo yaliyostahiki ya ofisi na makaazi mazuri, *uniform* za askari wake pamoja na mambo mengine, basi kazi ya kuwapatia vifaa hivi isiwaachie kuwa ya vikosi peke yake bali iwe ni kazi ya Serikali nzima ili badala yake wajiwekee utaratibu maalum wa kuwasaidia ujenzi wa mahanga askari kupitia miradi ya maendeleo kama ilivyo kwa Taasisi nyengine za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuangalia umuhimu wa kuanzisha kiwanda ambacho kitashughulika na utengenezaji wa sare na viatu vya askari wetu ili kuepuka gharama kubwa zinazotumika kwa kuagizia nje ya nchi vifaa hivyo. Mhe. Naibu Spika, aidha, Kamati inashuri Serikali kuandaa Mfuko wa Bima ya Afya kwa wafanyakazi wote wa Idara Maalum katika kuwajengea mazingira mazuri ya utendaji wa kazi zao, kwani baadhi ya askari wa vikosi hivyo hujitolea maisha yao moja kwa moja katika kuokoa maisha ya watu, hivyo nao wafikiriwe kwa kuangaliwa maisha yao wakati watapofikwa na matatizo ya kiafya. Hata hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuanzisha mfuko wa Hifadhi ya jamii kwa upande wa vikosi vya SMZ kwa kuangalia utaratibu unaotumika wa vikosi vya ulinzi na usalama vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili nao wapate kujifariji wakati wanapofikia muda wa kustaafu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaagiza Wizara kufuatilia maeneo yote ya Kambi za Idara Maalum na kusimamia upatikanaji wa Hatimiliki za maeneo husika hususan kwa upande wa vituo vya JKU Pemba kama vile Msaani, Chokocho na Ngezi pamoja na kituo cha KMKM Sengenya kilichopo Mtambwe. Pamoja na kikosi cha Kojani, Tundauwa, na kadhalika. Vile vile, kwa kuwa Serikali imeamua kurudisha tena utaratibu wa kuwapeleka vijana wa kujenga Taifa katika vituo vya JKU, Kamati inaishauri Serikali kuwapatia vifaa na vijana na vijana wa kutosha katika Jeshi la Kujenga Uchumi ili kuweza kuzalisha kwa kiwango kizuri.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya kambi za vikosi vya SMZ vimekosa huduma ya Afya kama vile Chuo cha Mafunzo Kengeja, JKU Chokocho na Chuo cha Mafunzo Tungamaa na kufuatilia huduma katika maeneo mbali mbali jambo ambalo ni kikwazo kwa wapiganaji wetu walioko vituoni. Kamati inaona ipo haja ya kuwa na vituo vya Afya katika kambi zote za Unguja na Pemba ambazo pia, zitatoa huduma kwa wananchi jirani na vituo hivyo. Aidha, Kamati inaitaka Serikali ifanye juhudi zote ili Kambi ya KMKM Sengenya ipatiwe Rada mpya kutokana na kuharibika kwa muda mrefu kwa Rada iliyokuwepo awali.

Mhe. Naibu Spika, tatizo la kutoshirikishwa kwa maafisa wa vikosi vya Pemba katika uandaaji wa Bajeti za Idara zao pamoja na tatizo la kutokuwa na *sub-vote* kwa upande wa vikosi vilivyopo Pemba, imekuwa ni changamoto kubwa katika kufanikisha miradi yao na hivyo kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, Kamati inaiagiza Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhakikisha wanasimamia vikosi vyote vya *zone* ya Pemba kupatiwa voti zao wenyewe na kuachana na mfumo unaofikiria matumizi kwa kutengewa kiasi kidogo cha fedha ambazo hazisaidii chochote katika kutatua matatizo yao pamoja na kuendesha kazi za vikosini. Pia ni vyema kwa maafisa wa vikosi hivyo *zone* ya Pemba washirikishwe wakati wa uwandaaji wa Bajeti ya vikosi vyao.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, katika kutimiza wajibu wa majukumu ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, imetumia vyema Kanuni ya 106(1) ya mwaka 2016 na kutoa ushauri na maelekezo ambayo matumaini yetu ni kuleta ufanisi katika ukamilishaji wa majukumu ya kila siku kwa Serikali, kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa pamoja na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maaalum za SMZ.

Aidha, Kamati inashauri kwamba wakati Kamati inapofanya ziara zake za kikazi basi tunapendelea Mhe. Waziri au Katibu Mkuu ashiriki katika ziara hizo ili kujua na kubaini matatizo yanayokabili Idara na Taasisi zao.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inapenda kuwashukuru sana wewe mwenyewe Naibu Spika, tunamshukuru pia Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi waliochangia kwa njia moja ama nyengine katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya kazi za Kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa ninakushukuru sana tumeipokea ripoti yako.

Waheshimiwa Wajumbe, shughuli ya sasa hivi mchana inasita hapa mpaka jioni. Lakini Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa nataka nikwambieni jambo moja. Wakati ambapo kwanza Mawaziri wanatoa majibu tunakuwa hatuna

utulivu sisi Waheshimiwa Wajumbe tunaokaa nyuma *back benchers*. Hii inasababisha kuanza masuala mazima ya kuanza kuchukua Kanuni na kuanza kuturudisha sisi nyuma. Waheshimiwa Wajumbe mmekuwa na tabia ya kutumia Kanuni ovyo ovyo, kuna wengine wanatembea kutwa na Kanuni mimi nawaona, mradi anasubiri mtu akosee aseme jambo lolote, hatuna muda huo wa kupoteza Waheshimiwa Wajumbe. Tusifanye hii kama *comedian class*. Sisi tunawakilisha wananchi, nakuombeni sana nafahamu kwamba mnazifahamu vizuri Kanuni lakini zitumieni kwa maslahi ya taifa hili sio kwa ajili yenu nyinyi wenyewe nawaomba sana.

Sisi tunaokaa huku juu mnatukera kwa sababu mnazitumia vibaya Kanuni, mtu kutwa nzima anapiga Kanuni mara tano, mara sita. Kwa kweli sivyo na sisi ni watu wazima Waheshimiwa Wajumbe na ni viongozi naomba sana, tupige Kanuni tunaruhusiwa kwa utaratibu lakini tuhakikishe zile hoja ambazo tunataka kuzisimamia tunazijua vizuri. Sio tunakuja hoja wewe mwenyewe unaepiga Kanuni huijui hoja, unasimama tu unaanza kusema Kanuni.

Ninawaomba sana Waheshimiwa, nikwambieni nimekereka sana leo, tunafanya sivyo Waheshimiwa ninawaomba sana tujirekebishe kwenye hilo. Mara nyingi ninakuwa ninapata lawama hapa, mbona unatubana, sipendi kumbana mtu mimi humu. Kazi yangu ni kuhakikisha kila mmoja anapata haki yake.

Baada ya kusema hayo naahirisha kikao hadi saa 11.00 jioni tukijaaliwa.

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, na nikushukuru nami kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwanzo na nimshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wataala* aliyeniwezesha hapa kusimama ikawa si uwezo wangu wala akili zangu neema zake za uhai alizonipa na nikushukuru tena kwa mara ya pili na nianza na mjadala huu.

Mheshimiwa moja kwa moja katika kitabu tulichopewa ndo mara nyingi huwa nasimama hapa kutumia kanuni kama ulizotupa lakini wakati mwengine zinapigwa chenga. Nianze na changamoto zilizoikabili ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mwanasheria Mkuu katika maisha yako siku uliyosema kweli ni moja hii ya leo katika ripoti yako hii, na methali hazikukatazi ukasema ukamuonea haya mke

ndugu huwezi kupata mtoto. Hapa umezungumza la kweli na vyengine vyote Mwanasheria Mkuu unaweza ukaja ukafeli nakunasihi, nakuwasa vingine vyote Mwanasheria Mkuu unaweza ukaja ukafeli ndio mara ya mwanzo kusikia kuzungumza maneno mazima.

Uliposema Kamati imeeleza changamoto nyengine ni kuwepo tatizo katika mikataba ya Serikali katika suala zima la utekelezaji kwani kumekuwa na tabia na Taasisi za Serikali kupitia Serikali kuu kuitaka ofisi ya *AG* ivunje mikataba wakati ambapo mikataba husika imeshaalipa kwa asilimia 90 na pesa kitu ambacho huwa ni hasara kwa Serikali na changamato hiyo husababishwa na usimamizi mbovu wa mikataba hiyo kutoka kwa Mawizarani na Taasisi mbali mbali.

Hiki usipate shida Mwanasheria fungua ukurasa wa 6 kama maneno umeandikia Mhe. Mwenyekiti Machano na hapo nimpongeze sana umakini wake alotumia huyu ndio Machano Othman Saidi Mwakilishi mzoefu, hapa umezungumza ukweli vyengine Mwanasheria ulomrithi viatu vyake aliita kuna Wizara moja akawaambia sitaki kumtaja jina.

Mzigo huu alimwita na Waziri akamwambia mzigo huu tukienda Mahkamani siku zote alikuwa na kesi karibu mia sita sijui mia nne kazipunguza mpaka zikabaki mia tatu mia mbili aka-*survive* nazo. Lkini ukiona haya Mwanasheria Mkuu narudia tena ukimuona haya mke ndugu huwezi kupata mtoto methali hazitukatazi. Watu wa mikataba washapewa baada ya muda wanafuta kienyeji Serikali siku zote utahangaika Mwanasheria Mkuu utakwenda ukasikitika kesi inapigwa chini inafutwa mpaka mtaji utaliwa.

Kuwa makini nakwambia kuna waziri mmoja alimwita akamwambia pindipo baadae hizi kesi utakwenda mwenyewe Mahkamani waziri alimwita mara ya kwanza waziri akakaataa mara ya pili akawaita na wakurugenzi wake na watendaji wake, baadae akafaahamu na kesi zikapungua. Sasa kama hukuziita baadhi ya Taasisi ukakaza macho kweli kweli mzigo utakuangukia wewe kosa la ng'ombe wa mbele anapigwa ng'ombe wa nyuma, wewe ndio macho yetu uwe makini hapa umezungumza la kweli.

Lakini maagizo ya kamati kwa umakini wa Mhe. Mwenyekiti Machano Kamati inashauri Serikali kupitia Taasisi zake kuzingatia kwa kusimamia umakini mkubwa masharti ya mikataba hii, itaisaidia serikali kuokoa fedha nyingi ambazo zinapotea kutokana na kuwepo na usimamizi madhubuti wa mikataba katika Taasisi ya Serikali lakini pia itaisaidia Serikali kuepusha kushtakiwa.

Mwanasheria Mkuu nakunasihi sana haya maneno ni mazima na jua halijatua muda huu, ziite Taasisi zinakutupia mizigo mingi utakuja kuonekana mdhaifu. Mwanasheria hayo mengine mtu ataogopa kukwambia, mimi nakuekea wazi, *otherwise* pesa za kuja kulipa zitakuwa kama kesi ya mchele na M-Thailand yule mpaka leo habari ya meli na mengine tuache kama unayajua mengine. *(Makofi)*

Tuje kwenye changamoto zinazoikabili Mahkama hapa. Mhe. Naibu Spika, Mahkama ndio kimbilio la wanyonge, mnyonge hawezi kumuendea waziri, waziri utakwenda siku sita humpati utampigia simu na wapo mawaziri humu ndani sitaki kuwataja majina yao, utawapigia simu kwa mujibu wa jimbo utafikiri unaenda kuomba msaada wewe Mwakilishi, endeleeni kuzifunga simu kuna siku tutazitaja humu ndani mmoja baada ya mmoja.

Rais kakuchagueni mawaziri ili mje muwasaidie wananchi, mwananchi anafika siku nne hajamuona waziri anatoka shamba nauli ya kwenda na kurudi hapati kumuona Waziri hatuwafanyii haki. Mhe. Rais ni msikivu kwa wananchi wake Mhe. Issa kasema hapa asubuhi mpaka harusini anakwenda usiku. Kweli tumemuona kwenye maziko lakini hizi simu mkazifunga mnawapa shida, sisi tushazowea, lakini umakini uko wapi mawaziri tunakusaidieni nyinyi tukuulizeni masuala tunasaidia Serikali hapa Mheshimiwa utacheka mpaka utaanguka Mhe. Naibu Spika.

Kamati bajeti ya Mahkama hairidhishi hata kidogo na hapa utakuta tunasingizia Mahkama mlimbikiziwa kesi zinakaa wala tusiwalaumu Mahkama hata kidogo ni kesi ya wizara na uingizaji wa bajeti. Mwezi wa Novemba Mahkama nzima ya Unguja inapewa Milioni 12,000,000 ambapo umeme tu milioni 5,000,000 au 6,000,000 Mahkama hiyo itakwenda kweli Vuga, Makunduchi itakwenda, Mfenesini itakwenda, Mwanakwerekwe itakwenda, Mahkama mnafanya kazi na tunaziona. Lakini ndio yale yale makosa ya ng'ombe wa mbele atapigwa ng'ombe wa nyuma.

Mwezi wa Disemba ni mwezi wa kumi na mbili wakapewa milioni 12,000,000 tena Mahkama tutazionea tu kuzilaumu Mhe. Machano Mwenyekiti wa kamati tunazionea tu, pana *stationery*, pana umeme, pana mambo ya *AC* pana mambo chungu nzima milioni 12,000,000 zitakwenda wapi. Lakini huku na huku kelele zikasaidia Januari akapata angalau milioni 80,000,000 Alhamdullilah jambo la kushukuru.

Lakini hii Mahkama kweli tutaendelea kuzilaumu hakuna utendaji bajeti yao hairidhishi halafu tena ishaongezwa mizigo mengine miwili sasa hivi kuna

Mahkama ya Biashara mpaka leo haijafunguliwa. Mahkama ya Biashara mpaka leo haijafunguliwa watafunguaje hawa pesa iko wapi wameongezwa mzigo mwengine na ndio kazi yao siku zote tunapiga kelele waheshimiwa humu mpaka dakika ya mwisho.

Mahkama ya watoto pesa hizi milioni 12,000,000 zitaendesha kweli Mahkama? Waziri mwenye dhamana hili suala liangalie hili ndio kimbilio la wanyonge, waziri mwenye dhamana wizara hii milioni 12,000,000 Januari wanapewa milioni 80,000,000 hebu tuangalie *difference* yake. Tutazilaumu Mahkama mpaka mwisho mizigo tunaiongeza tumeongeza Mahkama ya Watoto, kuna Mahkama ya Biashara mpaka leo haijafunguliwa tusiwalaumu Mahkama wala tusiwatupie kesi majaji hatuwezi kwenda pesa haziridhishi hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti kuna changamoto kuhusu hilo suala la bajeti lakini kamati imeleza kuna kiwanja cha Mwanakwerekwe hiki kiwanja muda mrefu sasa nataka kuuliza yule waziri na hivi viwanja vya serikali atavifuta, hiki kina miaka kumi na tano ishirini atavifuta viwanja wa serikali vitakavyojengwa.

Mhe. baada ya hapo nije katika Ofisi ya Mufti, Ofisi ya Mufti haiheshimiwi sasa hivi Mhe. wacha kwa Kamati ya Baraza vile vile kuwa haiheshimiwi wache amri nyengine Mkuu wa Mkoa haiheshimiwi lakini hatufanyii haki. Ofisi ya Mufti haiheshimiwi nina barua mimi hapa Mhe. Mwenyekiti iliyokwenda kwa Wizara ya Wanawake na Watoto, naomba hata nisizungumze Wanawake na Watoto Wizara sitaki kumtaja nani lakini haiheshimiwi, Ofisi ya Mufti haiheshimiwi. Tutapiga kelele humu ndani mtatuona wabaya, mtatuhukumu mtavyohukumu lakini jaribu kutuheshimu amri ya mufti ishatoka inakwenda Wizara ya Wanawake na Watoto leo hee *Inallihah Waina illahi rajiuun. (Makofi)*

Msiba mkubwa si pahali pake lakini kama Mufti Ofisi yake haiheshimiwi haya twendeni si langu wala si la baba yangu mimi, wala si la mjomba wangu mimi, Mungu ndie atakaye kwenda hukumu haya ni maisha ya kupita njia tu hapa leo tupo kesho hatupo.

Mheshimiwa changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Kuzuia Rushwa alikuwa dhamana Mhe. mmoja waziri hapa ananzisha Mamlaka hii alifika akanitolea ukali ndani humu kipindi cha bajeti. Nikawambia mbuzi anakula majani kutokana na kamba yake, tusianzishe kitengo wakati hatujawa tayari tusiige watu, leo hapa changamoto hizi hapa si maneno yangu ya kitabu hiki miye hata sijatoka nje, kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa bajeti ya ZEKA ambayo inakwaza kutekeleza shughuli zake, hawa hawana gari wanapiga kelele gari

moja waliopewa msaada ndio hiyo hiyo mwaka watatu wanne . Tutaanza kuendelea kupiga mziki wa taifa huu sijui lini. Nilisema hapa tusifukuzie mambo wakati upo tuwe tayari mtoto hazaliwi akaenda mbio siku hiyo hiyo hutambaa, akapata mguu akakamata kiambaza hii tunawapa mzigo ZEKA tutakulaumuni basi.

Maagizo ya Kamati, Kamati inashauri kuangalia suala la bajeti la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ili iweze tengeneza kazi zao, kamati inashauri suala ka usafiri kipau umbele nilisemea miye na *Hansard* zipo miaka minne au mitatu nyuma utamkamata mtu Makunduchi utamuongoza kama mpaka kafika Bungi kwa miguu mlaze kwanza halafu siku ya pili unganisha safari, haya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije Baraza la Manispaa, kwanza nitakuwa sijafanya kazi kama sijamshukuru Mkurugenzi wa Manispaa wa Mjini sijui anaitwa Serenge kitu kama hivi na kama mimekosea nisamehe. Kkama kuna mtu anaongoza ukimpigia simu akapokea moja yule Mkurugenzi alikuwepo sasa hivi, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni na akaiona simu yako kwenye kikao akitoka baadae atakupigia unasemajie haichagui ya nani wala ya nani Serenge kama upo umefanya kazi kwa wajibu wako Mungu atakulipa kwa hili. *(Makofi)*

Lakini nilianza kupiga kelele Baraza lilopita tunakushanya mapato lakini wananchi wanaonewa, soko la samaki soko chafu shilingi 2,000 unashangishwa asubuhi na jioni wengine elfu mbili vibaraza vile tokea ukoloni mpaka leo hakuna liwalo. Wala tusiwalaumu kama wachafu wauza samaki pesa mnachukua tunawakamua kutekeleza hapana nilipiga kelele miaka mitatu minne nyuma tokea Baraza lililopita. Lakini imekuwa kelele mkwezi wa minazi, mkwezi wa minazi akateremka mnazi huimba yule nipe kalamu niandike wau nisije kusahau, humwambia tajiri wake andike kuwa mnazi wa ngapi huo wa sita, lakini twenda hoi hoi nacho kilindo. Kama hapatoshi njia ya kwenda kwa Zakaria vipenu nilisema bati sitini hazifiki thamanini mwaka wa nne hii si dharau kitu gani. Wananchi mnawachangisha pesa, vibanda vishaanguka hivi vipenu bati sitini sabini hazifiki alimuradi tunavuta tu ndio yale niliyosema unaandika lugha za kiarabu unavutia kwako tu kiarabu ukandika hivi. *(Makofi)*.

Hatuwafanyii haki mwaka wa nne mnasikia kitu gani tunawasaidia wananchi na sio msaada ule kama mnawagawia bure watu wanalipa. Lakini jengine nazidi kuowambea tena wale wanouza biashara zao usiku wale hata kwa Mhe. Rais nitakwenda kuwaombea mimi Mungu akinijaalia kama wataendelea kufukuzwa sijawahi kufika kwa Mhe. Rais, lakini kwa wale wanaopanga

bidhaa zao usiku nitakwenda mpaka ka Mhe. Rais sijawahi kutamika hii. Na ninavyomjua Dk. Ali Mohammed Shein kwa umakini wake na huruma zake na anavyowajali wananchi halirudi nyuma nategmea sana hilo.

Tumeshuhudia barabara zikafungwa huko wafanyabiashara wakapewa wale walala hoi na sio kama wamekaa bure pale Mheshimiwa Machano pale anauziwa vitu rahisi kwa bei.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Jaku umebakiza dakika tatu umalizie

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hizi tatu hazinitoshi Mhe. niongezee nyengine mbili za asubuhi, kwa wale nawaombea wabaki, Mhe. Waziri mwenye dhamana hii hawa nawaombea wewe ni mcha Mungu na nafikiri utanisikia na watu wa Tumbatu wasikivu wacha mungu hata kuzikana kwao hawazikani kwa mapauro huzikana kwa mikono hivi mchanga. Kwa hili Mhe. Waziri nakuomba sana wasikilize uwafahamu ni wanyonge wale hawana kibarua chengine.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika changamoto za Mkoa wa Mjini Magharibi Mhe. Machano hapa umefanya kazi sana Mwenyekiti wa Kamati yale yale, Kamati ukurusa wa 23 wajumbe, Kamati imeeleza kuwepo kwa migogoro ya ardhi katika Mkoa huu ambayo ipo migororo baina ya raia na kwa raia na migororo baina ya serikali.

Mhe. Mkuu wa Mkoa hapa umezungumza kweli kweli kama umeiambia kamati nikushukuru sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini jembe, unafanya kazi na Wakuu wa Mikoa mengine tunaomba wajaribu kufata nyayo zako. Hii migogoro inafanywa na nani Kamisheni ya Ardhi au Wizara ya Ardhi ndio inasababisha chanzo chote hiki, kuna ushahidi wa kutosha si mmoja si miwili si mitatu, chanzo hiki kinasabaishwa na mtu mmoja au wawili pale Kamisheni ya Ardhi kusoma kwingi kuna matatizo yake, Kamati imeagiza inashauri Uongozi wa Mkoa kushirikiana na Taasisi kuhusika kwa wawakilishi wamesema migogoro hiyo ya ardhi kusuluhishwa, itasuluhishwa wapi wakati huu. Mtu keshakula hasara pesa chungu nzima unataka kwenda kusuluhisha hapa hiki kitu hakielekei.

Lakini nije katika sijui ndio Wilaya ya Magharibi A na B pana banda Wilaya ya Magharibi A au B sijui mmelijenga nyumba za Mombasa linakera watu lile banda na uchafu na hauzolewi. Lile banda limejengwa bila kibali bila ya chochote lakini ndio mwenye nguvu mpishe. Llile banda linakera watu uchafu umekuwa mwingi kuna vyakula vya watu maghala ya watu pale lile banda

mtafute pahali pengine wenyewe wako tayari kujitolea kwenda kujenga haielekei.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Jaku muda wako umekwisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mheshimiwa namalizia nukta moja tu. Kuna wafanyakazi walioajiriwa wa Manispaa wana miaka kumi mshahara wao thamanini mpaka hii leo.

Mhe. Naibu Spika: Muda wako umekwisha Mheshimiwa, Mhe. Nadir Abdul-Latif baada ya Mhe. Nadir Mhe.Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy: *Assalamu Aleykum, Bismillah Rahman Rahim.* Ahsante sana Mhe. Naibu Spika mimi kwa kuwa Mjumbe wa Kamati hii nitachangia kwa ninavyo fahamu mimi sitopata buku sana kwa sababu dakika kidogo na Wizara mbili. Lakini nitaanza na Wizara ya Katiba na Sheria kwanza nitaenda kwa Mufti Mkuu kwa sababu ndio dini yangu naianza mwanzo.

Mhe. Naibu Spika katika suala la Mufti Zanzibar kwa kweli naweza kusema wananyanyaswa kwasababu dini hasa imewekwa nyuma Zanzibar, dini Mufti Mkuu kwa kweli ukiangalia hata changamoto zake ni maana kwamba hakuna fursa kote inapoweza kufanya kazi zao wafanye kwa uzuri na ndio maana hukwama kwama na mambo hayaendi, ukiangalia Mufti Mkuu changamoto zao walivyoeleza Ofisi ya Mufti bajeti haikidhi haja Ofisi ya Mufti haina *vote* yake wanaiomba *vote* sijui muda gani sasa muda mrefu sana *vote* hawataki kupewa tatizo liko wapi kwamba Mufti Mkuu ofisi yake wasipewe *vote* wakawa nayo wenyewe. Wanaomba hawalazimishi lakini muwafikirie isifike hatua tukaenda tu, hii nchi tunafahamu tunafahamiana wenyewe kwa wenyewe Mufti Ofisi yake ijaliwe kwa sababu katika Zanzibar nzima asilimia 99.9 waislamu itakuwaje Ofisi ya Mufti itupwe, changamoto zote ukiangalia ya Mufti mazishi matupu kwa ufupi ni hatari.

Vile vile Ofisi ya Mufti imeeleza katika changamoto zao mambo waliyoyagundua, wamegundua kwamba lipo tatizo ambalo watu wanafanyiana jinsia moja, mfano, mwanamke kwa mwanamke, mwanamme kwa mwanamme. Suala hili lipo kwa watu wenye uwezo wamefanya upelelezi na usishangae ukakuta humu ndani ya Baraza watu kama hao wamo. Maana yake ukiambiwa watu wana uwezo basi wameshafanya utafiti. Ssimtaji mtu lakini masuala kama haya unaweza ukakuta ndani ya ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi wenye jinsia moja wenye kufanya maovu basi humu wamo

unaweza ukakuta wakichunguzwa. Sasa mambo kama haya ili tutibu basi sisi viongozi tuoneshe mfano, lakini utakuta leo viongozi ndio waharibifu wa mwanzo wanaoharibu mambo halafu tunalaumu huko chini.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimefurahi sana kwamba Ofisi ya Mufti Mkuu imekubali kwamba suala hilo lipo na wafanyaji wa vitu hivi ni wafanyabiashara au watu wenye uwezo, watu maarufu, wanasiasa na wengine wa chini. Hili suala lipo tunaona na lipo dhahiri kabisa na tunawajua wengine.

Mhe. Naibu Spika, pia kamati imeeleza kuharibiwa kwa watoto na walimu. Mhe. Naibu Spika, hili suala limeshakirihisha watoto wanaharibiwa na walimu wa dini kabisa, skuli, walimu wanawaharibu watoto wadogo wakiwemo wanawake na wanaume. Lakini hadi hivi leo kwamba hili suala linachukuliwa vipi kwani mambo yanazidi kuharibika, ukisema uende Zanzibar nzima ufanye utafiti basi watoto katika baadhi ya vyuo sio vyote unaweza ukakuta watoto watatu au wanne wameshaharibiwa. Hili suala lipo wamekubali wameshafanya utafiti.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Idara ya Teknolojia na Mawasiliano ya *E-government*. Mhe. Naibu Spika, *E-government* ni suala zuri litarahisisha mambo, lita-*save* baadhi ya fedha katika serikali kupunguza gharama, lakini ukiangalia nchi yetu wenyewe mambo bado hayajawa katika teknolojia ya hali ya juu. Japokuwa watu wanasema kwamba elimu itakuja kama ilivyoanza simu watu walikuwa hawajui kutumia simu baadae wamejua, lakini suala hili ni zito kwa wananchi kutumia kompyuta kuingia kwenye kuangalia hivi vitu. Kwa hivyo, mimi ningeomba kwanza elimu ya e-*government* itoke kwa wingi, wananchi waelimishwe ili waweze kufahamu uzuri wa *e-government* lakini kwa sasa hivi ni ngumu na tunapokwenda hasa kwenye nchi yetu watu wachache sana wanaoweza kutumia kompyuta ku-*eccess* kwenye masuala ya *internet*.

Mhe. Naibu Spika, vile vile mimi nitakwenda kwenye Tume ya Utumishi wa Mahakama na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia suala lipo watu wanaodhalilishwa wapo, watu wanaobakwa wapo lakini hali ipo tata. Ukiangalia vile vile watu wanaobaka au wanaobakwa utakuta wazee wao ndio wanaokwenda kutaka kufuta ile kesi, mtoto wake keshabakwa basi mzee keshapewa 200,000/= na yule mbakaji basi anathubutu kwenda kufuta kesi polisi. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana wizara, Mahakama na vyombo vyote vya sheria yule mzee atakayekwenda kufuta kesi basi awekwe yeye ndani mwanzo halafu ndio iendelee hiyo kesi inayofuata.

Mhe. Naibu Spika, masuala haya tumeyaona na yako mengi wazee wako tayari kuuza watoto wao kwa kufuta kesi weshabakwa, wameshaendewa kinyume na wako tayari wazee wenyewe kufuta kesi kwa sababu ya fedha au kwa ajili ya kutiwa maneno. Lakini ukiangalia Mhe. Naibu Spika, ningeomba vile vile suala la Mufti tuje tupate kidogo kichwa cha habari yule jamaa aliyemtukana Mtume Muhammad (S.A.W) kipindi cha nyuma alimtukana na kumdhalilisha kiongozi wetu wa dini amefikia wapi na kesi inaenda vipi na imeamuliwa vipi. Maana yake tumeona kimya hatujui nini kinaendelea mpaka sasa kuhusiana na suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye suala jengine Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Naibu Spika, kuna haja ya wao kuleta ushauri au na sisi wenyewe kutunga sheria na baadhi ya sheria kuziweka katika muongozo mzuri. Sheria zipo nzuri lakini nyengine nahisi bado zinataka kurekebishwa katika masuala ya sheria ili nchi izidi kuwa na sheria ngumu na watu wasifanye mambo haya hasa kwenye masuala ya jinai, masuala ya udhalilishaji na masuala hata ya sheria ya watoto kutoka nje usiku, vitu kama hivyo viwekwe kwenye sheria ili sheria iwe ngumu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kwenye suala la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Suala la rushwa Zanzibar bado lipo na ndio maana hatufiki popote. Suala la rushwa lipo na lipo mpaka mawizarani inafika sehemu wanaokwenda huko kufanya mambo yao ya kazi hasa katika *project*, mtu kama hajalishia fedha basi hapewi. Kwenye mawizara wana watu wao wamewaweka maalum hawatoi tenda kwa watu wengine ambao wanaostahiki na wana vigezo vizuri katika kazi zile, wanawafelisha tu kwa sababu hawajafahamiana kuhusu suala la *percent*, kwa sababu hajatoa rushwa au hawaelewani, kila mtu ana mtu wake mkononi.

Mhe. Naibu Spika, mimi suala la rushwa halitomalizika kama watu hawajawa wasafi, hili suala lipo na sehemu nyingi unazokwenda na ndio maana ukakuta hata kwenye masuala ya ardhi kupata mtu *title deed* yake ngumu, kila sehemu alishie, alishie wakati kitu ni halali mpaka kupata *title deed*. Leo ukiuliza unaweza ukakuta asilimia 90 Zanzibar watu hawana *title deed* wala hawana chochote katika ardhi zao na mali zao au nyumba zao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakwenda kwenye vikosi sasa hivi nimeshatoka kwenye Katiba na Sheria. Mhe. Naibu Spika…

Mhe. Naibu Spika: Una dakika tano za mwisho.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, uongozi wa vikosi tumetembea tumeona ni mzuri lakini baadhi ya mambo yanasikitisha kwa vikosi vyenyewe na wafungwa. Tumeona baadhi ya kambi na naweza kuthubutu kusema kwamba wale Polisi wenyewe wa vikosi basi wao wanatiwa adabu zaidi kuliko wafungwa. Hili linachangiwa kwa sababu makaazi wanayokaa ni mabovu, hayaridhishi kuna baadhi ya kambi tumekwenda na vile vyumba vya wafungwa ni vizuri kuliko nyumba wanazokaa Polisi wa vikosi. Mimi niwapongeze sana kwanza kila kambi tuliyokwenda nimekuta Msikiti wamejenga kwa nguvu zao wenyewe, Mwenyezi Mungu awazidishie nguvu na nawa-*support* sana kwa suala lile kuona Msikiti kila kwenye kambi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile vikosi vinajitolea katika mazingira magumu sana, mimi ningemuomba Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ningemuomba sana aende kwa sababu kuna baadhi ya vikosi viliomba hata kumuona Mhe. Rais kwenye ziara yake apite katika maeneo yale pamoja na Mhe. Waziri husika akaone hali halisi mapolisi wa vikosi wana hali ngumu, wana hali tata majengo hayafai, majengo yanavuja. Nyumba zimejaa kunguni magodoro yamegeuka rangi ya dhahabu. Mhe. Naibu Spika, mimi sitoenda sana kwa sababu mambo mengine ni siri ya waziri mwenyewe na watendaji wake lakini ingebidi ningetandika hapa hapa hadharani.

Mhe. Naibu Spika, kitu kingine ambacho ninachoshauri au ninachoomba kwamba kwenye vikosi basi angalau kifunguliwe kiwanda cha kutengeneza *uniform* zao wenyewe, kiwanda hicho hakifiki hata dola milioni moja, bilioni 2 hazifiki. Lakini cha ajabu kwamba kuna vikosi leo mwaka wa 11 *uniform* hizo hizo mbili walizopewa tokea wameingia kazini mpaka leo miaka 11 hawajapewa *uniform* mpya. Sasa hili suala linasikitisha na ni suala sio zuri kwa kweli lazima tuwape *full support* na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kwenye masuala ya *engineering* wapewe elimu ya kutengeneza wenyewe majumba, wapewe vifaa vya kutengeneza, wawe wanatengeneza kwa urahisi na bei nzuri. Pia twende kwenye masuala ya Mkuu wa Mkoa mimi nam-*support* Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini na mtu anapokesea mimi namtandika humu humu lakini anapofanya vizuri namsifia.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Zanzibar alitangaza kwamba Kendwa hajapendezewa ifungwe kutokana na vigezo fulani. Ni kweli Kendwa kumechafuka kunauzwa unga, kila siku mziki kwenye mahoteli wana-*complain* na masuala mengine. Kama *full moon* walioi-*support* humu ndani kila mmoja anaijua, *full moon* inafanyika kwa mwezi mara moja, kama ni kibali cha mwezi

mara moja kifanyike lakini sisemi mimi watajijua wenyewe wanaohusika, mimi sitaki kuingilia masuala ya maklabu. Lakini *he was very right* Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini ni mtu ambaye aliyefanya *study* na kuna mashaka makubwa na kuna haja ya kum-*support* lakini kuna watu wamem-*crush* kwa sababu tu wanapewa *complimentary* ya kuingia Kendwa bure na kupewa chakula bure na vyumba wana-*support* masuala kama hayo. Mimi niko kinyume nao na nam-*support* Mkuu wa Mkoa, Nungwi kumeharibika, Kendwa hakufai masuala ya madawa ya kulevya, wageni wanakerwa na mapapasi, mziki unapigwa kila siku hakuna Jumatatu wala Jumanne wala Ijumaa. Mimi ningeomba siku iwe moja tu tena iruhusiwe na serikali iwe *official* kama ni *full moon* iwe *full moon* mtu anataka ajijengee ndani ya vyumba vyake visisikilikane nje hakuna aliyekuwa hapendi starehe lakini matatizo ndio haya.

Mhe. Naibu Spika, kingine ninachosema kwamba kila mmoja kiongozi ajue mamlaka yake sio, kuna baadhi ya viongozi leo watakuja kuingilia mpaka kazi za Baraza la Wawakilishi huko nje. Tumemuona Makonda kaitwa na Bunge kwenye maadili kwa kulisema Bunge, na sisi tutakuja kumwita Mkuu wa Mkoa humu ndani kwenye maadili au Mkuu wa Wilaya pindipo atakuja kutusimamia sisi kwenye kauli zetu au kutuingilia kwenye kazi zetu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir muda wako umekwisha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Hili ndio tatizo wizara mbili dakika 15 zilikuwa dakika 30 kwa wizara mbili. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Hiyo ndio ahsante yako Mhe. Nadir.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana. Naibu Spika jembe, naunga mkono.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kupata fursa hii nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kufika hapa leo lakini pia nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Kamati yetu hii ya kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, pia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu wao nikiwa sauti yao pia msemaji wao katika hili Baraza letu la kutunga sheria hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme vitu viwili. Jambo la kwanza wakati Mkurugenzi wa *NOKIA* nafikiri anaitwa Bwana Steven wakati *NOKIA* inataka kununuliwa na *Microsoft* nafikiri nyote mnaifahamu aliongea kwa machozi hasa mwisho nam-*quote*.

"We didn't do anything wrong but we just lost". Yaani hatujafanya kosa lolote lakini tulishindwa.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kukizungumza hapa wakati serikali inajipangia mafungu yake kujiendeleza kwa pamoja ili kwa ajili ya maslahi na maendeleo ya wananchi, hakuna maeneo muhimu wa kulisimamia kama eneo la Mahakama hasa wizara hii. Tusije tukajikuta sisi tunafikiria tuko mbele tunakimbia lakini huku kuna maeneo muhimu tumeyaacha hasa wizara hii, na ukisoma ripoti yao ya kamati kuna mambo mengi sana wameongea mapungufu na wametoa mapendekezo yao na mengine hayasemeki. Wengine wameyataja lakini mengine hayasemeki na changamoto zilizokuwepo.

Mimi nitaanza kwa upande wa *E-government* ambayo imekuwa inazungumziwa muda mrefu, lakini niseme bora tungekuja tuelezwe na waziri baade hapa anayehusika maana kukaa na kupiga kelele wakati jambo halipo, tunaambiwa *E-governmen, E-government* lakini hadi leo nafikiri ni Wizara ya Fedha kwenye hicho kitengo chao cha *Integrated Financial Management System* (*IFMS***)** huko ndiko nafikiria ndio wanaotumia, lakini kote hakuna cha *E-government*, baba yake *E-government* wala mwanawe *E-government*. Mimi tangu sijawa mwakilishi nasikia suala hilo, na hilo linaenda sambamba na mambo ya *fiber optic* wala sitoliongelea tena maana yake ishakuwa historia. Mmenisema wee, mmenisema wee na *E-government* ndio vile vile bora tuambiwe hakuna tufunge tujue tunakuwa na ma-*file* yetu kama zamani, tusiimbe wimbo ambao haupo. Kwa hivyo, akija hapa waziri atwambie hili suala la *E-government* likoje tuelewe.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia Ofisi ya *AG* ambayo wanasimamia mikataba mingi ya serikali, mengine hatuijui sisi lakini *AG* na Mhe. Waziri mpo hapa kuna mikataba wengine sisi tutapenda tuione tuifahamu. Nasikia sasa hivi huko nje kuna fununu mkataba wa Bwawani ni mbovu haufai, tunasikia miaka 99 ujenzi haujaanza, mmekuja hapa kwa mbwembwe kabisa mkatwambia mnafunga mikataba lakini makontena yameondoka sasa hivi yamerudishwa pale pale. Hebu twambieni kuna matatizo gani wawekezaji wapo wengi, na wengi wanataka kufanya kazi vizuri na hapa Zanzibar. Jana Mhe. Nadir alisema kitu hapa akawa anamgonga Mhe. Waziri wa Ardhi lakini *message* aliyokuwa anajaribu kuisema wakati mwengine mawaziri mnatoa kauli

kuharibu jina la Rais. Kwa sababu mnasema jambo halipo halafu wananchi tunawajengea matumaini hasa hizi ahadi. Leo Bwawani iko wapi mje mtwambie mikataba mnayofunga na Mwanasheria Mkuu unafahamu lakini *content* hatuzijui.

Sasa hivi jumba limejaa mashetani mle ndani hata kupita usiku huwezi kama hujamezwa, tena mashetani madume, ya kike, wadogo yote yameshakuwa pale sasa hivi. Naamini wale mashetani wa Forodhani wote tulisikia wadogo kwenye la Beit-el-Ajaib wameshahamia pale sasa hivi, ukipita usiku unaona kama mazunguzungu wamekaa wamekaa mle. Kwa hivyo, hili jengo mimi niliwahi kutoa mawazo mengi huko nyuma, lakini mimi kwa kweli sitaki kuyagusa lakini hapa hii mikataba kwa kweli kuna matatizo. Tunaingiza serikali na wananchi hatuelewi kinachoendelea kwa nini tunafika katika hatua hii. Kwa hivyo, hii mikataba mikataba Mwanasheria Mkuu kwa kweli itabidi tukae tuje tuzungumze mimi na wewe, sio kila wakati unatugonga sisi lazima na wewe zipo kasoro zako tuzijue.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Tulipewa zile fomu kujaza lakini unapojaza zile fomu unaambiwa sasa na mke wako mjazie *account* yake. Kuna wengine humu Waheshimiwa Wawakilishi wakina mama wawapelekee zile fomu waume zao wamefurushwa. Mume gani atakayeweza kumpa mke *account* yake aende akamwambie huko Barazani. Sasa zile fomu ziangaliwe tena upya utaratibu gani ziwekwe, leo unanambia mimi nikatoe *account* ya mke wangu, mke wangu akinikatalia mimi ningefanya nini, hataki. Sasa kuna wengine humu wameolewa wake watatu, wake wa nne nambie kwa mfano ukienda kwa Mhe. Ali Khamis Bakar ukamwambia wake zake wote wajaze eeh itakuwa balaa. Kwa hivyo, unawaambiwa waume za watu wajaziwe *account* zao hivi mimi leo unanianika mpaka benki yangu *statement* hebu fateni utaratibu na wabunge wamefanya vipi.

Leo hiyo akiba yangu niliyokuwa nayo mimi benki chote mmeshakijua kwani mngekitaka mngeshindwa kukijua, si muende tu pale *PBZ.* Ukichukua kadi yangu ya Mzanzibar ukienda *PBZ* unajua, lakini leo unakwenda kumkabidhi mtu simjui mbele wala nyuma ananiangalia alah kumbe bwana Simai wewe nilikuwa najua tajiri sana kumbe una milioni mbili tu, kudadeki. Mmetuanika utupu waheshimiwa, mmetudhalilisha kutokana na kujaza zile fomu kuna mambo mengine yalikuwa hayana haja kujua. Hivi leo mtu mtendaji mdogo anaanza kujua fedha alizokuwa nazo kwenye benki Katibu Mkuu Kiongozi ya nini haya yote, si mjue *account* zake mkafatilie kama mtu ana *account* si amekwishajaza mtajua mkimuhitaji hamna haja ya kuchukua *balance* ya benki ni aibu mmetudhalilisha, mmewadhalilisha wanawake, mmewadhalilisha watu

wote hazifai fomu. Kwa kweli mwaka ujao mkija mje hapa na fomu zenye maana na zikafahamika au nitatumia ile kauli aliyotumia mheshimiwa itakuwa hapa hakulaliki naam au sio.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni suala la Idara ya Nyaraka, hii sehemu ni muhimu sana. Mimi namshauri waziri hebu tafuta utaratibu gani wa kwenda kuwasaidia hawa watu, hebu iangalie ile ripoti. Ukiangalia sijui wanahitaji *smorking alarm* vitu vidogo lakini eneo hili ndio la kihistoria, kama mnaweza niliwahi kutoa mawazo hapa lakini serikali mnakuwa wagumu sana kupokea mawazo sijui kwa nini tumewafanya kitu gani. Nilisema hapa tujengeni *Museum* ya kisasa *Modern Museum* sijui kama hamjui maana yake, hizi nyaraka mtazipunguza kule mtazipeleka upande wa pili na mtapata pesa. Leo ukichukua gari ya mheshimiwa aliyekuwa Rais mstaafu Mhe. Salmin Amour Juma mkichukua mkenda kuweka pale kwa mtoto aliyekuwa na miaka 20 anaona ile ni sehemu ya historia.

Sasa kuna mabarua mengine ukitoa barua ya Mhe. Rais Mstaafu Mwenyezi Mungu amrehemu Mzee Jumbe leo ukiweka pale barua yake wengine wataona ile ni sehemu ya historia. Kwa hivyo, punguzeni hizi *document* tengenezeni *Museum* watu watapenda kwenda hata Mhe. Suleiman hapa yeye anapenda mambo kama haya atawapeleka watoto wake siku za Jumamosi au Jumapili kujua historia yetu ya Muungano wetu, Zanzibar yetu watu waelewe lakini mnakuwa wagumu. Sisi sio maadui mawazo yetu hebu yapokeeni.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna suala zima la sheria kwa upande wa Mahakama hasa katika sheria ya usalama barabarani (*Road Trafic Act*). Kweli mshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tulipokuwa tunazungumza akanisaidia hii sheria kuweza kujadiliana. Kwa kweli hapa Zanzibar kila siku kuna watu wanakamatwa barabarani, twii shilingi 1000, twii shilingi 500 ekeni faini ya bei nafuu mtu kafanya kosa analipa mnapata mapato ngoma imeisha. *What is the problem*? Nyinyi mnasema mnataka kuondoa rushwa lakini hii serikali ndio mnafanya wakati mwengine watu watoe rushwa, si Polisi jiwekeeni utaratibu. Leo unamkuta askari mama amepakiwa kwenye vespa baba hajavaa helmenti, mama kavaa helmenti mama kashika mtoto mchanga sasa askari amfanye nini yule, anampeleka mtoto skuli lakini hajavaa *helmet* keshafanya kosa, eeh bwana! nisamehe anamuachia akishatia mkono mfukoni akitoa 2,000, lakini angalau mngekuwa mmeweka faini ya hapo kwa hapo. Ipitieni sheria ya *Road Traffic Act* ya Mwaka 2003 aangalieni mazingira.

Sasa hivi ukienda Dar es Salaam wala huna haja ya kuzungumza na *traffic*, mnawasumbua. iangalieni hii sheria halafu wekeni faini ambayo angalau inalipika sio kutozwa faini mtu hajavaa *helmet* shilingi 50,000 utakuwa wazimu huo tena, mnaweka faini ambazo hazisemeki hasa, wekeni faini mtu kakosea anajua analipa hapo hapo anasema basi kuanzia leo mimi sitafanya hili tena. Duniani kote haya ndio yalivyo sijui hapa mpaka leo Mwanasheria Mkuu kazi yake kutushughulikia sisi tu hebu tutengezee hiyo sheria utuletee. *(Makofi)*

Chengine nimezungumza wakati wa bajeti kuhusu masuala ya *Tourism Court*, Mahakama za Kitalii. Watalii wananyanyaswa, wanapigwa, wanaibiwa wao kazi yao kupokea *tax* za wawekezaji lakini kuwalinda hatuwezi tunaandikwa vibaya kwenye mitandao. Sawa, fungeni macho si tatizo hamna tabu watalii wataendelea kuja lakini iko siku tutazidi kuandikwa vibaya na vizazi vyetu vitakuja kutuhukumu sisi, tutengezeni Mahakama za Watalii mtu akifanya kosa pale pale masaa 24 *evidence* ipo anakamatwa anapelekwa kule anahukumiwa, *24 hours* Mzungu anapoondoka tayari anajua kenda kule haki ameipata, lakini hapa Mzungu akiondoka pale *airport* basi kama hakupigwa kirungu bahati, anaondoka na sura mbaya ya nchi. Watu wanaibiwa kamera, wengine wanashikwa sehemu zao za siri wakitembea baharini kwenye fukwe, unakuta ni vijana wetu. Kumbukeni kila siku nasema mtalii haji hapa kutuharibu sisi, *lack of parental guidance* moja, mtalii anakuja hapa kujifunza sisi kwetu, mtalii ni mgeni.

Mhe. Mzee Ali Hassan Mwinyi alisema, Zanzibar ni njema atakaye na aje, sasa wakija mnaanza kuona wao kama si watu, wanatumia fedha zao, yule kila kichwa sisi tunasema kule nje kwenye biashara hii tuliyokuwa tukifanya kazi miaka mingi, tunasema kila ile ni kichwa tunahesabu ni pesa. Akitembea tunamuuza tunapata *commission*, hawa wote kwenye mitaa mpaka na mahoteli. Sisi tuwathamini katika mambo yao muhimu wanayosema miaka yote tuwasikilizeni. Mahakama kwa ajili ya kesi za utalii zianzishwe.

Pia nije suala la bodaboda. Bodaboda zimekuwa nyingi sana sasa hivi. Mhe. Waziri mimi nashauri suala la bodaboda wanapita Zanzibar tuna *two wheels* vespa miaka nenda na *ciao*, lakini sasa hivi bodaboda anapita Serena hasa ile *no entry* na baiskeli, anapita huyo mpaka Tumekuja kwenye kona, lakini bodaboda huyo anavuka anachomeka tu. Keshokutwa kesi zitaanza kwenda Wizara ya Afya Mhe. Jaku Hashim Ayoub ataanza kumshika Mhe. Waziri wa Afya watu waanze kukatwa miguu kuwapeleka Moi hakuna, maana yake utaanza kukatwa miguu kila siku, mtu wa bodaboda ukienda Muhimbili anaachwa hivi hivi kwa sababu kutokana na mapungufu yao wanayoyafanya. *(Makofi)*

Kwa hivyo, bodaboda ziangaliwe jinsi ya usalama wa barabarani kwa kupitia Mahakama na ikiwezekana kila muendeshaji wa bodaboda apigwe picha awekwe kwenye mtandao bodaboda huyu hapa ili akifanya hata uhalifu wowote tunamjua, lakini twende kwa utaratibu huo. Leo bodaboda kila pahala hata humjui huyu mtu ni bodaboda kweli.

Juzi katika Tamasha la Busara kuna mtu wa bodaboda kamramba Mzungu fedha, kamchukua kampeleka akamuibia kaondoka hajulikani nani. Kwa hivyo, hawa bodaboda wapigwe picha, picha zao ukishachukua unaziweka katika mtandao hata mtu akishajua nambari yake anajua huyu aliyenichukua nambari yake ni hii ana namba moja tu au mbili, tatu kitambulisho chake hiki hapa unamjua basi, tena akifanya uhalifu tutamjua nani. Lakini leo mtu anaendesha anafanya anavyotaka tena mzigo huu halafu tunapeleka Mahakamani tunaaza kuwalaumu Mahakama na Polisi, lakini utaratibu haujafanywa.

Ukienda katika ripoti kuhusu *DPP* Pemba kesi zilizokuweko Pemba za masuala haya ya chini ya umri wa miaka 18, watoto wanaharibiwa, watoto wameingizwa mimba wajawazito, nini kifanyike. Ofisi ya *DPP* haina uwezo. Lakini katika eneo moja mimi kwa kweli ningeomba hasa wawakilishi wenzangu kutoka Pemba huko Pemba hata suala la familia, watoto kweli wanazaliwa wengi lakini wanazaliwa wengi sana sio wengi ni wengi sana. Watu wanaoa wake wengi lakini *family planning* haipo, Serikali isiache kuwasemea na kuwaelimisha. Mtu ana miaka 35 ana watoto tisa sasa huku inakuwa ni balaa mambo yatayotokezea ni mengi, ingekuwa angalau tunazaa kwa mpango ingekuwa huu mzigo tunapunguza. Kwa hivyo, serikali iendelee kutoa elimu juu ya suala la *family planning* haiwezekani kila mmoja ana watoto kumi una miaka 40 kwa kweli ni hatari.

Sasa katika haya unapoangalia watoto wanaanza kulelewa na jamii mambo yanaharibika katika skuli, mtoto anataka simu, anataka buku, anataka begi, miaka 15 tayari keshatiwa mimba, ukimuulia katiwa na nani mtu wa miaka 50. Hivi mtu ana miaka 50 anamtumia mtoto wa miaka 15 na bado serikali hii imekaa kimya mtu anatembea njiani, kwa nini, Ofisi ya *DPP* haina pesa ni jambo la aibu sana kwetu. Kwa hivyo, tuende tukaangalie huko kweli tufanyeni kazi.

Rais ameteuwa hivi karibuni mshauri wake kwa upande wa Pemba, mawaziri waende Pemba wapange *plan* na mshauri waende kila wilaya wafanye mambo kwa mpango washughulikie wilaya moja mpaka waimalize watoe majina. Najua kuna ugumu kwa masuala ya siasa, lakini wakijipanga wataweza. Lakini leo akienda mtu yeyote Pemba anataka kufanya kazi hiyo wanaanza kupinga aa

hatutaki sisi kwa sababu kiongozi mmoja yeye kama fulani hataki, haiwezekani wananchi wakaathirika. Mimi nakupenda sana Pemba, Wapemba nawapenda kama ndugu zangu sisi ni Wazanzibari, kwa hivyo tusichoke siasa haziwezi zikatugawa sisi watu wakaathirika kiasi hicho, twendeni tukawaambie mzae kwa mpango sio watoto wanawazaa ili kwa sababu twende wanaongezeka kwa sababu ya siasa haiwezekani. Leo watoto wanalelewa katika jamii na hizi kesi zitaendelea mpaka lini halishi hili.

Kwa kumalizia nashauri pia Ofisi za Mikoa Kaskazini na Kusini. Mhe. Naibu Spika, nilinde watu wanazungumza sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe minong'ono imezidi naomba tumsikilize tumpe raha Mheshimiwa mchangiaji.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika ahsante. Mimi wakati ilipozama Meli ya *Spice Islander* nimekwenda Pemba kuwatafuta wale ambao wameathirika waume zao wamefariki, nilimkuta mama mmoja kwenye kibanda mpaka leo nakumbuka yale machozi ana miaka 32 ana watoto 7 halafu mjamzito, nikamuomba tukusaidie kitu gani? Akasema nataka ng'ombe wa maziwa, tukampelekea lakini sijui kama yule ng'ombe atamsaidia. Lakini pia tatizo hilo haliko Pemba tu hata hapa Unguja wapo wengine, huku mikoa ya mjini pia sasa hivi tunaongezeka, hapa watu tunazaliana wengi tunalaumu serikali lakini kote ni tatizo. Kusini kidogo angalau Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Simai Mohammed Said: Dakika mbili namalizia Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Nakupa dakika moja tu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante. Kwa kumalizia nashauri upande wa vikosi. Mhe. Waziri kwenye Vikosi na Tawala za Mikoa suala la *assembling clans* inawezekana mkajenga kwa ushirikiano pamoja na Wachina na ubia kuangalia ni mfumo gani endelevu mnaweza kuupanga kwa pamoja, lakini Mhe. Waziri nitakwenda kuzungumza na yeye *in personal*.

Pia kwenye Mikoa ya Kaskazini na Kusini kwenye masuala ya utalii, nashauri waunde kamati za kizalendo ili kujenga umoja na kuwasikiliza wawekezaji ni njia gani au mfumo gani unaweza kufanya kazi kwa pamoja.

La kumalizia la mwisho soko letu la Kaebona, *roundabout* ya Unguja Ukuu. Namshauri Mhe. Waziri wazo tayari Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amelipokea nimewahi kuliuliza katika *caucus* ya Chama cha Mapinduzi Rais amelipokea, sasa hivi *roundabout* inajengwa, Mkuu wetu wa Wilaya Mhe. Mashavu Said Sukwa anafahamu, naomba sana soko la Kaebona itakuwa tunasogeza huduma kwa watu wa Mkoa wa Kusini na itakuwa ni zawadi pekee, lakini sio soko la kabati soko la kisasa, tutaunganisha watu wa Unguja Ukuu, Kitogani, Chwaka na barabara mpya inayokuja.

Mhe. Naibu Spika, Muda wako umekwisha.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo maelezo yangu machache naunga mkono hoja, naipongeza kamati na nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kila mmoja wetu hapa naona anataka kuchangia, mpaka sasa hivi nina majina kama 27 na leo tumekusudia tunataka tumalizane na ripoti ya kamati hii. Kwa hivyo, kuna wengine baadae nitawataja lakini wengine itabidi walete michango yao kwa maandishi. Sijui mmenielewa? Ninaendelea kupata lakini nawaambia wale wa mwisho mwisho ambao wanaleta karatasi kwa ajili ya kuchangia bora wajitayarishe kwa maandishi zaidi kuliko kuchangia kwa maneno. Tunaendelea Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuipata nafasi hii kuchangia wizara hizi mbili Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wa wizara hizi pamoja na manaibu wao na watendaji wote wa wizara hii, hususan tunaangalia kwamba sheria ndio inayotuongoza katika nchi hii, lakini na ulinzi ndio unaotupa usingizi katika nchi hii. Kwa hivyo, nazipongeza wizara zote mbili kwa kazi nzuri wanazozifanya mpaka tukafika kusimama hapa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitapongeza kazi nzuri wanazofanya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya halikadhalika vikosi vyetu vya SMZ pamoja na Mahakama zetu kwa kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kutokana na taratibu ili tufikie lengo ambalo linatakiwa.

Mhe. Naibu Spika, natoa pongezi za dhati kwa Mkoa wangu wa Mjini Magharib kwa kuweza kuzaa Manispaa tatu, kuanzia Manispaa moja na kuwa

tatu Magharibi 'A' na 'B'. Kwa hivyo, niseme tu kwamba suala hili ni zuri na naipongeza wizara kwa kulisimamia hadi leo madiwani wetu wameapishwa na mamea tayari wanafanya kazi zao ipasavyo. Lakini Mheshimiwa nina ushauri kwa hapa, kwa kuwa Mkoa wa Mjini Magharibi una idadi kubwa sana ya wakaazi lakini katika wakaazi hao wilaya mbili za Magharibi 'A' na 'B' ndio zina watu wengi kuliko Wilaya ya Mjini, hivyo, natoa ombi kupitia kwa Mhe. Waziri anapogawa mipaka au unapogawa sehemu moja zikatolewa nyengine tatu mpya panakuwa na matatizo, naiomba wizara kupitia Manispaa zake iangalie mgao wa magari ya kuzoa taka katika Manispaa zetu mbili mpya.

Mhe. Naibu Spika, pia sio vibaya kuangalia uwezekano wa kuwasaidia kwa mambo mengine. Kwa sababu Manispaa zetu mbili hizi "A" na "B" bado mpya zina shida kubwa sana, zina matatizo makubwa kiuwezo. Sasa namuomba Mhe. Waziri atumie busara zake wakigaiwa gari moja moja au mbili mbili atajua yeye lakini pia kugaiwa na makontena ya kutupia taka katika sehemu zetu. Mwenyezi Mungu atuepushie kinapotokea kipindupindu maeneo yanayoathirika sana ni wilaya zetu mbili hizi Magharibi 'A' na 'B' huwa ndio kichocheo cha matatizo ambayo yanatukuta kutokana na uchafu uliokithiri katika maeneo yetu.

Jengine ninaloliomba tuna matatizo katika maeneo yetu, mimi nasemea jimbo langu la Kijitoupele. Bahati nzuri siku za jua tunaishi vizuri bila ya matatizo lakini ikianza mvua tuna shida kuanza kufikiria je, tutaamka vipi mvua hizo zinazoendelea na athari zake huonekana. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa tuna mitaro miwili mikubwa ya maji Daraja la Meli Nne Uzi na Daraja la Meli Nne kwa Shunda Mwenyekiti wetu wa Wilaya ya Magharibi kichama Dimani namuomba sana Mhe. Waziri tutembelee maeneo haya, yeye na watendaji wake ajue vipi tutawanusuru wananchi wetu hasa siku za mvua. Kwa sababu nikisema mimi Mwakilishi na Mbunge tuchangie hata shilingi milioni 40 hatuujengi mtaro ule, lakini mtaro ule uangaliwe na wataalamu wanaohusika je, tutafanya nini pindi ikija mvua na maji haya yaelekezwe wapi kwa usalama wa wananchi wetu na walioko mbele ya huko yanakoelekea maji.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine wilaya zetu mbili hizi za Magharibi 'A' na 'B' nasemea Wilaya ya Magharibi 'B' sasa hivi nimpongeze Mhe. Waziri baada ya kukaa kuwa hatuna ofisi tumepata ofisi pale Mwanakwerekwe. Lakini nimuombe sana kutokana na idadi ya watu kama nilivyosema mwanzo na msongamano mkubwa wa wananchi wilaya yetu bado ofisi haitoshi, kama kuna mpango au ikiwa kama kwa muda sina maneno, lakini kama ndio tumefika pa kudumu tufikiriwe tena pale pahala pagumu kiutendaji wa kazi. Kwa sababu kama patafungwa safari pale kuna magari 10 au 20 hayakai hivyo tubadilike.

Nimuombe sana Mhe. Waziri hili aliangalie kwa maslahi ya wilaya yetu hii ya Magharibi 'B'.

Jengine kuna matatizo ambayo yanajitokeza katika maeneo mengine. Hivi sasa maji ni kero kubwa katika manispaa zetu zote mbili, Wilaya ya Magharibi 'A' nimesema changa na 'B' ni changa, ili kuwa Manispaa lazima tupate kweli huduma ambazo zinastahiki kwa sababu hapa utajua kweli manispaa ile imetimia kiwango chake. Mheshimiwa tuna shida kubwa sana ya maji, hivyo kupitia Wakuu wa Wilaya na Manispaa zetu tufanye ziaara za kutembelea katika maeneo yetu ili tujue wapi maji yanapatikana na wapi hayapatikani. Hii iende sambamba na kuwa Manispaa jina zuri na ni eneo kubwa lakini huduma zake kidogo zina matatizo hazipatikani.

Mhe. Naibu Spika, jengine niseme tu kwamba Mhe. Waziri katika jitihada zake alizojitahidi mimi nampongeza sana kwenye vikosi. Mheshimiwa mimi narudia tena, napenda sana kujisifu na nitajisifu mpaka nitakufa. Mimi nilikuwa mwanajeshi faida ya uaskari na ugumu wake naujua, askari anataka kulelewa kama mtoto mdogo, askari anatakiwa kupewa stahiki zake kama mtoto mdogo. Kwa mfano, ikiwa leo tumeamua vikosini kutolewe mchi wa sabuni au kijembe cha kunyolea ndevu basi mmoja akikosa yaani ule utoto ulioko ndani kama maumbile basi atalalamika mimi kiwembe changu sikupata, kiwembe tu. Kwa hivyo, ujue askari anataka kulelewa ilivyo.

Kwa hivyo nampongeza Mhe. Waziri kwa sasa hivi jitihada nimeiona kwa sababu lazima uangalie kweli, magari yapo mazuri wamejitahidi na kazi zao lakini pia hata manung'uniko ya hapa na pale naona yamepungua, sijui ndani kabisa sijaingia lakini yamepungua vijana wanakwenda kazini wanaona raha, pia wanapokwenda kazini wanakwenda na magari wanarudi na magari. Lakini pia naomba kama kuna stahiki zao wapewe, nimetanguliza kusema madogo kabisa mchi wa sabuni ama kijembe cha kunyolea ndevu sasa kuna mengine makubwa siku nyengine yapo yasije kubanwa wapewe vijana wetu hawa wafanye kazi zao vizuri ndio ambao tunawategemea katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa mahakama zetu mimi nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake na mahakimu wetu, majaji wetu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Lakini niseme tu Mheshimiwa wakati umefika sasa hivi wa kuongeza bidii katika utoaji wa hukumu.

Mhe. Naibu Spika, kesi za udhalilishaji zimezidi na kilio kizima katika nchi yetu udhalilishaji wa watoto wetu, watoto wanabakwa, wanaibiwa, wanatoroshwa makwao hatujui wanapelekwa wapi. Kwa hivyo, niseme tu kesi

hizi ziwaandame watu na naomba kusiwe na urasimu mkubwa sana. Kwa sababu mfano, kama imepelekwa kesi hii huu unga wa muhogo utajulikana unga wa muhogo mfano huo, kama hii sukari itajulikana sukari na lile tendo ovu linalofanyika lisichukue muda likafichwa, watoto wetu wanazidi kuharibika katika nchi yetu au wanaharibiwa na bado tuko kimya.

Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein alisema namsikiliza sana mimi katika hotuba zake za asubuhi, lazima nimsikilize, anasema umefikia wakati tumechoka. Kwa hivyo, kama tumechoka tushirikiane jamani tufanyeni kazi. Mimi niwaombe wenzetu wa mahakama wote nawajali sana, nawapenda, wafanye kazi zao kwa uangalifu na uadilifu mkubwa sana kusiwe na mzunguuko wa hapa na pale. Lakini na wananchi nao wakubali kujitolea kusema tu kwamba ushahidi huu mimi nauthibitisha kweli hili tendo limefanyika. Kwa sababu bila ya hivyo mahakimu wetu na majaji watapata shida.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika tano.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mheshimiwa. Hili nalisema kwa uchungu kabisa na nimesema ni tokeo ambalo linakera katika nchi yetu ya Zanzibar. Kila siku ya Mwenyezi Mungu ukiamka kama leo hukusikia kabakwa mtoto sehemu fulani ushukuru Mwenyezi Mungu, lakini hakuna siku hata tatu kupita lisitokee tatizo hilo. Narudia tena yuko mjumbe mwenzangu alizungumza hapa sitaki kumuiga yeye lakini nasema haya niliyokuwanayo katika moyo wangu. Vyuo vya Madrasa walimu wengine wamekuwa wahuni wengine, sio wote wengi wamekuwa wahuni. Kwa sababu watoto wanawachukua kwenye madufu wanawarudisha saa saba za usiku au nane wanawaambia mtabakia chuoni hapa hamrudi mpaka kesho tunakulindeni, hawa wanawaharibu watoto wetu, ushahidi Mheshimiwa upo kwa baadhi ya vyuo.

Jengine ninaloliomba hizi madrasa zetu kupitia Ofisi ya Mufti Mkuu tujaribu kuzisajili rasmi na walimu pia wasajiliwe atajulikana huyu kweli, huyu si kweli. Kwa sababu vyenginevyo vyote tutakuwa hatupati faida. Naiomba serikali kwa hili. Madrasa ni sehemu ya dini lakini ina kitengo chake ambacho kinasimamia Ofisi ya Mufti, walimu wote wasajiliwe rasmi wajuilikane na nyendo zao zijulikane ili kunusuru vijana wetu wasipotee wake kwa waume.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo kwa heshima kabisa, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele, naziunga mkono wizara hizi mbili, nampongeza Mwenyekiti wa kamati pamoja na wajumbe wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya wakaweza kutuletea ripoti hii

ambayo leo tumekaa hapa tunaisoma na tunaichangia kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu. Nashukuru Mhe. Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nashukuru. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Abdalla Ali Kombo, baadae atafuata Mhe. Zulfa Mmaka Omar, halafu atafuata Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa, na ajitayarishe Mhe. Khadija Omar Kibano.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mmoja katika kuchangia. Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa na mambo mawili, wizara moja swali moja na wizara nyengine swali moja.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu cha Rais cha hotuba yake ya Januari mwaka huu, alitusifu kwamba kulikuwa na maswali 910 yaliulizwa katika Baraza letu, 254 ya msingi na yaliyobakia yalikuwa ni ya nyongeza. Nashukuru sana kwamba tunafahamika tunachokifanya.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri niliwahi kusoma mawasiliano, kwenye ujumbe wowote kunakuwa na mtu anayeitwa *sender*, anachukua ujumbe unakwenda kwa *receiver*, na halafu inabidi kuwe na *feedback*. Sasa tuliuliza maswali yamejibiwa na kama Mhe. Rais alivyozungumza kwamba kulikuwa na buti na zilikuwepo. Lakini sasa hakuna jibu mpaka sasa hivi ya maswali mengine.

Kwa mfano, kwenye Wizara ya Katiba na Sheria kulikuwa kuna suala la mambo ya nyaraka, ilizungumzwa sana katika ripoti, kwamba tuna matatizo tuna hivi na hivi. Tunayakubali na kweli yapo, lakini na yale ambayo tuliyauliza na yakazungumzwa mpaka kwenye sherehe, hakuna majibu hadi leo. Sasa kwenye mawasiliano hii inaitwa ziro.

Kwa hivyo, ningeomba waziri anayehusika akija hapa basi atufahamishe, yale mambo ya nyaraka yamekwendaje. Mhe. Naibu Spika, hii ni nchi, wananchi sasa hivi wamekaa kitako wanatutizama sisi na mara nyingi wanatuambia aah! nyinyi mnakwenda tu, mbona mnachojibiwa baadae hakionekani, na hakionekani kweli. Kuna tume hapa ilipendekezwa tuleteeni majibu hawa wanaofanya hivi wako wapi wakamatwe watiwe adabu, mpaka leo hakuna kitu.

Mhe. Naibu Spika, hivi juzi tulijaza fomu za maadili hapa tukapewa sisi viongozi wakubwa, mwisho wakenda kupewa na masheha. Sheha unampa sawa sio vibaya yuko kwenye serikali, lakini watu wakupewa fomu za maadili wakajaza na wakaonekana hawa wanaofanya vitendo hivi, na huu ndio utawala

bora. Wizara hii inaitwa Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hapa utawala bora uko wapi mwaka wa ngapi huu hakuna ukweli.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba ili kuwe na utawala bora na ili kuonesha kwamba maadili tunayafuata, basi tupeni hizi ripoti aliyekosea, aliyeharibu achukuliwe hatua ndio serikali. Tuna serikali ya wenzetu hapo Bara, nadhani tunaona, tunasoma kinachofanyika *otherwise* namna hii hatwendi. Kwa hivyo, mimi namuomba anayehusika atuletee majibu ndio utawala bora na ndio maana ya wizara hii, nani kachukua, nani kafanya. Nadhani tukipoteza kondoo mmoja mpaka watatu katika shamba letu hili sio tatizo. Bora tubakie na kondoo ambao ni watiifu kama wanavyoitwa. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi naomba anayekuja atupe majibu ni nani kakamatwa, ziko wapi, niliambiwa diplomasia, diplomasia yuko wapi wa kutuibia vitu vyetu. Kwa hivyo, mimi langu ndio hilo.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye wizara ya tamisemi. Ninachofahamu mimi sasa hivi serikali imesitisha mambo ya biashara, biashara sasa hivi ni *private business*. Lakini kuna kitu kidogo kinanishangaza kwenye vikosi vyetu hivi. Sasa hivi vikosi vyetu, baadhi sio vyote vinafanya biashara kitu ambacho kinanitisha, mpaka Makao Makuu ya JKU imezungukwa na maduka pembeni mule.

Mhe. Naibu Spika, mimi sio askari ingawaje kila Mtanzania ni askari, lakini sitegemei kama kutakuwa na usalama. Unayempa duka humjui ni nani na anatoka wapi, na tusije tukashangaa sasa hivi tuna vita vya unga, wala sio wa muhogo, unga wa hatari. Tusije tukashangaa tukaambiwa kwenye maduka hayo kunauzwa unga tukakataa ni hatari Mhe. Naibu Spika. Kama haya maduka yanafahamika ya Serikali basi mimi ningeomba nipate Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu tunapata nini, kama hizi pesa zinakwenda kwenye serikali.

Mhe. Naibu Spika, nazungumza haya kwa sababu kuna maduka pembeni, lakini kuna vijana wetu, tulikwenda kwenye kamati, askari wetu wanalala pamoja wanawake na wanaume tumewaona, askari wetu hawana vifaa vyovyote, askari wetu wanachangia pesa jioni wale, lakini huku kuna maduka haya sijui kama ni ya serikali au ni ya watu binafsi au sijui kama kweli ni ya askari, wanakula utamu tu wao, maana yake ukisema uroda siku hizi matusi lakini kuna vijana wanateketea. Kwa hivyo, mimi ningeomba hii ripoti ya pesa zipatikane na je, serikali inafanya biashara hii ama hii ni idara maalum kama inavyoitwa iwe na maduka maalum.

Jengine Mhe. Naibu Spika, mambo haya yanawafanya askari wetu kujisahau, mfanyakazi au askari anatoka dukani au popote ambapo sio pakawaida, anakuja kwenye mlango mkuu wa makao makuu ya JKU au mlango wa askari, kavaa kanga katia rangi humu hana *uniform* keshazowea uraia, keshazowea dukani huyu. Wewe unakwenda anakuuliza wewe nani, mimi fulani, shida yako nini, nataka kuonana na kiongozi fulani au mtu fulani, aah! niambie shida yako. Kama hutaki kuniambia shida yako basi huwendi kakae kule au nenda zako, wameshazowea uraia.

Mhe. Naibu Spika, hayo ninayozungumza sio kama namzungumza mtu, yamenikuta mimi. Unakaa wapi Mwanakwerekwe, niambie shida yako au humu ndani huingii, na kweli sikuingia nikarudi zangu. Lakini ni kwamba wameshazowea uraia sasa watu hawa, anatoka dukani anakuja kukaa Makao Makuu ya mlango wa jeshi. Kwa hivyo, naomba mambo mengine tuyarekebishe, tufuate utaratibu nadhani huu ndio utawala bora na ndio maadili huna haja ya kujaza fomu, haya haya yanatutosha.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, nasisitiza tena ripoti ya nyaraka tupewa ili sisi wenyewe humu ndani tuwe kiyoo cha utawala bora, hatuna haja ya kufichana. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe. Mhe. Zulfa Mmaka Omar, halafu Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa ajitayarishe, na Mhe. Khadija Omar Kibano.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa leo. Mhe. Naibu Spika, nataka nianze kuchangia katika mahakama. Hiki ni chombo kizito sana cha mahakama. Nianze kumpongeza Mhe. Rais kwa kutuanzishia mahakama ya watoto. Naamini kwamba Mhe. Rais alijua kwamba lile suala lina umuhimu wake mzito na sisi tumekubali tunampongeza na tunamuahidi kwamba tuko pamoja na yeye, ili kuzifanya mahakama zile ziwe zinasonga mbele sio kufungwa.

Mhe. Naibu Spika, pia naiomba serikali kwa sehemu ya mahakama ianzishe mahakama maalum inayosimamia masuala ya udhalilishaji wa kijinsia ambako huko ndio tutakwenda kwenye mambo ya ubakaji. Mhe. Naibu Spika, suala la udhalilishaji sasa hivi ni kubwa tena sana, wazazi wengi tunapoteza nguvu katika miili yetu kwa sababu ya masuala haya. Lakini tunaona Mhe. Naibu Spika, masuala haya yanapofika mahakamani yanasukumwa huku na huku bila ya kupata hukumu kwa muda mzuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano kama sasa hivi katika Mkoa wa Kusini Pemba, juzi tu nilisikia kuna jibaba moja lililoshinda limekwenda kumkamata mtoto wa *nursery one* na kumbaka. Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana. Hii mahakama mimi naamini kwamba ikikaa hasa chini na kujua kwamba hii mibaba mikorofi. Kwanza Mhe. Naibu Spika, haina haja hii mibaba kutafutiwa ushahidi, kwa sababu jitu ushalikuta kwamba limefanya kesi kama hii, tunalisubiria nini Mhe. Naibu Spika. Hii mibaba itupwe tu huko jela ioze, ikiwekwa huku mitaani itafundisha na wenzake. Lakini mimi naamini kwamba mibaba hii mibakaji au mibaba hii midhalilishaji, ikikamatwa ikienda mahakamani na ikikutikana kwamba ushahidi upo pale pale ikitolewa kesi na mijitu mingine nayo itaogopa Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunaomba sana suala la udhalilishaji liwekewe mahakama yake. Mhe. Naibu Spika, suala hili litolewe *DPP*, kwa sababu *DPP* wanaonekana kwamba wako *busy*, wana kesi nyingi na ikiwezekana Mhe. Naibu Spika, suala hili liwekewe kitengo chake maalum. Pengine kidogo hii mibaba mikorofi itapungua na itaogopa hii minyangumi, lakini bila ya hivyo suala la udhalilishaji Zanzibar itakuwa bado hatujaliweza na litaendelea kutuumiza akili zetu. Kwa hivyo, niiombe sana serikali suala hili nalo mlifikirie.

Pia tukienda kwenye hukumu hizi Mhe. Naibu Spika, hukumu ya kesi hizi bado ndogo. Mtu kenda kumuharibia maisha mtoto mdogo unasikia kafungwa miaka mitatu au miaka saba. Mhe. Naibu Spika, kule anakwenda kuongezwa nguvu tu, hendi kutiwa adabu. Lakini ikiwa kesi hii itakuwa hukumu yake mtu afungwe miaka 30 au afungwe maisha basi na aende hatuna haja naye. Akijua kwamba mimi nikifanya jambo hili nafungwa maisha hafanyi tena, hii hukumu iwekwe hasa kwa sababu wengine pale wanajua kwamba hili suala limeshatokezea, lakini pakawa na mambo mengine ya chini kwa chini, chini ya kapeti mtu huyu pengine atakwenda atafungwa miaka saba, huyu miaka mitatu, huyu miaka mitano hawakomi hawa. Kwa hivyo, mimi naiomba serikali hii hukumu hasa iwekwe kwamba hawa watu wafungwe kifungo cha maisha, tumechoka Mhe. Naibu Spika, na suala hili la udhalilishaji. Mimi Mhe. Naibu Spika, bora niondoke suala hili, kwa sababu nahisa kwamba linaniuma katika nafsi yangu.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza suala hili, niende katika mahakama hiyo hiyo. Mhe. Naibu Spika, kule Pemba tuna kilio chetu ambacho siku zote tunakileta serikalini. Tunaiomba hii wizara ituletee Jaji mmoja Mkaazi kule Pemba, kwa sababu kuna kesi ambazo ni lazima watoke Majaji Unguja kuja Pemba kwa ajili ya kuziendesha, watakapotuletea Jaji Mkaazi, basi mimi naamini hata ile hasara itapungua, kwa sababu katika mwezi mmoja unakuta kwamba wanakuja Majaji

watatu Pemba tofauti. Majaji wale wanatumia tiketi za ndege, Majaji wale watatumia mafuta, Majaji wale tunawakodia mahoteli. Lakini sasa ikiwa kuna Jaji pale pale Pemba basi kesi zetu zitaweza kwenda kwa urahisi bila ya kupoteza pesa nyingi za serikali za kuwaleta Maji wale mara kwa mara kwa ajili ya kuendesha kesi, pia na mahakama zitapungua msongamano wa kesi ambazo zinamtaka Jaji Mkuu. Kwa hivyo, niiombe tena serikali, hata juzi katika siku ya sheria suala hili pia nao waliliomba. Kwa hivyo, sisi tunaomba tena suala la Jaji Mkuu Pemba tuletewe japo Jaji mmoja aweze kutusikiliza matatizo yetu.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, niende katika Ofisi ya Mkemia Mkuu. Mimi naiomba serikali iongeze *expert* katika wizara hii, kwa sababu utakapoongeza mimi naamini ndio wataweza kufanyakazi kwa ufanisi. Kwa mfano, Mhe. Naibu Spika, Pemba katika Ofisi ya Mkemia Mkuu kuna mfanyakazi mmoja tu. Mhe. Naibu Spika, hii inaweza kusababisha hata msongamano wa zile kesi za madawa katika mahakama zetu. Kwa mfano, Mkemia huyo mmoja kuna kesi nyingi sana za madawa ya kulevya. Pale panatakiwa kwamba mtu anapimwa mkojo. Nadhani ni lugha nyepesi hiyo. Sasa Mhe.Naibu Spika, kesi kama hizi akiwa mtu mmoja ndio pale tunaambiwa ule ulikuwa sio mkojo ni maji, au tunaenda kuambiwa ile ilikuwa sio kokeni ni unga wa dona. Wakati mwengine inakwenda kesi ya bangi unaambiwa inakwenda kupelekwa kwa Mkemia Mkuu, mwisho kwenda na kurudi unaambiwa kwamba ule ulikuwa ni mchicha. Mhe. Naibu Spika, sio kweli mchicha hauwezi kufungwa kama vile na vikawa vinauzwa kwa siri, mchicha tunaukuta marikiti.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tunaiomba serikali Ofisi ya Mkemia Mkuu izidishe watu wenye ujuzi huu, ili iweze kuondoa msongamano wa kesi zile ambazo zinakwenda kwa Mkemia Mkuu, na makesi haya ambayo yanamtaka Mkemia Mkuu, mimi naamini kwamba yatapungua hasa kwa upande wa Pemba, naomba tuongezewe wafanyakazi japo watatu ili waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi na katika muda ambao unafaa.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye suala la wastaafu kuongezewa muda. Mhe. Naibu Spika, mimi naiomba serikali itaje kada maalum au fani maalum ambazo zinafaa kuongezewa muda, kwa sababu sasa hivi tunajua kwamba ajira hamna, lakini utakuta mtu mmoja huyo huyo anaongezewa miaka, na ukitizama mtu yule ambaye anaongezewa miaka, kuna watu ambao wamesomea fani zile na wana uwezo wa kufanyakazi zile. Lakini utakuta pengine kwa mapenzi tu binafsi ya mtu yule au uzoefu wake tu ambao alionao

anaongezewa muda. Mhe. Naibu Spika, itakuwa wale ambao wamesoma na wamejitolea kusoma hawafaidiki na hizi ajira.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kwamba serikali itaje kada au fani maalum, na hizo fani zitaje muda maalum ambao upo kwa ajili ya kuongeza. Sio leo anaongezwa miaka miwili baadae anakuja kuongezwa. Mhe. Naibu Spika, wale watakuja kutufia maofisini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende katika Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo. Mimi naishauri serikali katika ofisi hii wakati wa bajeti iongezewe fungu nono, kwa sababu tunaona kwamba mara nyingi sana ofisi hii kila unapokwenda, kwa mfano kama kule kwetu Pemba watu wengi sana wana matatizo ya kukosa vyeti vya kuzaliwa. Lakini kosa hili pia sio la wananchi wenyewe kudharau. Unaweza kwenda ofisini pale mtoto wako umeshamzaa mwezi wa kwanza ukaambiwa njoo mwezi wa nne, mwezi wa nne njoo mwezi wa sita.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu hawana ujuzi wa kujua maana hasa ya vyeti vya kuzaliwa, wakiona kwamba wanapigwa dana dana kama vile basi hawaendi kuvichukua hivi vyeti. Sasa wasipokwenda kuvichukua hivi vyeti vile vizazi vinakuja kupata usumbufu wakati wanapotaka kutumia vile vyeti. Kwa hivyo, mimi naiomba serikali huku katika Ofisi hii ya Vizazi izidishe bajeti yake kidogo ili iweze kukua na waweze wenyewe kufanyakazi zao zile walizopangiwa kwa muda ambao unastahiki..

Nikimaliza hapo Mhe. Naibu Spika, mimi nitowe pongezi tu kidogo. Katika Mkoa wetu wa Kusini Pemba tunaona kwamba tuna Mkuu wa Mkoa mwanamke, Mkuu wa Wilaya mwanamke tunaweza, na katika ripoti hii utakuta kwamba Mkoa wa Kusini Pemba umetumia vizuri mambo yake, pesa zake na umekwenda kwa wakati. Hii ni dhahiri kwamba wanawake tunaweza bila ya kuwezeshwa. *(Makofi)*

Pia niwapongeze wakuu hawa kwa kushirikiana na wananchi mbali mbali kupiga vita juu ya madawa ya kulevya pamoja na udhalilishaji wa kijinsia. Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiwa katika eneo langu la makaazi, watu hawa nashirikiana nao bega kwa bega kama ambavyo ninavyoshirikiana navyo wewe. Nikiwa hapa nitashirikiana na wewe, lakini nikiwa Pemba nashirikiana nao hawa bega kwa bega kupiga vita udhalilishaji. Kwa hivyo, tumuombe mheshimiwa katika sehemu kama hizi kubwa basi atuwekee wanawake, kwa sababu wanajua kwamba wanawake dhiki gani tunazipata na dhiki gani zinatuumiza. Kwa hivyo, mimi niwapongeze kwa kufanyakazi zao vizuri na pia

niwashauri kwamba popote wakati wowote, kukitokea lolote tushirikiane katika kufanyakazi tuko pamoja nao. Naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka Omar, sasa ni zamu ya Mhe. Mohammed Said, anafuatia Mhe. Khadija Kibano na ajitayarishe Mhe. Ali Khamis Bakar.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa imani yako kwa kunipa nafasi na mimi angalau nidokoe japo hizo dakika kumi na tano kuweza kuzungumza machache sana kuhusu Wizara hizi mbili.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwapongeze sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri na wote ambao wamewasaidia katika Wizara hii, katika majukumu yao na wamefanya vizuri sana, lakini moja kwa moja niende kwenye Idara ya nyaraka na kumbu kumbu za taifa. Mhe. Naibu Spika, niwape pongezi sana na kwa kazi ngumu sana niwape pole wafanyakazi wote wa Idara ya Nyaraka lakini hasa wale wa *strong room* wanafanya kazi kubwa, lakini vile vile wana changamoto nyingi changamoto zao hata makabati yale ya kuhifadhia nyaraka zile hawana.

Lakini jambo jengine la umuhimu ningeshauri sana Serikali kuweza kutumia muda mwingi kuwapima afya zao kwa kila mwaka kwa sababu wanatumia kemikali nyingi zaidi, ningeomba tu nitaje umuhimu wa kuhifadhi nyaraka na naomba ninukuu ili watu wajue nini umuhimu wa kuhifadhi nyaraka hizi.

Jambo la kwanza umuhimu wa nyaraka wa kumbu kumbu za taifa sio kwa ajili ya kuhifadhi na kusoma tu bali inalinda historia na kumbukumbu muhimu na matukio ambayo nchi yetu na ushahidi ambao tunaweza kuupata.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe mifano ambayo mikataba mikubwa ya nchi yetu imehifadhiwa lakini na nyaraka hizi ambazo zipo, moja katika hapo ni mkataba wa majenzi wa gati ya Zanzibar kuhusu malipo ya fedha kutoka kampuni ya *GOGEFA* katika mkataba huu kulikuwa na kipengele cha fidia iwapo gati hiyo imepata athari kwa kipindi fulani, sasa tunaona jinsi gani Serikali ilipofaidika na mkataba ule ukatolewa.

Lakini jambo la pili ni umiliki wa jengo la Posta la Kijangwani ambalo liliwahi kudaiwa na Shirika la Posta la Tanzania kwa maadai kuwa inajengwa ka fedha za *East Africa Community* na jengo hili lilikuwa ni jengo la Zanzibar. Sasa nimesema nioneshe angalau mambo mawili na umuhimu huu wa kuhifadhi nyaraka zetu, sasa tuwapongeze sana Idara ya Nyaraka kwa kuhifadhi nyaraka zetu lakini jambo moja ambalo nataka kusema kunaweza kuwa na nyaraka tatu,

nne au aina tofauti. Kuna nyaraka ambazo za mawasiliano lakini kuna nyaraka za ardhi, lakini kuna nyaraka ambazo za usajili hizi zote ndio nyaraka muhimu sana na ukiangalia katika Mawizara yetu mbali mbali tuna nyaraka nyingi lakini zimetupwa zimekuwa *dump* haziwezi kuwekwa sawa.

Ningeomba Serikali kuishauri tu zile nyaraka za Mawizara mbali mbali ambzo zimetupwa ovyo ovyo zikusanywe pamoja na ziwekwe katika Idara ya nyaraka ili siku moja tu ikitoka kama huu mkataba wa *GOGEFA* ukitokeya basi tuweza kuupata.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tuna kamati teule ambayo mwaka jana imeundwa kuchunguza nyaraka ambazo zilipotea, kuna kiongozi mmoja wa ubalozi wa Serikali ya Oman alikwenda akawahadaa wafanyakazi wa mle kuhadaa kwa pesa, kuhadaa kwa rushwa na mengi yaliyotokea. Lakini matokeo yake Serikali ikatumia pesa nyingi na baraza lilitumia pesa nyingi kuunda Kamati teule, Kamati teule ilifanya kazi yake kwa makini zaidi na ikatuletea ripoti hapa Barazani. Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuchukua *hansard* ninayo hapa ya maelezo mbali mbali ambayo matokeo yake ya mwisho Serikali iliunda tume ya watu watano ikiongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje wakati ule Bernad Kamilius Membe, Dkt. Mwinyihaji Makame akiwa mjumbe, lakini vile vile Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni alikuwa Mjumbe walifuatilia vitu vile Oman lakini cha kushangaza zaidi mpaka sasa wananchi kupitia Baraza lao hili hawajapata ripoti ile au Serikali kuleta majibu ndani ya Baraza.

Mhe. Naibu Spika, nitataja ripoti ya uchunguzi wa Baraza la Manispaa ambayo zililetwa ripoti zake humu Barazani, ripoti ya mwanzo ililetwa tarehe 18 April, 2012 Wawakilishi wa wananchi kupitia sehemu mbali mbali walirudisha Serikalini kwa sababu utekelezaji ulikuwa sio mzuri. Lakini ripoti ya pili ililetwa tarehe 29 Januari, 2013 ikarudi tena kwa sababu haikuwa ripoti nzuri, lakini ripoti ya tatu ililetwa tarehe 21 Oktoba 2013 ambayo ilijadiliwa na kwa maslahi mazuri sana ya nchi hii tukapata ripoti yao. Sasa kinachonishangaza na kile ambacho kinanipa ukakasi kwa nini Serikali mpaka leo hawajaleta ripoti ile ndani ya Baraza la Wawakilishi ili wawakilishi wa wananchi wakaweza kuona manufaa yao ya kuunda Kamati Teule na pesa nyingi za wavuja jasho zikatumika pale.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunatumia mzaha mzaha sana na tunatumia pesa za wananchi vibaya sana Mungu atatuhukumu kwa hilo na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kasema tufanye *modality* ya kuwapa labda kwa Kanuni tusiape kwa

misahafu, lakini tukiapa kwa misahafu tutasema kweli hata mkitunyamazisha tutasema tu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba niwape pongezi sana Afisi ya Rais wamefanya kazi nzuri lakini wana changamoto nyingi sana, ofisi yenyewe mbovu, wafanyakazi kidogo wana changamoto nyingi. Ningeomba Serikali na niishauri sana kuweza kumuwezesha kijana yule anafanya kazi muhimu sana anafanya kazi bora, ili basi tuone amefanikiwa katika mambo yake, lakini kila idara ambayo tulikuwa tukiitembelea kulikuwa kuna kitu kikiitwa ufinyu wa bajeti. Mimi nataka nijiulize sana bajeti tunayoipitisha hapa ni bajeti halisia ambayo bajeti ya wananchi wa Zanzibar. Bajeti ile tusahau kabisa kuwa tunapata misaada kutoka kwa wenzetu yoyote yule, lakini nchi yetu ina *opportunity* nyingi sana Serikali itueleze kwa makini sana hivi vyanzo ambavyo tumeviona vya kupatia mapato havifanyi kazi, havituletei mapato yaliyokuwa bora, hatukusanyi vizuri au yanavuja hebu tuambizane halafu tutasema bajeti finyu kila mwaka.

Lakini vile vile hebu tuweze kuiga sasa kama sisi tuna *opportunity* nyingi hapa tuweze kuiga nchi kama Rwanda, kwa nini Rwanda wameendelea, kwa nini sisi tusiendelee ukiangalia *population* yake takriban inafanana au yetu iko ndogo zaidi, watu 1.3 milioni au kuzidi kidogo kwa nini tusiendele mimi nadhani tuweke mpango imara na niwashauri Serikali, kama tutaweza basi tukodi hata *Economist* kutoka nje waje watushauri kwa nini sisi hatuendelei mimi siwezi kusema sasa hivi nchi yangu changa naona aibu. Tangu Mapinduzi tumeshafika miaka 53 bado tuna uchanga.

Lakini tumetembelea Idara ya Mahakama, majengo ya Mahakama Vuga madogo ufinyu na kila kitu lakini leo nimesikia tayari kule Mwanakwerekwe kumeanza kazi, lakini vile vile Pemba Mhe. Naibu Spika, aibu sana Mahakama zetu Pemba mbovu sana hawana pa kukaa Mahakimu wetu, mimi niliwashauri sana Mahakama wakitiliwa *OC* zao angalau watafute ma-*helmet* ya kuwapa Mahakimu, dari mbaya inatisha na huwezi kukaa ndani. Mimi niwashauri sana tunapopata pesa angalau kidogo tukawatengenezee sehemu zile angalau mwanadamu yoyote anapokaa katika mazingira mazuri ya kazi basi anafanya kazi vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye vikosi kwa sababu mwingi sana siwezi kwenda mote dakika kidogo sana, niwapongeze sana vikosi vyote niwapongeze kwa umahiri wao wanavyofanya na nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa, lakini Naibu Waziri tulifuatana mguu kwa mguu kujionea hali halisi ambayo inatokea pale.

Mhe. Naibu Spika, nitaanza Bubwini kwenye kambi ya Chuo cha Mafunzo kama tutaitumia vizuri kambi ile kwa kufanya (*fish farming)* ufugaji wa samaki wale wana eneo kubwa sana, nimuombe sana Mhe. Waziri na hili nimeshawahi kuwambia tunazungumza mimi na yeye *personal* kupeleka angalau kijiko wakaweza kutengeneza mabwawa yale nafikiri pesa za *OC* za kununulia samaki katika makambi yote kila mwezi itakuwa zinafanyia mambo mengine. Lakini kwanza tukubali kutumia pesa ili tuweze kuweka miundombinu imara, mimi niwashauri sana tutumie pesa lakini tuweke miundombinu imara sana na hili linawezekana kwa nini haliwezekani linawezekana.

Lakini jengine nishauri Pemba katika Vyuo vya Mafunzo askari wanapata tabu sana niwape pole sana lakini hata ile kula wanashindwa wakati mwengine wale wanaokuwa kwenye ulinzi, lakini si kula tu Mhe. Naibu Spika, kuna wakati wale tutawalaza kwenye nyumba zao waweze kuwa wamevaa *raincoat* kwa kuwa nyumba zinavuja sana tuwatizame kwa kuwekea katika hali nzuri sana.

Sasa niende kwenye kikosi cha JKU. Kwanza nipendekeze sana wale vikosi vya kule kila mkuu wa kikosi kule Pemba apewe *sub vote* ili aweze kutumia mwenyewe bila ya kupewa s*ub vote* kutumia mwenyewe na kugaiwa tu na Makao Makuu itakuwa haiendi, lakini kama itakuwa tuko *serious* na tunataka tuende basi tufanye hivyo. Lakini JKU kama Msaani tukiwawekea miundo mbinu imara ya kuweza kulima kilimo cha mpunga wa umwagiliaji nafikiri tutapata mazao mengi na tutasahau sasa jinsi kambi zile kuzipelekea vyakula na pesa ambazo tunazowapeleka wanaweza wakutumia kwa mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, ningependekeza jengine kwa hawa vijana wetu kwenye mazingira mazuri sana moja niwaombe Serikali vijana wanafanyakazi kwenye mazingira magumu lakini wanaacha familia zao wanakuwa makambini kwa nini basi Serikali isifikirie kuwapatia bima ya afya, mimi niwashauri sana tuweze kuwapatia bima ya afya wao na familia zao hata wakiwa katika makambi mbali mbali watajisikia wamekwenda vizuri sana, na hata wakiumwa watakuwa hawana *tension* kwa sababu tunaweza kuwapeleka watu Pemba, hakuna makazi wanakaa uraiani siku moja Mhe. Waziri tunaweza tukapata hasara sana mungu atuepushe nayo.

Mhe. Spika, sasa niende kidogo katika Idara ya Zimamoto niwapongeze sana kwa kazi kubwa ambayo wanafanya na tumetembelea sehemu mbali mbali lakini ufinyu wa makaazi ya Idara ya Zimamoto nayo inanipa ukakasi sana, hasa Wete Pemba lakini kile kiwanja ambacho wanacho kwa nini tusiwape vifaa vya kujenga tukawaambia hebu sasa tumieni nguvu kazi na ile dhana ya kupeleka operesheni watu wa hapa wakenda wakahamia kule ili tujenge basi

hilo ingetumika tungepata afya sana. Ukweli makaazi ya askari hawa yako duni sana kila sehemu ambayo tumetembelea lakini nahisi madamu tumezungumza hapa kidogo tutakwenda vizuri, na miundo mbinu hii ambayo tunaijenga kuona wanafanikiwa katika miundo mbinu mbali mbali ambayo nimeitaja tunaweza tukafika pahala tukenda vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilisema nidokoe kidogo kidogo ili wenzangu wapate nafasi nakushukuru sana kwa imani yako, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Khadija Omar Kibano: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kwa kunipatia nafasi hii leo kwa kuchangia na mimi japo kidogo katika ripoti hii. Mimi moja ka moja nitakwenda kwenye masuala ya unyanyasaji na udhalilishaji kwa watoto suala hili ni kubwa kwa wananchi kwa sababu ni watoto wengi wanaodhalilishwa katika jamii, udhalilishaji huu hauondoki nchini mwetu ni kawaida hii imeshazoeleka.

Kwa hivyo naomba Serikali au Wizara ya Wanawake na Watoto kwa kupitia masuala yetu ya udhalilishaji na Mahakama hizi za Watoto, ninachokiomba mimi kwa Serikali huyu atakayefanyiwa tendo hili la udhalilishaji kwa mwanawe ikiwa atakuja katika masuala ya rushwa muhali, huyu azungukiwe yeye kufunguliwa mashitaka. Kwa sababu watoto wengi wanapata udhalilishaji huu kwa kutokana na kuwa wanaofanya vitendo vile vya udhalilishaji wa watoto mimi niliyefanya tendo sihukumiwi anahukumiwa yule aliyekuwa hakufanya tendo, kwa hivyo nataka wale watakaofanya rushwa muhali basi ile kesi iwazungukie wao ili hili suala liondoke.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kuna kesi nyingi sana za watoto za udhalilishaji na wanawake kijinsia ndani ya maeneo yetu, masuala haya katika jamii hayaondoki kabisa tatizo linalotusababisha ni kuwa mimi mwanangu amefanyiwa kosa na mdogo wangu au mjomba wangu mimi namuonea muhali katika kesi nataka kesi ile isiende mbele naona aibu kumshtaki, kwa sababu nitakuwa mimi na yeye tutakuwa hatuzungumzi. Kwa hivyo nataka suala hili lifanyiwe kazi katika masuala ya kuhukumu kesi hizi jaji hapa asione muhali wowote ili amkamate yule mwenye kesi hii.

La pili nazungumzia katika hati miliki za majengo yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, majengo yetu ni kero kubwa sana katika kupatikana hati miliki sijui ninachokiona mimi katika hati miliki maisha mengi tuiyoishi katika majengo haya ya Serikali tuliyomiliki zamani tokea enzi za mababu mpaka leo, hatujui sababu gani inayosababisha ya kuwa hatimiliki hazipatikani

katika majengo haya na ofisi zetu hizi za Serikali. Ni sababu gani Serikali mpaka leo imelala ikiwa yeye ni baba au ni mama wa uzalishaji wa mambo haya Je, leo mpaka sasa hivi hati miliki hizi tutazipata wapi kama hawakuzitoa wao na wakasimamia kidete kutokana na hati miliki hizi. Hasa katika majengo yetu ya Pemba mengi sana ya ofisi hayana hatimiliki hili naliomba Serikali lifungue macho zipatikane hatimiliki za ofisi zetu.

Mhe. Naibu Spika, nikienda suala jengine kwa upande wa Kikosi cha KMKM jamani mpaka sasa hivi magendo ni mengi sana katika majimboni mwetu, kuna bandari bubu zinafanyakazi kwa suala la magendo, mpaka sasa hatujui kinachoendelea katika vikosi hivi, vikosi vya kuzuia magendo naona mimi katika changamoto zao walizozitoa ni kuwa hawana vitendea kazi vya huko baharini ni kidogo sana. Sasa naona hapa katika bajeti yao itakayoingia mara hii ya mwaka 2016/17 naomba Serikali iwasaidie wapiganaji hawa wanamaji ili kupatikana vile vitendea kazi ili kuimarisha nchi yetu na kuondosha usumbufu wa magendo kutoka nchi jirani.

Suala jengine kuhusu habari hiyo hiyo ya hayo magendo kuhusu madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya mimi ninavyohisi kuwa kuna watu wanachukua dawa za kulevya kuzipitisha katika bandari bubu na bandari nyengine hizi za kawaida. Kuna askari wanaovaa nguo za kiaskari hasa kama jeshi, polisi, Valantia, yeye kama atakuwa ana nyota kwenye bandari pale kama patakuwa na mdogo wake anamtolea heshima kutokana na maeneo yetu yalivyo.

Mimi kuna kesi moja ilitokezea katika Wilaya yangu ya Wete, kuna askari mmoja alitoka Bara kupitia katika maboti haya ya wasafirishaji wa mbatata na tungule, alikuwa askari yule kila siku anatoka kuja Pemba anapita njia hiyo. Lakini wakati wa kurudi anarudi kwa ndege. Siku hiyo nikamwambia askari mmoja aliyekuwapo kwenye kituo cha Mhe. Mkuu wa Mkoa, nikamuuliza yule askari aliyepita hapa unamfahamu? Akanambia hapana simfahamu, ah! ni mwanajeshi mwenzangu. Nikamwambia umemmwagia saluti kubwa sana. Nikamwambia yule ni askari anayepitisha madawa ya kulevya, kama unataka upelelezi wake mfatilie huko anakokwenda. Yeye kila siku anapita pale anampigia kishoka.

Sasa sijui kama ni askari wa kawaida, sijui kama ni mtu alikuwa kavaa nguo zake za kawaida, lakini alikuwa akipitisha dawa hizi za kulevya. Yeye akipita pale anampigia kishoka. Kwa hivyo hawa askari na wao wakipita katika masuala ya uchunguzi wachunguzwe sio tuchunguzwe sisi tu na watu wengine, sio wapitishwe mbele kupigiwa kishoka tu, wachunguzwe na wao kwa sababu na wao wana sehemu wanapitisha madawa ya kulevya.

Suala la madawa ya kulevya kwa upande mwengine kama mfano wa vitu vyengine wanamoingiza, wanaingiza katika usafiri wa mafuta haya ya kupikia katika ndoo, wanaingiza katika magunia ya mbatata, magunia ya mkaa hasa katika bandari zetu bubu na zile bandari tulizozifanya kama ni bandari sahihi kama Mkokotoni, Bandari ya Tumbe, Chunga, hizo ni bandari ambazo kuwa zinafanya kazi. Mimi ninachoomba naishauri serikali kutokana na hali hiyo wale watu hata akiwa ana chupa ya chai maji yamwagwe kama chai imo ndani imwagwe, ili kupatikana kile kilichokuwemo ndani. Lakini wenzetu wanatufanyia masuala kama haya ya kupitisha madawa ya kulevya. Kama ni magunia ya mkaa yamiminwe magunia yote ya mkaa zisachiwe wanapitisha vitu kama hivyo.

Nikija kwenye Kikosi cha KMKM kwenye upande wa rada. Serikali mpaka sasa hivi tangu mimi nifahamu *radar* yangu ya Mtambwe, Sengenya ile rada zamani ilikuwa ikifanya kazi, nimeshaisemea hii ni mara ya pili au ni mara ya tatu. Ilikuwa ikifanya kazi sana zamani na ilikuwa ikikamata watu, ikikamata vyombo baharini sana. Ilikuwa ikituendesha Pemba nzima kwa vyombo vinavyotoka nchi za nje kwa kuona usalama wa nchi ya Zanzibar. Lakini sasa hivi *radar* ile mpaka leo sijui serikali kitu gani kilichokuwa hakiwezi ikaifanyia marekebisho ile rada tukapata kuondosha usumbufu.

Kwa sababu sasa hivi tukitizama hali yetu ya nchi ilivyo hujuma nyingi zinapita katika sehemu za baharini, hasa hizi bandari zetu bubu watu wanazishughulikia sana. Hapa kwenye Bandari ya kawaida mtu si rahisi mtu kupita na kitu cha hujuma ni lazima mtu atapitia kule.

Sasa kwa hivyo chombo kikionekana tu kinapita basi tayari wameshaanza kuchunguza na wanapeana taarifa katika maboya yao wanayokaa wenyewe, kwenye yale maaeneo wayoishi askari wa KMKM, kwenye vituo vile. Lakini mpaka sasa hivi chombo hiki katika jimbo la Mtambwe, Sengenya hakifanyi kazi. Naomba serikali ikiwa kuna uwezekano hichi chombo kirejeshwe kifanye kazi kama zamani kama hakuna uwezekano basi serikali itajua wenyewe jinsi gani ya kuamua.

Mhe. Naibu Spika, huo ndio mchango wangu, nashukuru sana na naipongeza ripoti iliyokuja hapa kwa asilimia mia. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi jioni hii ya leo kuweza kuchangia ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala Bora na Utumishi wa Umma. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nitumie

dakika chache sana kwa sababu ni miongoni mwa Wajumbe wa hii Kamati, nimeona ni vyema nigusie gusie kwa sehemu ambazo kama kutilia mkazo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naipongeza Kamati yangu kwa kazi kubwa ambayo tuliifanya ili kuongeza uwelewa juu ya Afisi zetu hizi ambazo zinasimamia serikali kwa upande wa Zanzibar yote nzima. Taarifa hii ni kubwa na imebeba mambo mengi. Kwa haraka haraka nataka nianze Afisi ya Mufti kule Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mufti Pemba ina changamoto nyingi, lakini miongoni mwa changamoto ambazo nimeziona kwa upande wangu ni baadhi ya Maimamu wa Misikiti pamoja na walimu wa vyuo kujihusisha katika masuala ya siasa. Sote ni mashahidi kwamba kuna baadhi ya maimamu wanategemewa sana na wananchi wamepewa kazi hii ya kuwaongoza wananchi katika ibada. Lakini la kusikitisha huongezea yao wakawagawa wananchi wale kwa misingi wanavyotaka wao kwa kutumia lugha mbaya na vigezo vibaya ambavyo vinasababisha uvunjifu wa amani wakati mwengine. Lakini vile vile kuwagawa wananchi katika makundi au vijiji tofauti kwa kisingizio cha siasa.

Mhe. Naibu Spika, niiombe Serikali ya Mufti, Waziri yupo na serikali ipo, hebu tuone kwamba wale maimamu pamoja na walimu wa vyuo ambao wamechukua jukumu hili kuwe na utaratibu maalum ambao utambana imamu yoyote ambaye atakwenda kinyume na sheria ile ambayo imewekwa basi huyo imamu awajibishwe. Kwanza aitwe ashtakiwe ama aondolewe kabisa katika ile kadhia ambayo watu wanaipata.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna walimu wa madrasa wao wamechukua jukumu kubwa. Ni kweli kwamba hali hii inapelekea mpaka wale wanafunzi hawapati ile haki yao ya msingi, mwalimu yupo lakini wanafunzi wanashindwa kusoma kwa sababu tu eti labda pengine ni wa upande fulani na wale wa upande fulani. Kwa hivyo naiomba serikali walimu hawa wa madrasa ambao wamebeba hili jukumu na jukumu lenyewe ni zito ambalo linasaidia kuwaondosha wanafunzi ambao hawapati haki yao ya msingi. Mimi naomba sana Afisi ya Mufti kule Pemba iangalie hili ili wanafunzi hawa wapate haki zao za msingi na yule ambaye atagundulikana akionekana kwamba anaingiza masuala ya siasa basi hatu za kisheria zichukuliwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini pamoja na Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake-Chake. Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini hii tumeona kwamba kuna changamoto nyingi lakini miongoni mwa changamoto ambazo nimeziona moja wapo ni ukosefu wa gari lake la Mkuu wa

Mkoa ambalo ni chakavu, halina hadhi ya kupanda Mkuu wa Mkoa kwa sasa hivi ni bovu hata ile kwenda katika kwenye harakati zake za serikali kusimamia majukumu yake wakati mwengine inampelekea kuweza kukwama njiani.

Lakini vile vile Mhe. Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya wa Chakechake wote wawili hawana sehemu ya makaazi yaani nyumba bado mpaka leo wanakodi majengo ya watu binafsi na kama tunavyoona hali ya siasa ambayo ipo, inawezekana majengo haya wanayokodi hatujui kama ni ya wafuasi wa upande wao au ni upande mwengine. Lakini ni jambo ambalo kiukweli haipendezi kwa wakuu wetu kama hawa kuwaona mpaka leo hawajapata sehemu maalum ya kuweza kukaa pamoja na familia zao, tukiangalia wao ni viongozi wakuu. Naiomba serikali sehemu zetu tunazo nyingi za ardhi pamoja na baadhi ya majengo, basi tuangalie tu tuwahamishie katika majengo yetu maalum ambayo yanatumika na serikali ili kuweza kupata na wao kukaa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi (B) Unguja. Sote ni mashahidi, ingawa tatizo hili baadhi ya Wizara nyingi tumekwenda majengo yao ni mabovu, hayatoshi, ufinyu umekuwa mkubwa kwa baadhi ya majengo mengine au afisi kuwemo na afisi nyengine. Lakini Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi (B) haina hadhi, haifai kabisa maana nataka niseme hata sehemu ya kuwekea magari ukenda unashindwa hujui wapi uliweke. Lakini vile vile tukizingatia pia kuna wenzetu ambao ni watu wenye ulemavu, mtu anakwenda pale wengine ulemavu wao ni wa kutambaa, pana mawe, ile njia haipitiki siku za mvua ilimradi ni mtihani, yaani ufika pale tope zimezagaa. Mimi naomba sana serikali ipo na Waziri yupo basi waangalie ni sehemu gani za kuifanya ile Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi (B) iondoshwe ama atafutiwe mazingira mazuri ya kuweza kukaa.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije kwenye suala zima la wenzetu wa Vikosi, mimi nataka niwataje kwa pamoja ingawa kuna changamoto nyingi lakini kati ya kadhia ambayo tumeigundua katika sefari yetu hii ya Kamati, ni kukosa hati miliki ya zile sehemu ambazo ni za wapiganaji wetu. Sehemu hizi ambazo kuna kambi mpaka leo Serikali yetu ambayo ni ya Mapinduzi ndiyo ambayo inasimamia harakati zote za maofisi yote, nashangaa mpaka leo kwamba kuna hizi kambi zetu zikiwa zinafanya kazi ndani ya Serikali na serikali ni yetu ambao wanatoa hati miliki ni watu wenye serikali na wizara zipo, nashangaa mpaka leo kwamba watu hawa hawajapatiwa hati miliki katika yale maeneo ambayo yamejengwa kambi.

Mhe. Naibu Spika, ukifika kwenye zile sehemu zao kuna mitihani tele, wananchi yale maeneo wanayavamia, wengine wanajijengea ovyo. Jambo

ambalo halipendezi kwa kambi zetu. Wale wapiganaji wetu kuna mambo mengine ni siri wanatakikana pale wakae na wapate mapana ya kukaa katika ile sehemu ili wanapokuwa na shughuli zao za kiserikali au za wao wenyewe binafsi kama za kiaskari iwe hakuna raia anayejua kwamba pale pangine kuna askari wangapi au kuna kitu gani cha siri ambacho kimeingia au kimetokan na mpaka leo bado haijakaa vizuri. Kwa hivyo naiomba sana serikali iliangalie hili kwamba zile hati miliki za maeneo yetu ya hawa wapiganaji wetu ya hizi kambi, basi zipatiwe hati miliki kadri itakavyoonekana inafaa.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nije katika suala zima la ushirikishwaji wa bajeti. Tumekwenda katika Kamati tulipofika baadhi ya viongozi wanalalamika wakati wa bajeti wao hawashirikishwi katika zile bajeti zinazopangwa hapa. Naiomba serikali na Wizara yote nzima ikiwa Waziri yupo, kile kipindi cha kuweka majumuisho ya pamoja kuhusiana na habari ya hizi bajeti, basi na wale viongozi wa Pemba waitwe kwa sababu wao ukisema tu kwamba labda tuwafikirie pengine fungu hili litawatosha kumbe wewe unaweza ukarafikiria kuwapa milioni 2 kumbe walikuwa wanahitaji 5. Kwa hivyo washirikishwe na wao walete malalamiko yao, waangaliwe. Najua bajeti wakati mwengine inakuwa inamtihani lakini kile kinachopatikana na wao vile vile wafikiriwe.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilisema nataka nitumie muda mchache kutokana na kwamba Mwenyekiti wangu ameshawasilisha yote ambayo tuliyazungumza na kwa bahati nzuri nashukuru sana mengi yameshasemwa na bado na wenzangu wanahitaji kuchangia. Mimi nimalizie tu Mhe. Naibu Spika, kwa kuipongeza Kamati yetu kwa jinsi tulivyofanya kazi vile inavyotakikana.

Vile vile nimalizie kwa upande wa vizazi na vifo kwenye habari ya vyeti.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia, dakika moja nakupa ulikuwa umeshamaliza naona unarudia tena.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kunakadhia kubwa kwa upande wa vizazi na vifo. Mara nyingi tunapofika pale hupata malalamiko ya wananchi juu ya vyeti vya kuzaliwa. Niiombe sana wizara na hili nalo ni changamoto kubwa juu ya wananchi, iangalie majukumu yao lakini vile waangalie na wananchi jinsi gani ambavyo wanahangaika katika hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda tulionao ni mdogo sana, kwa hivyo nitakaowataja ambao ndio watakaomalizia watatumia dakika kumi,

kumi ili tuweze kuwapa Mawaziri wanaohusika na Wizara hizi na wao waweze kuchangia na baadae tumpe mwenyekiti kwa ajili ya kufanya majumuisho. Mchangiaji wa mwanzo atakuwa ni:

Mhe. Abdalla Maulid Diwani atafuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na baadae tutamalizia na Mhe. Mhe. Suleiman Makame Ali. Ahsanteni.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, wizara mbili. Kabla ya yote mbele yangu nina Katiba ya Chama cha Mapinduzi naomba kunukuu ahadi za mwanachama ibara ya 8 ya kwamba:

"Nitasema kweli daima, fitna kwangu mwiko".

Ibara ya 9, "Nitakuwa mwanachama muaminifu wa CCM na raia mwema wa Tanzania na Afrika".

Nimetanguliza maneno haya kwanza ili iwe kinga kwa upande wangu. Kwa sababu imekuwa kila mara unaposimama ukaikosoa serikali au ukaieleza serikali basi unaambiwa wewe mpinzani, wewe sijui umetumwa, wewe sijui umefanya nini, Katiba ndiyo inayonielekeza hivyo, kuwa nitasema ukweli daima na fitna kwangu mwiko na nitakuwa mwanachama muaminifu wa CCM mpaka nitakufa sibadiliki.

Baada ya hapo niwapongeze kwa dhati kabisa Wajumbe wa kamati hii kwa kazi yao nzuri waliyoifanya na hadi hii leo kutuletea ripoti yao Barazani muda huu tunauchangia. Mhe. Naibu Spika, nisipoteze muda niende kwenye ukurasa wa 3 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa. Imekuwa ni nyimbo ya muda mrefu, upotevu wa nyaraka za SMZ tulisema mwaka jana na narudia tena katika ripoti hizi, tunataka ripoti yetu ya ukaguzi ya Tume tuletewe tuone, serikali imetumia pesa nyingi sana kuwapeleka watu Oman kwenda kuzitafuta hizi nyaraka. Tuombe Mungu mambo yaende hivi hivi yakijakubadilika tutakujakuambiwa keshokutwa mtu atakuja na nyaraka atasema hata Ikulu yake itabidi tumpe. Watakuja Karimjii watasema hata Hospitali ya Mnazimmoja ya kwao tuwape, kwa sababu zile nyaraka ndio zimeibiwa hazipo wanazo wao.

Sasa naiomba sana Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nyaraka muelekeo wake tupewe, tusibaniwe siyo *time* ya kufichwa sasa hivi, tuambiwe nyaraka zetu ziko wapi na kwa nini zimefika huko. Kwa hivyo kama ambavyo walivyotangulia kusema wenzangu

tumetumia pesa nyingi sana kuziunda hizi Kamati au hizi Kamati kwenda kuzitafuta, kwa hivyo ripoti ije isomwe tusipigwe dana dana katika hilo.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye ukurasa wa 7 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Awali niipongeze kwanza kwa kufanya kazi vizuri pamoja na changamoto walizokuwa nazo ya maslahi na masuala mengine. Lakii *CAG* hiyo hiyo nayo ina malalamiko. Kuna ubadhilifu wa *CAG* kutoka Idara ya Vikosi yaani KMKM na Wizara ya Fedha wakishirikiana na *CAG* kwa kutengeneza malipo ya viinua mgongo hewa. Kuna ripoti au kuna fedha zilizokuwepo kutoka Wizara ya Fedha kukagua hili kitu 2015/16, bado haijapatikana na 2013/14 kuna fedha hizi zimepotea. Hapa. *CAG* lazima wawajibike tujue namna gani atwambie hizi fedha zimekwenda wapi. Fedha za wafanyakazi hewa ambao watu wametengenezewa viinua migongo sio vya kweli. Hilo suala linajulikana na hivi sasa Wizara ya Katiba na Sheria bado inawabembeleza watu hawataki kuwasimamisha kazi.

Kuna watu tulivyosema hapa kwa Wizara ya Fedha mbio walisimamishwa kazi na mpaka leo wapo hawajijui kamati imeundwa na leo hii ile kamati imeshavunjwa, lakini bado mustakbali wao mpaka dakika hii haijatokea hatma yoyote kama wamepelekwa Mahakamani wana makosa au hawana makosa. Wizara sasa hivi inapiga mguu kwamba wasimamishwe. Wale nani hawa nani tunaomba sana kujua hilo. Hii nchi ni yetu sote, isiwe wengine wakaonekana bora wengine wakaonekana sio bora.

Naiomba sana Wizara najua kwa ukamilifu wake hili suala watalichukua na kulifanyia kazi. Kwa kweli inaumiza fedha nyingi sana za Wazanzibari nyaraka zipo huo ubadhirifu uliofanyika, hata akitaka ziletwe tutafanya utaratibu tutazileta, ili kuthibitisha kwamba ni hizi. Kwa sababu tunachosema sisi hatutoi kwenye vichwa vyetu tunafanya utafiti na tunagundua haya mambo. Kwa hivyo naiomba sana wizara katika hiyo iwe na jibu la kuzungumza je, hizi pesa ilikuaje na kwa nini ikawa watu wakafika kutengeneza wafanyakazi hewa leo hii wakalipwa hizi pesa zikapotea bure katika Serikali yetu ya SMZ. Tunapiga kelele hatuna pesa lakini pesa kuna wachache wanazifanyia ujanja ujanja.

Nitakwenda katika ukurasa wa 11 Mkurugenzi wa Mashtaka na udhalilishaji, wenzangu walizungumza kwamba Mkurugenzi wa Mashataka kuna matatizo, kweli mwenyewe anasema si kweli. Kuna kesi nyingi za udhalilishaji pale ushahidi wake kidogo una matatizo, kuna mambo yamefanyika *red handed* hasa mpaka *video clips* zipo lakini mpaka dakika hii hakuna ndio kwanza inaundwa Tume nyengine ya kuchunguza yale eti isiende Mahkamani. *Video clips* zipo tena ushahidi gani mwengine unatakiwa pale ambao unaonekana hiki

kitendo kimefanyika. Leo hii imeundwa Tume ya Kamati tano kwamba kujadili lile suala limefika vipi mpaka liende Mahkamani, naona bado kuna ubabaishaji katika Mkurugenzi wa Mashtaka. Naiomba sana watimize wajibu wao hili tatizo kwa nchi yetu, ikawa kila siku ya Mungu tunakuja humu tunazungumza udhalilishaji tunapeleka kesi zetu kwa Mkurugenzi wa Mashtaka lakini zinaishia pale pale zinaambiwa hazina ushahidi, kesi hazendi mbele, inaumiza sana. Nategemea hata tunawapa kichwa hawa wengine wasiofanya na wao pengine waingie hamu ya kufanya hayo ambayo yasiyotakiwa. Kwa sababu *at least* ingekuwa watu wanapelekwa Mahkamani na wanafunwa ingeogopesha kidogo, lakini ikipelekwa pale kesi imelaliwa watu wanaona kawaida kawaida kwa hivyo inazoeleka.

Kwa hivyo nasema niende haraka haraka dakika zenyewe 10 muda hautoshi nitakwenda tena katika suala la Tume ya Kurekebisha Sheria. Tunajua kwamba bado ziko sheria mpaka dakika hii zinakandamiza, nathubutu kusema kwamba kuna sheria hii ya kuongeza muda waajiriwa katika miaka 60 inaumiza. Kuna vijana wetu wengi sana wanasoma wana-*graduate* vyuo vikubwa vikubwa lakini hawapati nafasi za kupewa kazi kwa sababu tu ya watu ambao wameshafika umri wa kustaafu washafika miaka 60 lakini bado unaongezwa miaka miwili, miwili hujafanya kazi huko mwanzo kijana utafanya kazi sasa hivi miaka 60.

Jamani ikifika *time* mlete sheria kwamba tuondoe sheria hii kandamizi kwa vijana. Vijana kundi kubwa sasa hivi ambao ni wakati wake wa kufanya kazi hawana fursa hiyo kwa kubebana bebana. Imeshafika *time* ya kustaafu pengine ana ukaribu na mtu fulani basi anazungumza anaogezewa muda ili aendelee inatuumiza katika kundi la vijana. Vijana tuko asilimia 63 muda wetu wa kufanya kazi ni sasa sio mtusubiri tushafika miaka 40 ndio mtupe ajira. Mtu kafika miaka 60 ende zake hizi sheria tumezitunga wenyewe. Haiwezekani sheria zinafika mtu miaka 60 tena anaanza kubembeleza anapewa tena nafasi ya miaka 2, hata tarishi, dereva, jamani tunafanya nini. Tutakuwa tunasema ajira hakuna lakini ajira hizo zimekaliwa na baadhi ya watu.

Nitakwenda tena katika suala la Ofisi ya Mufti, wenzangu walisema kudharauliwa kwa Ofisi ya Mufti. Sisi wazanzibari kudharauliana tumezoea. Chombo kikubwa kama hiki cha Baraza la Wawakilishi, Wawakilishi na Wawakilishi wanadharauliana iweje tena Wizara isidharau Wizara nyeziwe. Ni kweli dharau zimekithiri, kuna kesi imetokezea hapa karibuni Mufti katoa maelekezo, maelekezo yale yalipingwa ilionekana si lolote si chochote kwa maslahi ya watu tu. Sasa sijui taasisi hizi ambazo zote ziko katika SMZ zinafika kudharauliana katika kitu kama hicho. Kuna kadhia ya mtoto

kutoroshwa inajulikana na kila mtu humu ndani na sote mashahidi. Tunataka kuizungumza kadhia ile ikafika time tukaambiwa kwamba imepelekwa Mahkamani isizungumzwe mnatufumba midomo. Kwa kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, ifike *time* watu waheshimiane hasa hizi taasisi zetu nyinyi ndio walezi kwa upande wetu sisi tulioko *back bencher*. Lakini leo hii taasisi na taasisi za Serikali hii haziheshimiani sijui nini tunafanya, kwa kweli mnatupa wakati mgumu sana tutafika lakini.

Niende katika Manispaa ya Mjini, kwanza nimpongeze Mkurugenzi Aboud Serenge kwa kazi yake nzuri sana anavyofanya. Lakini malalamikio yangu mimi makubwa katika suala hili juu ya wale vijana wake pale Malindi ambao ninafikiri wanajiita Polisi Jamii. Sasa hivi ninafikiri wanavuka mipaka juu ya suala zima la kufunga magari pale barabarani gari iko kwenye njia kuu inafungwa jamani tunaonekana sisi sote wendawazimu haiwezekani. Naomba sana Wizara izungumze na wale vijana angalau wawe na heshima kidogo. Pale ndio mlango mkuu wa kuingia Zanzibar, time ya saa 9 vinapokuja vyombo kutoka Tanganyika au kutoka Tanzania Bara au kutoka Pemba unakuwa msongomano mkubwa.

Leo hii mtu kafanya kosa kidogo unakwenda kumfungia gari kati kati ya barabara nini unamaanisha, ina maana unazidisha msongomano zaidi. Kwa hivyo tunajua utaratibu lakini zisimamiwe katika hicho, ninajua ukizungumza suala hili mwenzangu Mkurugenzi analichukua najua kwamba ni makini sana baada muda si mkubwa atalifanyia kazi. Ni kweli tatizo lipo kwa wale vijana ambao wanafanya kazi pale Malindi ambao wanajiita Polisi Jamii wa Mji Mkongwe ina matatizo. Matatizo hayo yashazunguzwa sana si mara moja si mara mbili na yataendelea kuzungumzwa hatunyamazi katika hili mpaka tunaona kwamba tunanyooka.

Mwisho, si mwisho kwa umuhimu wake nizungumze suala la Mrajis wa Vizazi na Vifo, wenzangu walisema kuna tatizo juu ya upatikanaji wa targisi za kuzaliwa, malalamiko haya yapo muda mwingi sana na mimi mwanzo nilivyoanza kukera nikaambiwa limehamishwa katika utawala bora liko Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Tatizo lipo Mhe. Waziri hili suala tunaomba liende *up to date* angalau mtoto anapozaliwa basi ndani ya mwezi mmoja, miezi 2 apate ile targisi yake.

Kwa sababu ile ndio uthibitisho wake tosha kwamba wewe ni Mzanzibari, leo inafika watu mpaka miaka 3 hawajapata vyeti vyao, kuna wa miaka 2 hawajapata, tukija huku tunaambiwa karatasi hakuna, karatasi zimechapishwa zimechelewa ninawaombeni sana mambo yenye uwezo ambapo tunajua

kwamba yatatumia pesa kidogo kwa ajili ya huduma za wananchi basi tuipeni kipa umbele. Haya mengine ya pesa nyingi sawa lakini kama suala la karatasi za kuzaliwa iwe tatizo unapokwenda pale utakuta mtu anatoka shamba kufata pale anakuja mara tatu, mara nne, mara tano, nauli anapoteza nauli zake tumuonee huruma, mnyonge anatoka Tumbatu au anatoka Matemwe anakuja pale ni shida.

Kwa hivyo, nasema ahsante sana Mhe. Spika, baada ya hayo machache niliyosema naunga mkono ripoti hii. Ahsante.

Mhe. Hussein Ibarahim Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ndani ya Baraza lako Tukufu tuko salama ninashukuru kwa afya pia niipongeza ripoti ya Kamati hii kwa ripoti nzuri, Kamati ya Sheria Utawala na Idara Maalum, kwa kweli wamefanya kazi nzuri.

Pongezi za dhati kabisa nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Machano kwa ripoti yake nzuri hajaficha kitu, ripoti hii ni mfano kwenye Baraza hili, yaani mambo yote yamewekwa wazi kabisa hakijafichwa chochote humu tumepata kujua wajumbe mambo mbali mbali ambayo yanatendeka katika nchi yetu. Lakini lengo, madhumuni, changamoto ni kuitatua hii changamoto aliyoiandika Mhe. Mwenyekiti, Mungu akujaalie upeo mkubwa na umakini wako.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwenye ukurasa wa 8 katika sehemu ya Mahakama. Mahakama ni moja katika mihimili muhimu sana katika nchi yetu, kila mwananchi apate haki kwa mujibu wa sheria. Kwa kweli hili suala ni muhimu na hasa Mahakama inatoa haki pande zote mbili kwa mtuhumiwa na aliyekuwa hajafanya hatia. Kwa hivyo mimi naomba sana hili suala la Mahkama ukiangalia kwenye ripoti ya Kamati imeeleza, kuna ongezeko kubwa la kesi za ubakaji yaani imeeleza wazi ongezeko linaongeza kila siku ubakaji. Tangu miaka mitatu ya mine ya nyuma au mitano hali hii inaendelea na inazidi na wewe Mhe. Naibu Spika, ulikuwa pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii unaijua hali hii ilivyo vizuri sana. Kwa hivyo mimi sitoridhika na hali hii inayoendelea kila siku kila ukiangalia hapa naona inaongezeka.

Mimi juzi juzi kwenye mitandao ya jamii niliona habari mtoto mmoja wa miaka 3 kabakwa mpaka kafariki, ili kusoma ile habari imenishinda nikaiacha, mtoto mdogo wa miaka 3 anafanyiwa hujuma mpaka anafariki. Huyu bado anatembea mitaani na bado mzima Mahkama au Serikali anakwenda kwenye vyombo vya ushahidi anaambiwa ushahidi haujakamilika. Hapa hapataki ushahidi, jambo kalifanya wananchi wameona wanajua yule afungwe tu, yule

sio mtu yule ni kama mnyama mimi nasema. Kwa kweli hili halitaki ushahidi iliobakia ni kufungwa tu na kuja hapa kila siku ushahidi, ushahidi tutakwenda wapi. Mimi naomba Mhe. Naibu Spika, tuangalie sana.

Pia kuna uhaba wa Majaji tukiangalia Pemba majaji 6 tatizo kubwa ni nyumba. Mimi naomba Mhe. Naibu Spika, suala la nyumba watafutiwe hawa majaji wapatikane hasa Pemba kuna matatizo makubwa ni nyumba. Mimi naomba Mhe. Naibu Spika, suala la nyumba watafutiwe hawa majaji zipatikane hasa Pemba kuna matatizo makubwa, wapewe japo nyumba kwanza wajishikize kwanza hawa majaji wetu wafanye hizi kazi, kesi zimekuwa nyingi tangu kipindi sisi tumekwenda Pemba Kamati kesi ziko nyingi. Mpaka leo unakuta majaji wako Unguja mpaka wapande boti wende wakahukumu warudi tatizo nyumba, mimi naona hatujawa *serious* tuwape nyumba wafanye kazi wazihukumu hizi kesi.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia suala la mashine bado hatuna mpaka leo za *DNA* haya yakitokezea tunakuwa hatuna upimaji. Kwa hivyo mimi naomba sana hii mashine pia ipatikane. Ukitizama Mkoa unaongoza kwa mambo haya Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa nyuma katika ripoti niliyosoma Mkoa wa Kaskazini, sasa hivi Mkoa wa Kusini, kwa sababu adhabu hamna kama wakipatikana watu 5 wakifungwa mambo haya yatakwisha.

Mhe. Naibu Spika, niseme haraka haraka kidogo nina mambo mengi kwa hivyo niende kwenye ukurasa wa 8 kifungu namba 3 kuhusu madawa ya kulevya. Jana nimezungumza suala la madawa hapa, nimezungumza kidogo lakini ningeomba niongelee tena. Suala la kesi ya madawa ya kulevya, hapa kwenye ripoti ya kamati mimi nampongeza sana Mhe. Mwenyekiti, kaandika ripoti na Mwenyezi Mungu atakulipa atakusaidia kwa kazi uliyoifanya.

Niseme kuwa ripoti ya Kamati imesema halipo katika ngazi ya Mahkama wao hupokea taarifa kutoka kwa Mkemia Mkuu. Sasa Mkemia Mkuu ni kama wakala na kuapa atoe taarifa kule, ije kwa Mkemia Mkuu, Mkemia Mkuu apeleke Mahkamani, sasa Mahkama inakuwa haina nguvu hii sheria ibadilike Mhe. Naibu Spika, haraka iwezekanavyo. Hapa inakuwa wakala Mkemia Mkuu, Mkemia akisema huyu hajafanya kitu kwa ndio hamna kesi yoyote. Kwa hivyo mimi nasema kwa ripoti hii lazima sheria tubadilishe haraka iwezekanavyo tuweze kuwapa Mahkama nguvu ya kufunga na kuwapa adhabu hao wanaofanya makosa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano ukitizama Jaji kama alivyosema hakuna jaji wa kudumu hakuna kabisa kwa hivyo kesi zinazidi kukaa na kuwa

hazishughulikiwi na nikenda katika ukurasa wa 11 suala pia la uingizajiwa dawa za kulevya na utumiaji kesi kumalizwa kwa rushwa Mheshimiwa jana nimesema lakini leo Mwenyekiti kasema, kesi za madawa ya kulevya zinamalizwa kwa rushwa ndani ya ripoti hii imezungumzwa, ripoti imesema mimi ninampongeza Mwenyekiti sana kuandika ripoti hii anasema waziwazi kesi ya madawa inamalizwa kwa rushwa hakuna njia nyengine. Wewe ukiuza madawa leo ukenda Mahkamani ukitoa punga pale milioni ishirini unaachiwa madawa yanaendelea.

Jambo jengine ukitizama ripoti hii imeandika wazi tena Mhe. Machano ninakushukuru sana, Polisi wameandika humu Polisi kuchangia kuharibu kesi hizo mambo yako wazi tunapewa ripoti wazi tunataka nini tena. Kama Mwenyezi Mungu keshatwambia mambo yote ndio haya kesi za madawa humalizwa na rushwa ni kweli, kesi za madawa zinamalizwa na Polisi wenyewe wanazimaliza wanazichangia kuziharibu kesi hizi, ripoti ipo sijasema mimi Ripoti ya Kamati. Sasa Mhe. Naibu Spika, tunakwenda wapi mambo yote yapo wazi na Polisi kama mpo mnanisikia nazungumza ripoti ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi, wajumbe wote mnayo ripoti hii mambo haya yapo.

Mhe. Naibu Spika, naendelea haraka haraka ninajua muda unakwenda ukitizama hapa pia kwenye ripoti pia ya Kamati ukurasa wa 18 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa, Kuhujumu Uchumi, kuwepo kwa uhaba Mhe. Naibu Spika, pia uhaba wa fedha, kuwepo kwa uhaba wa bajeti kwa chombo hichi pia hawana fedha kuzuia rushwa, huwezi kuwalaumu sana hawa kwa sababu wanakuwa wenyewe fedha hawana. Kwa hivyo naomba Serikali isaidie hawa waingiziwe fedha waweze kufanya majukumu yao kwa uhakika.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 28 Baraza la Manispa, hapa pana muingiliano mkubwa wa kodi Mhe. Naibu Spika. Ukitizama *ZRB* wanataka kodi hiyo hiyo, ukitizama *TRA* wanataka kodi hiyo hiyo, ukitizama Mamlaka ya Mji Mkongwe wanataka kodi hiyo hiyo. Mhe.Naibu Spika, hapa tuwe wazi, hili tatizo pia changamoto ipo hapa ukitizama Zanzibar *ZRB* ni chombo kinachokusanya kodi ndio chombo chetu, ukitizama *TRA* ipo hapa japo fedha za *TRA* hazendi Bara kwa mfumo wa sasa hivi muungano ulivyo lakini *ZRB* ni chombo maalum cha kukusanya kodi, wapewe nguvu hawa *ZRB* kwa sababu leo unakwenda kulipa *ZRB*, kesho unalipa *TRA* una risiti mbili tofauti. Wakati Bara unaweza kulipa sehemu moja yote ni *TRA* moja.

Sasa *ZRB* mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, hawa watu wanafanya kazi hata hisi mafao yetu wanatulipa hawa *ZRB*. Ukitizama juzi nilikuwa natoka Dodoma mimi kufika *airport* nakuta *ZRB* Kamishna na watu wake wapo

airport pale wanalinda mapato, kwa kweli niliwapongeza na niliwaonea huruma sana Kamishna mwenyewe yuko pale anatizama mapato yanapotea, anatizama anachunguza ili kuona yasipotee. Ninampongeza sana kuwa hawa jamaa wanafanya kazi vizuri sana

Lakini pia nimpongeze Mhe. Haji Omar Kheri Waziri anafanya kazi kubwa sana nimpongeze sana. Ukitizama sasa hivi kuna deni Manispaa wanadaiwa fedha nyingi sana. Manispaa wanadaiwa na *ZECO* lakini na *ZECO* wenyewe wamesema jana wanadaiwa bilioni 124 na Tanesco kweli mtihani mkubwa sana. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri sasa hivi anatia taa za solar jana nimepita usiku Darajani taa zinawaka za *solar* mji unan'gara. Mhe. Waziri anafanya kazi nzuri, Manispaa kwa kujitahidi kutia hizi taa za *solar* kupunguza hata ile nguvu ya umeme kuwa hautumiki sana. Pia nimpongeze kwa zile juhudi zake za kufanya mji wetu una *CCT Camera*. Kwa kweli sasa mji huu utakuwa unapendeza hata watalii watakuwa na uwezo wa kutembea kwa sababu utakuwa na *camera*. Hawa *ZTE* wanatusaidia wafadhili na Mhe. Waziri uwe nao vizuri hawa jamaa wanatusaidia sana na mji wetu na *camera* tuweze kufanya kazi na watalii waweze kuja wengi kuweza kutembelea hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe.Haroun kwa kazi yake kubwa ile Tume ya Maadili ya Viongozi, mimi niipongeze sana. Nasema hivyo kwa nini mimi nimejaza Tume ya Maadili ya Viongozi wa Baraza la Wawakilishi, nimejaza Tume ya Maadili ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lile jambo la kujaza mali zako ni jambo zuri. Sisi wanasiasa tumechaguliwa na wananchi tumekuja kwa kutuamini, leo ukiwa wewe mwanasiasa lakini una fedha huzijui unazipata wapi, hujui una majumba umeyapata wapi, lazima ile Tume ya Maadili ijue mali zako uwe msafi. Mimi silalamiki na napongeza hili suala la Tume ya Maadili kila mwaka liendelee.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono. Ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Sheria ya Utawala Bora na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niwapongeze wajumbe wa Kamati au Kamati kwa ujumla chini ya Mwenyekiti wake Mwakilishi mzoefu Mhe. Machano Othman Said kwa kuongoza Kamati hii vizuri, lakini pia Mhe. Naibu Spika,

niwapongeze Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba na Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake, dada zangu hawa kwa kuhakikisha kwamba wanawaelewesha wananchi ndani ya Mkoa ule na ndani ya Wilaya ile kwamba nini lengo la Serikali. Niwape pongezi hizi, Mhe. Naibu Spika, nathubutu kusema kwamba hawa wanahitaji kutunukiwa nishani kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Ofisi ya Mufti. Ofisi ya Mufti ndio kimbilio letu sisi waislamu lakini hapa wakati mwengine hutokezea mambo kusema la ukweli yaliyokuwa hayastahiki kufanyiwa kama ile Ofisi kudharauliwa, kuna mambo mengi wanadharauliwa hata kufaya baadhi ya watendaji wakakosa imani kabisa.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la *DPP*. Mhe. Naibu Spika, kuna kesi nyingi ambazo zinafanywa lakini hazipelekwi kwa *DPP*, ukiangalia kama kipindi cha nyuma badala ya kumaliza uchaguzi kumetokezea mengi sana hususan kule Pemba, watu kunyanyaswa, kudhalilishwa na wengine kupigwa hadi misikitini, lakini ukitizama kesi zile hazifiki popote kwa sababu hazikupelekwa kule baadhi ya kesi nyengine kupelekwa kwa *DPP*.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Tume ya Maadili. Hapa ndio penye kishindo Mhe. Hussein Ibrahim alizungumzia kwamba kila kiongozi wa umma anastahiki kujaza fomu hii. Lakini Mhe. Naibu Spika, ninathubutu kusema kwamba kuna baadhi ya wengine nathubutu kusema kuwa wana majumba hata kuyajua wenyewe hawayajui lakini sifikirii kama wameyaorodhesha kwenye Tume.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Mamlaka ya Kuzuia Rushwa. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa ni taasisi ambayo ni muhimu sana katika nchi kwa sababu rushwa ni janga la taifa lakini nathubutu kusema nao hawa wakati mwengine huvunjwa moyo. Kuna kesi moja ilitokea kwenye hoteli ya Iyana kule Pemba watu wa rushwa wakamkamata jamaa yule aliyehusika na kesi ile wakampeleka kule kunakohusika kule Mahkamani lakini labda kulitokea mtu tu, kesi ile haikuendelea tena ikafika mpaka wale wafanyakazi wa Zaeka na wao tayari wakabidi kwamba kuvunjika moyo wakanitafuta na wakanipa haya malalamiko kwa hiyo Mhe. Naibu Spika kwenye suala hili nalo liangaliwe vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nende kwenye masuala ya wakfu Mhe. Naibu Spika wakfu nayo ni chombo muhimu sana ni taasisi muhimu sana lakini ukiangalia nayo wakfu kwamba nao ndio wanaotoa haki badala ya kutizama ile misingi yote, taratibu zote washakamilisha huyu haki yake apewe, huyu haki yake ni hii basi kusema la ukweli hutokezea pale wakanyimwa haki yao wale waliokuwa

hawana nguvu hawana uwezo ni baadhi ya watu waliokuwa kidogo tu wenye nafasi zao kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika na hili kusema la ukweli linadhalilisha sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika twende kwenye nende kwenye masuala ya utumishi serikalini Mhe. Naibu Spika hapa nithubutu kusema kwamba ile Tume ya Utumishi Serikalini kusema na ukweli iko haja ya kufanyiwa marekebisho, ipo haja kubwa ya kufanyiwa marekebisho au ikiwezekana ivunjwe kabisa iundwe nyengine *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nende kwenye masuala ya hapo hapo kwenye Tume ya Utumishi mfanyakazi kuwekewa miaka 60 kufanya kazi kusema la ukweli ni mtihani mkubwa, miaka 60 inafika mpaka yeye mwenyewe akishastaafu akakosa kukaa na familia yake kuhudumia vizuri na kuishughulikia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo niunge mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Miraji.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi naanza kwa kushukuru kwa kunipa nafasi ya dakika 5 na nitajitahidi nitumie nne ili moja niiache kwa kazi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niunge mkono hoja kwa ripoti hii kwa Mwenyekiti mwenzangu Machano Othman Said lakini pia nianze na mchango katika eneo moja la Mahkama, Mahkama na SAG kwa ujumla naongea maeneo ya kiutumishi kuna wafanyakazi wa Mahkama tuliwahi kuzungumza katika bajeti katika kipindi cha upitishaji wa bajeti tulizungumza suala la watumishi wa Mahkama ya mwanzo na hao walifuatana na ile ahadi ya Mhe. Rais ya kuyaona mazingira yao siku mkutano wa *Law Day*, na akasema atashughulikia suala la mafao yao.

Lakini bado mahakimu hawa hawajapata marekebisho ya mishahara yao sasa kupita kwa ripoti hii tumeipitia zipo changamoto zimeonyeshwa lakini changamoto hasa ni mahakimu ambao wanafanya kazi kubwa sana tukiwa bado hatujaanza kuwafikiria ni tatizo. Lakini eneo hilo hilo la kiutumishi wafanyakazi wa ofisi ya *CAG* tulizungumza pia kipindi cha bajeti nao walikuwa na mazingira magumu wanafanya kazi kubwa kwa sababu watumishi hawa ndio wanaokwenda kuwakagua wahasibu wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Lakini ukitazama mhasibu yule ambaye anafanya kazi ya matumizi ya fedha kisha baadae zile *document* alizozifanyia kazi wanapita hawa watumishi wa *CAG* kwa kuzifanyia kazi na kuzitolea ripoti, lakini pia kuushauri utekelezaji mzuri wa matumizi ya fedha. Wafanyakazi hao hawapati stahiki nzuri kazi wanafanya kubwa kwa sababu mlingano wa kazi zile huyu anatumia huyu anamkagua *document* ziko sawa majukumu yanakingana basi tukashauri kipindi cha bajeti wafikiriwe na haya lakini changamoto hiyo imejitokeza tena katika ripoti hii ya Mwenyekiti. Nakushukuru sana Mhe. Machano Mwenyekiti wa kamati hii kuiona bado inaendelea niiombe serikali waweze kuwasaidia watumishi hawa kwa mazingira yao magumu.

Mhe. Naibu Spika, lakini mwisho naomba niende katika eneo la Mamlaka ya Serikali za Mikoa. Eneo hili nazungumzia hasa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya ambao wao kwa mujibu wa sheria ni wenyeviti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa nchi yetu wanamsaidia Rais katika maeneo yao. Viko viashiria vinatolewa na baadhi ya viongozi na wananchi wa nchi hii, viashiria hivi vina upotoshwaji kwa wananchi wetu, ziko kauli zinatoka kwa baadhi ya viongozi wa nchi hii ikiwa wastaafu au viongozi ambao walitumikia serikali. Kuna eneo hili la kuonekana kesho nitapewa Urais, kesho itakuwa hivi, kuna wananchi wanahamasika, kesho nitaapishwa, vitendo hivi vinatokea ndani ya Mikoa ambao wanaishi hawa wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama. Sasa hatuwezi kuwaachia tu viasharia hivi kila siku vikiwa vinazidi iko siku hii nchi itakuwa haiishi katika mazingira salama. Sasa niwaombe wenzetu Wakuu wa Mikoa sheria zipo za nchi hii wazitumie vizuri hawa ambao wanatoa matamshi haya ni sehemu ya kuhatarisha sehemu ya ulinzi na usalama wa Mikoa yao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika nakushuru kwa kunipa dakika tano naunga mkono kwa asilimia mia moja hii ripoti ya Mhe. Machano.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa wajumbe bado tunawachangiaji au watu waheshimiwa mawaziri wawili wanaohusika na wizara hizi ambao watakuja kujibu baadhi ya maswali pamoja na kufanya majumuisho.

Lakini vilevile tuna Mwenyekiti wa Kamati ambaye naye pia atakuja kwa ajili ya kufanya majumuisho na kuwashukuru waliochangia wote. Kwa kuwa muda wetu tumebakisha dakika kama ishirini nitamuomba Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atuongezee muda ili tuweze kumaliza shughuli yetu hii ya leo ya kamati hii, Mhe. Waziri karibu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika nakushukuru, kwa kuwa shughuli iliyo mbele yetu bado inahitaji muda zaidi ili kutoa nafasi kwa waheshimiwa wajumbe kuendelea kutoa michango yao, lakini pia kwa waheshimiwa mawaziri waweze kuelezea baadhi ya hoja ambazo waheshimiwa wajumbe wamezitoa na pia kutoa nafasi kwa mwenyekiti kufanya majumuisho ya hoja hii. Kwa sababu muda uliobaki ni mdogo naomba tuweke kanuni ya muda kando, ili tuweze kukamilisha shughuli iliyo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Sasa nimpe nafasi Mhe. Haroun Waziri wa Katiba na Sheria aje kwa ajili ya kujibu baadhi ya maswali. Mheshimiwa karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia hadi saa hizi kuwa na afya njema, pili nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kutupa nafasi hii adhimu kabisa ya kutoa ufanunuzi wa mambo mawili matatu tu ambayo yemejitokeza kimsingi.

Sababu waliowasilisha hoja ni Mwenyekiti wa Kamati kwa hivyo mambo yote atayamaliza yeye lakini kwa ujumla nataka nipongeze sana wachangiaji wote waliotochangia hapa leo michango yao ni mizuri na kwa kweli inatia moyo sana, kuona kwa jinsi gani wanaofanya utafiti na kwa jinsi gani ambavyo wanavyoifanyia kazi ripoti ambayo imewasilishwa na Mhe. Mwenyekiti wetu.

Kwa ujumla mimi upande wangu nimeridhika sana na jinsi michango yao ilivyokuja. Nashukuru sana na nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii ya

Katiba, Sheria na Utawala pamoja na kamati nzima Mhe. Machano Othman Said na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri walioifanya na kwa kweli imetufikisha hapa ambapo tumefika leo kupata ufanisi huu nashukuru kwa pongezi zake.

Mambo ya ujumla ambayo yamezungumzwa kwenye ripoti hii ambayo ndiyo nitajikita zaidi kwenye ripoti hii na yale mengine ambayo yamejitokeza sio kama tutayadharau lakini nayo yatakuwa na wakati wake tutakuja kuyawasilisha lakini kwa leo tutajikita zaidi na ripoti ya Mwenyekiti. Lakini kwa ujumla kuna masuala ya kimsingi yamezungumzwa hapa, suala la hasa hali ya Mahkama zetu ni ucheleweshaji wa kesi kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, wizara yetu kwa kushirikia na taasisi ya Mahkama napenda niwahakikishieni kwamba tumejiandaa vizuri sana na sasa hivi Serikali tayari ishatenga eneo maalum Tunguu kwa ujenzi wa Mahkama mpya kubwa ya kisasa itakayokidhi mahitaji. Mahkama ya Mwanakwerekwe tayari imeshafanyiwa inaendelea kufanyiwa ukarabati hivi karibuni na nyengine zote *in shaa Allah* tukijaaliwa zitafanyiwa ukarabati. Lakini ucheleweshaji wa kesi hii unatokana na sababu mbali mbali na *DPP* hapa vile vile nizungumze kabisa kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka inaonekana kama labda kwamba kesi zinacheleweshwa.

Tatizo sio kucheleweshwa kwa kesi tatizo ni upatikanaji wa ushahidi lakini napenda niwaahidi waheshimiwa wote humu pamoja na wote waliochangia suala zima la udhalilishaji wa watoto na kujinsia kwamba hivi sasa *DPP*, Polisi, Mahkama wamejipanga nakuhakikishieni *in shaa Allah* katika siku mbili tatu zijazo tutaanza kuona mabadiliko makubwa yatakayochukuliwa katika hatua hizo. Suala la udhalilishaji nakuhakikishieni kwamba litaondoka kabisa hapa katika nchi yetu kwa sababu kamati nzima imejiandaa vizuri ya *DPP* yaani Muendesha Mashtaka, Mahkama na Polisi wamejipanga vizuri pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na sisi wizara yetu tunahakikisha kwamba tunalisimamia vizuri. Kwa hivyo, nawatoa wasiwasi kabisa kuhusu suala hilo.

Pia kulijitokeza suala zima la kuimarisha Ofisi ya Mdhamini Pemba, hivi sasa tunajenga jengo jipya kwa kushirikiana na wizara nyengine Wizara ya Fedha, Tawala za Mikoa jengo jipya kabisa la kisasa na wale wote ambao wanabananabanana kule *in shaa Allah* tukijaliwa watapata jengo zuri la kisasa. Kwa hivyo, tuwe na subira kidogo.

Suala la Tume ya Utumishi tumesikia ushauri tunauchukua matatizo yao mbali mbali yapo lakini kweli kuna baadhi ya matatizo tutayaangalia na ile sheria

tutaiangalia. Lakini pia limezunguzwa suala la Nyaraka, Nyaraka hali yao si nzuri kule wanavyosema hasa wale wasomi, hasa Mhe. Dimwa alizungumza kwa nia nzuri kabisa ya kuona hali halisi ya kule ni kweli wanaumia ninashukuru kwenye ripoti imeandikwa angalau tunawapa posho lolote, tunawapa kweli ili ziwasaidie kutokana na afya zao, na tutachukua juhudi kila mwaka tuwapime afya zao ili waendelee kupata matibabu mazuri. Pia tutaangalia kwa vizuri zaidi ili kuhakikisha kwamba maslahi yao nayo tunayangalia vizuri hilo ni la uhakika na jambo zuri.

Lakini pia naomba nichukuwe nafasi hii kuzungumzia suala zima la ucheleweshaji wa kesi tatizo la ucheleweshaji wa kesi nalizungumza, nishalizungumza nalizingumza tena hapa kwa sababu limezungumzwa hata karibu na waheshimiwa wote hili linatokana na kwamba ushahidi haupatikani na mwananchi anapoambiwa njoo utowe ushahidi hatowi lakini sasa kutokana na sheria mbazo tulizipitisha humu na ndani ya Baraza Mheshimiwa nashukuru sana waheshimiwa kwa sheria ile ya ushahidi iliyopitishwa humu ndani haitotusumbua sana tujaaliwe ushahidi ule utapatikana kwa njia ya *electronic* na tusiwe na wasi wasi mabo yote yatakwenda kwa utaratibu mzuri na serikali imejipanga vizuri.

Kuhusu Jaji kupelekwa Pemba mpaka sasa hivi hatuoni tatizo na lakini Mahkama bado inahisi kwamba kumpeleka Jaji Pemba mpaka sasa hivi haijaona haja hiyo, kwa sababu kwa mfano katika kipindi hiki cha miezi mitatu hii kesi za jinai zilizopatikana ni nne tu. Sasa naona kumpeleka Jaji kumuweka kule ni hasara kubwa, lakini tu tuwe na subira bado Taasisi yetu ya Mahkama imeomba uwezekano wa kuajiri wengine *inshaallah* tukipata ziada ya Majaji hatutokuwa na sababu yoyote kwa nini tusimpeleke Jaji Pemba hakuna tatizo lolote.

Kuna waheshimiwa wamesema kwamba ile *machine* ya *DNA* tuiharakishe tatizo lilokuwepo hapa wala si *machine* ya *DNA* tunaweza tukapata *machine* ya *DNA* kwa sababu hii *machine* ya *DNA* inafanywa na mwanadamu vile vile na huyu mwanadamu anaweza huyu huyu akasema hakuona dalili zozote kwamba kuna ushahidi fulani. Kwa hivyo suala la kimsingi ni kubadilika kitabia sisi sote jamii yote ibadilike na wawe tayari kutoa ushahidi pale unapohitajika.

Lakini *DNA* inaweza kuwepo na bado vitendo vikaendelea mimi ninachosema tujitahidi sisi wenyewe kuelimisha jamii zaidi kwamba wanapoambiwa wakatoe ushahidi basi waende wafanye haraka sana. Kuna suala zima la *rare profession* ambazo zimezungumzwa na mikataba ifanywe lazima. Kada maalum hizi amabazo zinatolewa mikataba ni zile kada ambazo utaalamu wake

unakuwa si rahisi kupatikana kwa mtu mwengine haraka sana kwa hivyo, ndio maana wake tunawapa mikataba. Lakini suala hili la kuongeza muda liko mikononi kwa mwenyewe Mhe. Rais. Sasa anapohisi kwamba iko haja Rais ana mamlaka haya yakufanya anapohisi ipo haja basi, anatoa *extension* ile na mambo yanakwenda.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima limezungumzwa hapa la ubadhirifu wa pesa katika Ofisi ile ya Kadhi kuhusu bahati ya mfanyakazi aliyefanya, nataka niwahakikishe waheshimiwa kwamba hatua zimechukuliwa mfanyakazi nimemsimamisha kazi na tayari sasa hivi tunachuka hatua nyengine kubwa zaidi. Kwa sababu tumemsimamisha kazi anapata nusu mshahara na hatua zaidi zinachukuliwa pamoja na nyengine ambazo ni mapema mno kuzisema humu, mambo mengine bado tunaomba tuyaweke siri kwa sababu tukiyatoa yote hapa yatakuwa si barabara.

Mhe. Naibu Spika, na nyengine ambayo napenda kuzungumza suala la serikali mtandao hili Mheshimiwa tulifanya semina na ni juzi tu tumefanya semina kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tumeshawafanyia kuhusu serikali mtandao. Lakini inaelekea bado tunahitajia kutoa taaluma zaidi *inshaallah* tutajitahi kutoa taaluma kwa jamii yote Unguja na Pemba ili waweze kuelewa vizuri zaidi. Kitengo chetu hiki cha rushwa tutakiimarisha na tutakiwezesha kiwe na uwezo mkubwa zaidi. Lakini pia suala la IPA lizingatie watu wenye ulemavu nalo Mwenyekiti katika ripoti yako tutalizingatia vizuri sana.

Mwisho naomba nizungumzie suala zima la mashirikiano Mheshimiwa, sisi Wizara ya Katiba na Sheria tunapenda sana kushirikiana na popote pale ambapo watahisi kuna jambo zito limejitokeza la kuisaidia serikali au wizara liwe la udhalilishaji au jambo jengine lolote basi naomba sana watuletee taarifa hizi haraka ili tuchukue hatua za kufaa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nashukuru sana na nikutakie kila la kheri namtakia kheri Mwenyekiti wangu kwa kazi nzuri aliyoifanya namshukuru sana nawashukuru waheshimiwa wote. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa Mhe. Haji Omar Kheir.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa kuchangia Hotuba ya Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati, ili niweze kufanya uchambuzi au kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo ambayo waheshimiwa wajumbe wameyazunguza. Kwa mujibu wa utaratibu wetu nitatolea ufafanuzi

maeneo machache sana kwa sababu ripoti hii sisi kama serikali tunakakiwa kwenye kikao cha mwezi wa Septemba au Oktoba tuje na mrejesho wa yale yote ambayo yameandikwa ndani ya ripoti hii.

Lakini kwa sababu waheshimiwa wajumbe wameeleza baadhi ya mambo nadhani ni vizuri tukapata muda wa kuweza kutoa ufafanuzi, na mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pamoja na kamati nzima kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum na nameonesha ushirikiano mkubwa katika kuja kufatilia utendaji wa serikali niwapongeze sana Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ.

Lakini pia nichukuwe nafasi hii kuwapongeza wajumbe wote ambao wameelezea baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza katika ripoti na yale ambayo hayakujitokeza lakini wameyaamua watuzindue ili tuweze kuyafanyia kazi, wajumbe wote kumi na nne ambao wamechangia kwenye ofisi yetu nao niwapongeze sana kwa moyo wao.

Mhe. Mwenyekiti nianze moja kwa moja kutolea ufafanuzi juu ya suala la udhibiti wa ukusanyaji wa mapato na utoaji wa huduma bora kwenye taasisi zetu hizi za Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti lazima nikiri kwamba ukusanyaji wetu wa mapato sasa hivi tunakwenda kwa utaratibu wa *manual*, katika mwaka ujao wa fedha Serikali za Mitaa zote tunataka tuhakikishe kwamba zinakusanya mapato kwa kutumia utaratibu wa kisasa wa *electronic*. Kwa hivyo, tukifanya hivyo tutaweza kudhibiti makusanyo na kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo lilizungumzwa na Mwenyekiti wa Kamati ni suala la Masheha ambao uwezo wao mdogo. Naliomba Baraza lako tukufu wawe wastahamilivu hivi sasa tuko katika hatua za mwisho za kuhakikisha kwamba tunateuwa Masheha wale ambao tunawahisi wanafaa, na wale ambao tunahisi wamefanya kazi zao vizuri basi tutaendelea kuwa nao na wataweza kuitumikia serikali hii.

Changamoto ambazo zimejitokeza ambazo zimezungumzwa na waheshimiwa wengi akiwemo Mwenyekiti wa Kamati ni suala la maslahi ya wapiganaji wetu wa vikosi maalum au Idara Maalum za SMZ. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba ahadi ya serikali kupitia Mhe. Rais wetu iko pale pale kwamba mwezi wa Aprili watumishi wote watakapoengezewa

mishahara yao na wapiganaji wa vikosi vya SMZ watapewa maslahi mazuri kama Mhe. Rais alivyoahidi.
Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine ambayo imejitokeza ni suala la vitendea kazi na suala la miundombinu ya wapiganaji. Vitendea kazi pamoja na *uniform* jambo hili limezungumziwa, nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Mwenyekiti wa Kamati kwamba serikali jambo hili la *uniform* kwa wapiganaji wetu imeshaliamua vizuri na hivi sasa liko katika hatua za mwisho za utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni tu imetoka timu ya serikali ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Idara Maalum za SMZ, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Makamanda watatu wa vikosi kwenda safari kwa ajili ya kukiimarisha Kiwanda cha Idara Maalum kilichopo Amani na kukiimarisha Kiwanda cha Viatu cha KVZ kilichopo Mtoni. Serikali imeshaamua kutenga fedha maalum ndani ya mwaka huu wa bajeti kwa ajili ya kuimarisha viwanda hivyo viwili ili *uniform* za wapiganaji wetu ziweze kupatikana kwa urahisi. Tayari tumeshafanya mazungumzo na kuingia mkataba na kampuni moja kutoka nje kwa ajili ya ku-*supply* vitambaa ili *uniform* hizo ziweze kupatikana na askari wetu waweze kuondokana na matatizo hayo.

Mhe. Naibu Spika, suala la miundombinu pia nalo serikali inalifanyia kazi, hivi karibuni tu tunatarajia wizara zetu mbili, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tutapita kwenye kambi na kituo kimoja kimoja cha wapiganaji wetu ili kuona uhalisia wa miundombinu iliyopo ili bajeti ijayo ya mwaka 2017/2018 serikali ilizingatie kwa umakini na kuweza kuimarisha miundombinu iliyopo katika idara zetu maalum. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe bajeti yetu itakapokuja ya mwaka 2017/2018 basi niwaombe watuunge mkono ili serikali iweze kutekeleza azma yake ya kuwajengea mazingira mazuri wapiganaji wetu na hayo yamezungumzwa na Mwenyekiti pamoja na wajumbe wengine.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa ni suala la uchakavu wa rada katika kituo chetu cha Sengenya. Mimi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba serikali inalitambua jambo hili na tutahakikisha kwamba jambo hili linafanyiwa kazi, hata hivyo, kwenye baadhi ya vituo vyetu vyengine huduma hii inapatikana. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe wasiwe na wasi wasi na kadhia hii bado nchi iko salama na adui popote anapotokezea sisi tunamdhibiti kwa sababu tunamuona.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo limezungumzwa na Mwenyekiti na wajumbe wengine ni suala la *sub vote* za Idara Maalum kule Pemba. Mimi

nadhani tukubaliane kwamba utaratibu uliopo sasa ndivyo hivyo, lakini suala hili tutalichukua tukae na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili waweze kulifanyia kazi na waweze kuona umuhimu wa kufanya hivyo. Pale tu Wizara ya Fedha na serikali kwa jumla itakapokubaliana na wazo hili basi sisi hatuna matatizo ili kuweza kuondosha tatizo hili.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa kama nilivyosema mengine tunayachukua tutakwenda kuyafanyia kazi sitaweza yote kuyatolea ufafanuzi. Lakini jambo lilozungumzwa ni suala la wafanyabiashara wa usiku pale Darajani. Nadhani Baraza la Manispaa imezingatia jambo hilo na kwa sababu limezungumzwa naomba nimuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba hili nitalichukua ili niende nikalifanyie kazi nijue hasa tatizo lao nini. Lakini bado biashara hizo zinatakiwa zizingatie utaratibu wa sheria ili zisiweze kuchafua mazingira na uhalisia wa Mji wetu.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu suala la vyeti vya kuzaliwa. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tumeulizwa masuala mawili yanayohusiana na suala hili, kwa hivyo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wastahamili majibu yake yapo, serikali itayaleta na itayajibu na wataweza kuelewa nini kinachoendelea. Kabla ya Baraza hili kumalizika majibu hayo yatatoka kwa sababu tayari ofisi yangu imeshawasilisha majibu hayo hapo Barazani. Kwa hivyo, mimi nikiambiwa kesho, mimi na Naibu wangu tuko tayari kuyajibu, lakini Baraza hili halimaziki majibu tutayatoa. Kwa hivyo, waheshimiwa mliouliza leo subirini majibu yenu tutayatoa kuhusu kadhia ya vyeti vya kuzaliwa.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa kuhusu bandari bubu. Nataka niwahakikishie kwamba ofisi yangu kupitia Ofisi za Ulinzi na Usalama za Mikoa tayari tumetengeneza utaratibu maalum na mkakati maalum kuhakikisha tunazitambua zote bandari bubu na kutafuta namna ya kuweza kuzidhibiti bandari hizi.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa kwamba baadhi ya wapiganaji tuwafanyie uchunguzi kwa sababu wasiwe wanachunguzwa raia tu. Nasema hakuna askari ambaye yuko juu ya sheria, kama atakuwa amefanya kosa basi atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa ni kuhusu suala la Ofisi ya *DC* Magharibi “B”. Mimi nimuombe Mhe. Mwakilishi jambo hili ndani ya Baraza hili, ndani ya wiki hii tumetoa jibu. Nadhani mheshimiwa yeye ndiye aliyeuliza

kwa hiyo mimi nadhani aridhike na majibu yale kwa sasa hivi hatuna majibu mengine zaidi ya yale.

Vile vile nataka nipokee pongezi za uwekaji wa *CCTV camera* ambazo zina kampuni mbili za utekelezaji. Kampuni ya *ZET* na Kampuni ya *Room Solution*. Waheshimiwa Wajumbe, naomba hili tutakapokuja kwenye bajeti yetu tutakuja na taarifa kamili juu ya utekelezaji wa mradi huu. Kwa hivyo, sasa sitakuwa na maelezo mengi yakuzungumzia suala hili.

Jambo la mwisho ambalo nataka nilizungumzie leo ni kuhusu viongozi wanaoashiria upotoshaji wa wananchi na kujiita yeye labda ni Rais. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, sote tuliomo humu ndani na wananchi wa Zanzibar kwa jumla wanajua kwamba Dkt. Ali Mohammed Shein ndiye Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa mujibu wa Katiba yetu ya 1984 Rais anatawala kwa kipindi cha miaka mitano, na huyo anayesema anawafanya mazuzu tu wafuwasi wake. *(Makofi).*

Kwa hivyo, mimi niseme kwamba ni sawa sawa na Komandoo mwaka 1993/95 alipokuwa anamwambia huyu jamaa kwamba wewe ukitamani urais, huyu akitamani urais anakwenda kwenye kioo anavaa joho, anajiangalia, anajiona yeye kama Rais. Rais nchi hii ni Dkt. Ali Mohammed Shein na yupo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na sheria ya Tume ya Uchaguzi ndio iliyomtangaza Dkt. Ali Mohammed Shein kuwa Rais. Sasa aliyekuwa haamini kwamba Dkt. Ali Mohammed Shein ni Rais aende Mahakamani, kama anavyosema mwengine. (*Makofi*)

Lakini juu ya suala la upotoshaji na viashiria vya kuvunja amani bado tunasema serikali haitishwi wala haijejewi. Serikali itachukua hatua stahiki kuhakikisha yeyote yule ambaye anavunja sheria anachukuliwa hatua za kisheria. Nadhani Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama wamewasikia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakitoa maoni yao. Sasa nadhani wao wenyewe watakwenda kulifanyia kazi jambo hili na hakuna ambaye yuko juu ya sheria yoyote ambaye anavunja sheria basi atachukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niipokee ripoti hii ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ. Ahsante sana, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Machano Othman Said: (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum) Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na uhaki jioni hii ya leo. Lakini pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kufunga hoja yangu hii.

Mhe. Naibu Spika, lengo langu sio kujibu hoja kwa hoja kama waziri, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati mengi yao tunayachukua kwenye kamati kuyafanyia kazi. Lakini pia, nitatoa kidogo ushauri wangu kwa Waheshimiwa Mawaziri ili waweze kuendelea na ile *speed* yetu ya kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya wachangiaji ni 31, waliochangia kwenye jukwaa ni 15 na waliochangia kwa maandishi ni 16. Sasa walau basi niwataje majina ili kila mmoja aonekane kama kachangia.

Wale ambao wamechangia kwa moja kwa moja ni:

1. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
2. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
3. Mhe. Simai Mohammed Said
4. Mhe. Ali Suleiman Ali
5. Mhe. Abdalla Ali Kombo
6. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
7. Mhe. Mohammed Said Mohammed
8. Mhe. Khadija Omar Kibano
9. Mhe. Ali Khamis Bakar
10. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
11. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
12. Mhe. Suleiman Makame Ali
13. Mhe. Miraji Khamis Mussa
14. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora
15. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Panya Ali Abdalla
2. Mhe. Ali Juma Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
3. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
4. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
5. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
6. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
7. Mhe. Salma Mussa Bilal

8. Mhe. Ame Haji Ali
9. Mhe. Said Omar Said
10. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
11. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
12. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
13. Mhe. Shehe Hamad Mattar
14. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
15. Mhe. Bahati Khamis Kombo
16. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla waheshimiwa wote wamechangia kama mambo matano makubwa. Kwanza wamezungumzia suala la udhalilishaji watoto na wanawake, hili waheshimiwa wengi wamelipiga vita sana na wameitaka serikali ichukue hatua kama ilivyopendekezwa na kamati kwamba serikali nayo tunaiomba ichukue hatua kama kawaida.

Pili, wamezungumzia matatizo ya nyaraka kwamba Ofisi ya Nyaraka, kwanza hawana vitendea kazi, lakini *strong room* ya nyaraka nayo ina matatizo na baadhi ya waheshimiwa kama watatu wanne wakazungumzia ripoti ya upotevu wa nyaraka. Sasa mimi nataka kusema, sisi kamati tunawaomba waheshimiwa katika kikao cha Septemba Mhe. Waziri atuletee ripoti ya Kamati ya Upotevu wa Nyaraka. Ni vikao vya kawaida ambavyo tutafanya kazi na tutapata muda mzuri haya maagizo yetu kwa kamati tutayafanyia kazi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora hili ni moja ambalo ni agizo la kamati kwamba mwezi wa Septemba wakati wa kamati ripoti hiyo tuipate.

Pia wajumbe kwa ujumla walizungumzia udhaifu katika mamlaka zetu za Halmashauri za Mitaa ikiwemo Manispaa, na wengine waliomba kwamba Manispaa mpya zisaidiwe sana kwa sababu hazina miundombinu mizuri, lakini pia kwa Halmashauri zote ukosefu wa mapato ya kutosha kwa hivyo hili nalo Mhe. Waziri nafikiri tutakutana tena katika suala hili.

Vile vile wajumbe walizungumzia Mahakamani ucheleweshaji wa kesi, wajumbe wengi walizungumzia hili na adhabu ndogo kwa wabakaji. Kuna mmoja alitoa mfano kwamba hapa kwetu Zanzibar mbakaji anafungwa kati ya miaka mitatu na saba. Ni kweli na wenyewe Mahakimu wamekiri kwamba ndio mwisho wa uwezo wao, lakini tunaomba serikali iandae kurekebisha sheria walau basi twende kati ya miaka 30 mpaka kifungo cha maisha. Wenzetu Bara wanakwenda katika kifungo cha miaka 30 mpaka kifungo cha maisha.

Suala la Jaji Mkaazi Pemba nafikiri hili halina mjadala tulikuwepo sisi wengine katika ufunguzi, au baada ya uzinduzi wa jengo jipya la Mahakama ya Chake Chake, Jaji Mkuu alimuahidi Mhe. Rais kwamba watapeleka Jaji Mkaazi Pemba. Kwa hivyo, tunataka serikali itekeleze hili ili Jaji Mkaazi Pemba apelekwe hata kama una uchache wa Majaji.

Waheshimiwa wengine walizungumzia kuhusu maadili kwamba fomu za maadili zina mambo mengi zaidi kuliko hata zile za Muungano, kuulizwa mkeo *account* yake vipi, mume wako ana *account* gani. Ndio kwanza tumeanza hii Mamlaka au Tume, kwa hivyo lazima kutakuwa na marekebisho kila muda ukienda. Wameona changamoto na nina hakika watazifanyia kazi.

Lakini pia, waheshimiwa walizungumzia jinsi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inavyopata tabu na mikataba ya serikali. Na hili sisi tuliliona na mwenyewe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wamelisema kwa hivyo tmatarajio kwamba Mwanasheria Mkuu atakaa na Mawaziri na Makatibu Wakuu ili kuwa na mikataba inayoeleweka ambayo kwa manufaa ya nchi yetu. Na tunaiomba serikali pia iongeze wafanyakazi kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, wana kazi kubwa, kazi muhimu kwa nchi yetu na wanafanya kazi mpaka muda wa ziada sana. Kwa hivyo, serikali tunaiomba ifanye kazi vizuri.

Ofisi ya Mufti nayo ikae na walimu wa madrasa waheshimiwa wengi wamezungumza hilo lipo tatizo kwa walimu wetu wa madrasa baadhi yao huchipuka na vijana wetu na kutoa imani kwa wazazi. Kwa hivyo, na hili nalo Ofisi ya Mufti tunaiomba itekeleze lakini pia bajeti ya Ofisi ya Mufti nayo iongezwe.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla haya ndio ambayo yamezungumzwa sana, lakini pia waheshimiwa wamezungumzia juu ya maslahi kwa vikosi vyetu na vitendea kazi kwa vikosi vyetu. Tunamshukuru sana Mhe. Waziri kaliahidi Baraza kwamba tayari wanayo changamoto hiyo na tayari wameshapewa agizo na Rais kwamba wapite kikosi baada ya kikosi kuangalia nini mahitaji na serikali ikae kati ya serikali kuu na wizara wakae kwa pamoja waangalie jambo gani litawasaidia katika kuimarisha vikosi vyetu.

Waheshimiwa tuna bahati sana vikosi vyetu vyote vitano vimefanya kazi nzuri sana na sote tunaridhika na kazi waliofanya vikosi kama sio wao nafikiri hata humu ndani tungelikuwa hatukai vizuri, wamefanya kazi vizuri sana. Lakini kama alivyosema mwenyewe mtu akifanya kazi vizuri mcheza kwao hutunzwa, kwa hivyo na vikosi lazima vitunzwe na kwa bahati nzuri hakuna mjumbe hata mmoja aliyelaumu utendaji wa vikosi vyetu.

Mhe. Naibu Spika, bima ya afya ni muhimu nayo na sio bima ya afya tu na ile pia kuwa na mfuko wao wa kustaafu *ZSSF* yao peke yao askari itengenezwe hata kama tutapitia mfuko ule ule w *ZSSF* watengewe dirisha lao maalum ili waweze kufaidika baada ya kustaafu. Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wote, Wajumbe wote wametupongeza na sisi tumepata moyo sana wa kufanya kazi hii, tunatarajia kwamba tukiwa hai na uzima mwakani tutaandaa ripoti nzuri zaidi. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum nakushukuru na nakupongeza sana hasa kwa kuwatetea vikosi vyetu na kama alivyosema Mhe. Ali Suleiman Ali sote tunalala salama ndani ya majumba yetu kwa ajili wao wanafanya kazi vizuri. Nawapongeza hata na mimi.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwaulize Mhe. Mwenyekiti ameshatoa ripoti wanaokubaliana na ripoti wanyooshe mikono, wanakataa, wanaokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mpaka hapa tumemaliza shughuli yetu kwa leo niwashukuru sana kwa utulivu wenu lakini niwashukuru wale wote ambao wamechangia pamoja na Mawaziri kwa kuchangia pamoja na kutoa ufafanuzi wa mambo mbali mbali ambayo yanatekelezwa na serikali. Waheshimiwa Wajumbe, sasa naahirisha shughuli hii yetu ya leo mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:58 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 23/02/2017 saa 3:00 asubuhi)